ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 06 Juni, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika,(Mgeni Hassan Juma) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa heshima kubwa naomba kuweka hati mezani ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2016/2017. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 78

Tatizo la ukosefu wa Ajira

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza**:**
Ukosefu wa ajira ni miongoni mwa Changamoto za nchi zinazoendelea ikiwemo hapa kwetu Zanzibar, hali hii inapelekea vijana wengi kuzurura mitaani baada ya kumaliza masomo wakiwemo wale wanaofaulu vizuri .

(a) Ni nini hasa sababu za ukosefu wa ajira hapa nchini kwetu.
(b) Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili.
(c) Kwa nini Serikali imekuwa ikiwapatia mikataba ya mara kwa mara wafanyakazi wanaomaliza muda wao wa utumishi kuendelea kuwemo katika ajira ya Serikali wakati vijana wengi na wenye ujuzi wanazurura mitaani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, ukosefu wa ajira ni miongoni mwa changamoto kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Zanzibar. Changamoto hii, pamoja na mambo mengine, inachangiwa na sababu zifuatazo:-

Mhe. Naibu Spika, uchache wa nafasi za ajira serikalini ikilinganishwa na idadi ya vijana wanaohitimu masomo kila mwaka:

- Bado sekta binafsi hapa Zanzibar haijakuwa ya kutosha kuweza kutoa ajira kwa vijana wetu.

- Halikadhalika vijana wengi bado wana mtazamo kwamba ajira ni serikalini tu, hivyo kutotumia fursa zilizopo kuweza kujiajiri wao wenyewe.

(b) Mhe. Naibu Spika, Serikali imeandaa Mipango kadhaa ya kuwasaidia vijana wenye elimu ya sekondari kupata ajira. Miongoni mwa mipango hiyo ni kuwajengea uwezo vijana hao ili waweze kuajiriwa au kujiajiri, ikiwa pamoja na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na mikopo waweze kujiajiri wenyewe. Mpango huu kwa sasa unatekelezwa na Wizara inayoshughulikia masuala ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, fursa hiyo ya mafunzo ya Ujasiriamali na mikopo inategemea utayari wa kijana mwenyewe kuweza kujiunga na mafunzo hayo kwa shughuli anayotaka kuifanya. Vijana wenye elimu ya kidato cha pili, tatu na nne ni miongoni mwa vijana wanaoweza kufaidika watakaofaidika na fursa hiyo. Hivyo napenda kutoa wito kwa vijana kuitumia fursa hii. Aidha nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwahamasisha vijana wetu wajitokeze kutumia fursa zilizopo.

(c) Mhe. Spika, suala la ajira ya mkataba lipo kisheria kwa mujibu wa vifungu Nam. 59(3) na 60(1) vya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011. Hata hivyo, ajira ya mkataba hutolewa kwa wataalamu wenye ujuzi na uzoefu maalum na sio kwa kila mtu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, ninavyofikira vijana wengi wenye elimu ndogo ya *Form II* na *Form III* ndio vijana wengi walio katika matatizo ya ajira zaidi, na kwa kweli serikali yetu kwa mpangilio unaokwenda watu hawa katika elimu katika ajira wanaonekana kama ni watu hawatufai katika ajira.

(a) Je, kama wao wana mpango gani watu hawa wenye elimu ya chini na wale waliokuwa hawakusoma kwa ajili ya kufaidika na maendeleo ya serikali.

(b) Katika kipindi cha nyuma nilizungumza kwamba serikali sasa hivi inaajiri moja kwa moja watu wake inaohitaji inaajiri, nilitoa wazo la kwamba kwa nini hakuna ajira ya muda mfupi ambazo zinaweza zikakusanya makundi ya watu na pale serikali itakapohitaji wakati wanaendelea kujitolea ikawa wanachukua. Mfano nikasema kwamba Hopsitali zetu nyingi ambazo kubwa na nyengine zina ukosefu wa watu ambao wana usafi maeneo mengi ambayo yanahitajika kusaidia. Lakini watu wale unakuta Hospitali bado ajira za watu kama wale zinakuwa chache watu wanapata tabu...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza swali maelezo mengi sana hayo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: (b) Kwa nini serikali haioni mpango wa kuajiri vijana kwa muda mfupi ili kusubiri ajira ambazo zitakuwa za muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

(a) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama serikali imekuwa ikijitahidi kuwashughulikia vijana hawa wenye elimu ndogo kuhakikisha kwamba wanajishughulisha na maswala ya ujasiriamali ili waweze kupata mikopo na serikali imekuwa ikitoa mikopo katika vikundi mbali mbali. Katika vikundi hivi wapo wale ambao wenye elimu na wasiokuwa na elimu. Kwa hivyo, hawa wote wanafaidika na wanapata nafasi ya kujiajiri wao wenyewe.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hivi serikali haijawa na mpango wa kuwa na ajira za muda mfupi lakini itakapoona haja ya kufanya hivyo, serikali itafanya hivyo.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Mhe. Naibu Spika, mbali ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini katika majibu yake amekiri tatizo la ajira kwa vijana ambao wanamaliza masomo yao, na katika majibu yake nakubaliana naye kwamba suala hili liko kisheria katika namba 59 (3) na 60 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma mwaka 2011. Lakini sasa katika majibu yake alisema kwamba hutolewa kwa wale wanaopewa mikataba huwa ni wataalamu au ni wenye ujuzi maalum wa uzoefu.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi ambao wataalamu wamepewa ajira kwa mikataba maalum.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, hapa mbele yangu nina muhtasari wa idadi ya watumishi ambao walioajiriwa serikalini kwa muda mrefu na wale ambao wa mikataba.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa huu muhtasari ni mrefu naomba nikitoka hapa nimkabidhi Mheshimiwa ili aweze kujionea yeye mwenyewe hii orodha ambayo ameitaja. Kwa hivyo, ninayo Mhe. Naibu Spika, hapa mbele yangu.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake ametwambia kwamba vijana wajikusanye na wapate *support* kupitia serikali. Tunakubali na tukizingatia kwamba wizara yako ndio wizara ambayo inategemewa sana na vijana, haijalishi kwamba wametoka skuli au wametoka wapi. Lakini kwenye kesi ya ajira tunakutizameni sana vijana.

(a) Je, kama wizara ambayo imepewa dhamana ya kuajiri vijana hawa mna mpango gani kuwa-*support* vijana wale ambao tayari wameshajikusanya kwenye maeneo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyozungumzia kwamba suala la ajira linahusiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake, Vijana na Watoto. Sasa kwa kushirikiana na kwa kuwa sisi tunashughulika na masuala ya Utumishi ni vyema tukahakikisha kwamba tunashirikiana na hii wizara ili tuweze kuwaajiri hao vijana ambao unaowazungumzia.

Nam. 58

Ukosefu wa Skuli Buyu na Shakani

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Aliuliza**:**
Kwa muda mrefu kumekuwa na usumbufu kwa wanafunzi wa Buyu na Shakani kukosa skuli za karibu na kupata usumbufu wa kufuata elimu masafa ya mbali, zipo taarifa kuwa kiwanja cha ujenzi wa skuli ya Buyu pia kimeuzwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kujenga skuli maeneo ya Buyu na Shakani ili kuwapunguzia shida watoto ambao wanafuata huduma hiyo masafa ya mbali.

(b) Je, kama kiwanja kilichokusudiwa kujengwa skuli Buyu kimeuzwa, Serikali inao mpango wa kukirejesha kiwanja hicho au kutafuta eneo jengine na kujenga.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa katika eneo la Buyu na Shakani hakuna skuli mpaka sasa, watoto kutoka katika maeneo hayo wanasoma katika skuli ya Chukwani, Maungani na Kombeni ambapo inawalazimu watoto hao kutembea masafa ya wastani wa maili moja na nusu.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa skuli unategemea mambo mengi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha na mahitaji husika katika eneo linalohusika. Kwa mustakbali wa eneo hili ni kwamba wizara kwa sasa haina mpango wa kujenga skuli katika eneo hili lenye wastani wa watoto 150 kwa mujibu wa takwimu tulizozipata kwa Afisi za Sheha.

Kwa hivyo, kwa vigezo vya Wizara ya Elimu idadi hii ni ndogo kuweza kujenga skuli. Wizara inaiomba jamii na wananchi kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ili kuanza ujenzi wa skuli na wizara itakamilisha kwa kuezeka, kupiga plasta, rangi na kuweka madawati.

(b) Ni kwamba serikali haina taarifa ya kuwepo kiwanja hicho seuze kuuzwa kwa sababu hiyo ni mchango wa wananchi wenyewe. Kwa hivyo, ni wananchi wenyewe wenyewe na kiwanja hicho hakitokani na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Ahsante.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Naibu Spika, na ahsante Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kwa majibu yako mazuri ambayo yamenipa moyo wa kuweza kufanyakazi karibu na wizara yako.

Lakini swali langu la nyongeza hapa ni kama kuna watoto 150; Je, hatuoni kama watoto hawa ambao wanafuata elimu hiyo masafa ya mbali na tutakuwa hatuwatendei haki. Wizara ina mipango gani kwa vile elimu ya maandalizi ni nguzo ya matokeo mazuri kwa watoto wetu.

Je, wizara yangu ina mpango gani kuhusiana na elimu hii ya maandalizi kwa upande wa walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe.Naibu Spika, napenda nimjibu swali lake la nyongeza.

Kama tulivyosema kwamba wizara inajenga majengo ya skuli kulingana na mahitaji ya pahali, lakini pia kulingana na wingi wa idadi ya wanafunzi. Kwa hivyo kwa sasa tunaendelea kusema kwamba tutajenga skuli maeneo mengine yenye mahitaji na yenye idadi kubwa kabisa skuli. Lakini katika sehemu hii bado wizara inasisitiza kwamba haitojenga, badala yake itawaomba wananchi kuchangia na hatimaye katika sehemu za mwisho mwisho wizara itasaidia kujenga. Iwe skuli ya msingi au ya maandalizi.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze watu wa Buyu kwa kuona kwamba elimu ni jambo la msingi. Lakini kutokana na masharti yaliyoelezwa hapa ninafikiri taratibu nyengine zitafikiwa ili wafanikiwe.

Mimi ninauliza swali hilo kwa upande mwengine. Je, kwa kuwa eneo la Kwarara hivi sasa inajengwa skuli ya sekondari nzuri tu na ninaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuliona hilo. Lakini azma kubwa kwa wananchi wetu ilikuwa ijengwe skuli ya msingi kwa sababu wanafunzi wengi wanatoka kule kwenda Kijitoupele ni masafa makubwa. Kwa kuwa eneo lipo na mimi Mwakilishi, Mbunge pamoja na Madiwani tumesema tupo tayari kujitolea kulinunua kwa njia yoyote yale mazao yao ili tupate eneo lile tujenge.

Je, wizara itatusaidia vipi wakati eneo yaani kulitolea pesa sisi ili tulipate na watoto wetu wapate kupata nafuu ya kutokwenda mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kwamba utaratibu uliopo kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kusaidia katika hatua fulani za ujenzi. Kama tulivyosema kwamba tutasaidia katika kuezeka, kupiga rangi na kutia meza na viti.

Katika hatua za msingi bado tunawaomba wananchi waendelee kujitolea katika kufanikisha masuala ya elimu. (*Makofi*)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi ninapenda nimuulize swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa wamesema kwamba Wizara itasaidia kuezeka na kutia rangi katika majengo yetu ya skuli. Lakini je, kuna majengo mengi ya skuli ambayo yanahitajika kuezekwa na kutiwa rangi na ni majengo mengi kwa Unguja na Pemba, hususan katika Jimbo langu la Kiwengwa kwenye Skuli ya Mgambo na maeneo mengine.

Je, ni lini serikali itamaliza majengo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli tunashukuru kuwa wananchi wamehamasika katika kujenga majengo kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wetu kupata kusoma, na ni kweli majengo haya yapo sehemu mbali mbali Unguja na Pemba.

Lakini sera ya elimu ipo pale pale kusaidia kumalizia ujenzi huo. Na katika mwaka huu wa fedha pia tumetenga fedha nyingi kidogo kukamilisha baadhi ya majengo na baadhi ya pesa zikipatikana kutoka kwa wafadhili.

Kwa hivyo kwa kuwa *kupanga ni kuchagua*, na majengo haya yapo mengi. Tumeomba kuwa labda baadhi ya majengo yatafanyiwa kazi na baadhi ya mengine yatasubiri kadri ya hali ya fedha itakavyopatikana.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Nam. 63

Kuchelewa Kupatikana '*Lease'*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza**:**

Tangu kuundwa kwa Kamisheni ya Ardhi kumekuwa na shida na mateso wanayopata wananchi kwa kufuatilia "*lease*" zao inachukua muda mrefu kuzipata.

Je, ni sababu gani zinazochelewesha kupatikana "*lease*" kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu ya msingi ya kukawia kutayarishwa na kutolewa kwa mikataba ya ukodishwaji ardhi kwa kipindi tokea kuanzishwa kwa Kamisheni ya Ardhi ni kuanza kuupitia upya utaratibu uliopo wa utoaji wa mikataba ya ukodishwaji ardhi.

Mhe. Spika, mapitio hayo yanalenga kuimarisha usalama wa mikataba hiyo, kupunguza migogoro itokanayo na ardhi, kuongeza uwazi juu ya utaratibu mzima wa utayarishaji na utoaji mikataba pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, katika mfumo ambao Kamisheni imeanzisha Mikataba ya Ukodishwaji wa Ardhi huwapatia ushauri wa Kisheria wa Serikali kabla ya kusainiwa na Mhe. Waziri wa Ardhi.

Mhe. Spika, aidha kuchelewa kwa utayarishaji huo kunatoa nafasi ya kupunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi kupitia utaratibu wa kuwapa fursa wananchi kutoa pingamizi juu ya mkataba husika iwapo kutakuwa na matatizo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe.Naibu Spika, ninamini azma yetu nzuri ya serikali kuhakikisha kuondoa migogoro katika ardhi. Lakini tumeshuhudia katika mikataba hiyo ya kutoa *lease* kwenye baadhi ya ardhi zetu inachukua muda mrefu na wananchi wanakata tamaa.

Je, hii ni pamoja na juhudi hizo zilizoelezwa sasa hivi, ni utaratibu gani wa kurahisisha kero hii iondoke.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyokuwa nimejibu kwenye jibu la msingi ni kwamba tunapitia upya kuona utaratibu uliopo tubadili vipi kusaidia jamii. Lengo ni kufika huko ambako tuondoe kabisa lakini pia kusiwe na urasimu usio wa lazima.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa nimuulize Mhe. Naibu Waziri maswali mawili yenye kifungu (a) na (b)

(a) Kwa kuwa Zanzibar tumefungua milango ya kufanya au ku-*promote* biashara za utalii. Ningependa kujua ni kampuni za wawekezaji kutoka nje ya nchi ambazo katika miaka kumi zimekuwa zimeorodheshwa na ambazo zinalipa na *lease*, na kiasi gani cha fedha kimepatikana.

(b) Katika Kisiwa cha *Prisoner Island* ambacho pia kinaitwa Changuu pamoja na Bawe. Visiwa hivi vilikuwa chini ya Mamlaka ya Kamisheni ya Utalii kwenye miaka ya nyuma na vimetolewa kwa kampuni binafsi. Ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kinapatikana baada ya kuvunja mkataba au kuvitoa kutoka Kamisheni ya Utalii na kuanza kulipiwa *lease* ambayo inayo serikali katika miaka tangu ilipoanzishwa visiwa vyote viwili hadi hii leo.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Ni kweli kwamba wawekezaji wageni wapo lakini kwa vile swali lake linataka takwimu, basi ninaomba nije nimjibu kwa maandishi ili upate usahihi zaidi.

Jawabu hili linajumuisha swali lake lote la (a) na (b). Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nina swali langu moja tu ninalomuuliza.

Kwa kuwa Zanzibar ni ndogo sana na ninaona kuna uimarishaji mkubwa wa Mahakama ya Ardhi. Je, inaonekana suala hili litakuwa endelevu kwa muda mrefu wakati Zanzibar ardhi yake ni ndogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, sikumpata vizuri Mhe. Mwakilishi angelirejea swali lake.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninarejea Mhe. Naibu Spika. Ninasemaje bado ninahisi kwamba Zanzibar inapanua Mahakama yake ya Ardhi wakati ninavyohisi mimi Zanzibar ni ndogo na haya matatizo ninayohisi yanaweza yakamalizika au yanaweza yakaja. Sasa katika wizara yako unahisi matatizo haya ya ardhi kwa Zanzibar hayawezi kumalizika na ndiyo ukawa upanuzi zaidi wa Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi la Chake Chake swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza afahamu kwamba sehemu pekee ya utoaji haki ni Mahakama. Iwapo kuna tatizo la kisheria basi anatakiwa akaitafute haki hiyo Mahakamani. Hivyo hatuwezi kuikwepa Mahakama, lakini katika jitihada ya kupunguza mizozo ili isiende mingi Mahakamani ni huu utaratibu mpya ambao tunaoandaa kupitia Kamisheni ya Ardhi itapunguza sana migogoro. (*Makofi*)

Nam. 108
Mpishano wa Mishahara kwa Wahasibu

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza**:**
Kwa kuwa Wahasibu Wakuu wa *VOTE*, Wasaidizi Wahasibu Wakuu wa *VOTE* na Wakaguzi Wakuu wa ndani wa *VOTE*, wanafanya majukumu yao ya kiutendaji sawia katika taasisi moja lakini wanapishana sana kimaslahi.

(a) Je, kwa nini Wahasibu Wakuu wa *VOTE* wanapishana sana kimaslahi (mshahara) na Wasaidizi wao.

(b) Je, kwa nini Wahasibu Wakuu wa *VOTE* wanapishana sana kimaslahi na Wakaguzi Wakuu wa ndani wa *VOTE* hiyo hiyo wakati wapo ngazi moja ya uongozi.

(c) Je, Serikali haioni mpishano huo mkubwa uliopo wa mshahara unavunja moyo na kupunguza ari na ufanisi katika kazi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vipengele (a), (b) na (c), naomba nitoe maelezo ya jumla.

Mhe. Naibu Spika, mishahara ya wafanyakazi wa umma inatolewa kwa kuzingatia mambo mbali mbali yakiwemo daraja la mfanyakazi kutokana na elimu na uzoefu wake kazini. Lakini vile vile inatolewa kwa mujibu wa dhamana aliyonayo mfanyakazi huyo.

Katika wizara aghalabu wakuu wote wa Idara ni wateule wa Mhe. Rais isipokuwa Mhasibu Mkuu. Lakini Mhasibu Mkuu huyu Mhe. Naibu Spika, ndiye mwenye dhamana na kuwajibika kwa masuala yote ya kiuhasibu kwa fungu lake chini ya Afisa Mas-uli. Kwa bahati mbaya kwa muda mrefu Wahasibu Wakuu pamoja na kuongoza Idara hiyo nyeti, hawakuwa wakilipwa maslahi yanayolingana na dhima waliyonayo.

Baada ya kuliona tatizo hilo, serikali iliridhia kurekebisha mishahara ya viongozi hao na kuwa sawa na mishahara ya Wasaidizi Wakurugenzi. Kama ilivyo kwa Idara nyengine zote za serikali Maafisa wote waliokuwa katika ngazi za chini ya zile dhamana hawalipwi kwa kuzingatia maslahi ya wenye dhamana, bali hulipwa kwa kuzingatia daraja la mfanyakazi husika kulingana na Muundo wa Utumishi *(scheme of service).*Utaratibu huu unatumika pia kwa Wasaidizi wa Wahasibu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, naomba sasa kujibu swali la Mhe. Yussuf lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, kupishana kwa maslahi baina ya Mhasibu na Wasaidizi kunatokana na Mhasibu Mkuu kulipwa kwa mujibu wa

dhamana wakati msaidizi analipwa kutokana na Muundo wa Utumishi.

(b) Kama nilivyotangulia kujibu, maslahi ya nafasi za Watumishi wa kada ya Uhasibu na hata kada nyengine zimetafautiana kulingana na jukumu, dhamana na uwajibikaji. Bado dhima na dhamana ya Mhasibu Mkuu ni tofauti sana na ya Mkaguzi Mkuu wa ndani.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, lengo la kulipa maslahi hayo kwa wenye dhamana ni kuongeza uwajibikaji. Mpishano unaotajwa haupaswi kuwavunja moyo watendaji bali unapaswa kuwaongezea ari zaidi ili nao wajitume na kupata fursa hiyo pindi nafasi ikitokea.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe.Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Wasaidizi Wahasibu wa *VOTE* pamoja na Washika Fedha wana majukumu makubwa na nyeti. Je, serikali haioni basi baada ya kukosa huo mshahara, haoni kwamba ipo haja ya kuwapatia posho maalum kama kada nyengine za wanasheria wanaopatiwa maposho.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza pale awali ni kwamba siyo Wasaidizi Wahasibu na Washika Fedha peke yao, lakini ndani ya serikali kuna idara mbali mbali ambazo Wakurugenzi nao pia wana wanasaidizi wao.

Sasa hawa wote wanalipwa kwa mujibu wa *scheme of service.* Wale wateuliwa lakini kwa Mhasibu Mkuu kutokana na dhamana maalum aliyonayo, hawa wanalipwa mshahara maalum kutokana na dhamana hizo. Sasa tutakapozungumzia kundi moja la Wasaidizi Wahasibu na Washika Fedha itabidi hiyo nayo pia tuyazungumze la Wasaidizi Wakurugenzi na wengine wenye dhamana.

Namuomba sana Mhe. Mwakilishi suala hili la mishahara tukubali kwamba linatokana na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi. Tuimarishe uchumi wetu, tuwatake wafanyakazi wajitume ili uchumi ukue, mapato yaongezeke na mishahara ya wafanyakazi nayo ifanyiwe marekebisho kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Waziri kwamba Wahasibu Wakuu wote wana *VOTE* na wana majukumu mazito, lakini Wahasibu Wasaidizi vile vile nao wana majukumu mazito hasa kwa kule Pemba. Ieleweke kwamba wale wa Unguja wana wasaidizi wao wa Pemba, na kule Pemba wapo Wasaidizi Wahasibu wanalipwa malipo ya wasaidizi. Lakini kuna baadhi ya taasisi hawajapata hadi leo kama vile Baraza la Wawakilishi, Mkurugenzi wa Mashitaka na Tume ya Uchaguzi.

Je, ni lini watu hawa nao watapata haki kama wenziwao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa arudie tena swali lake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Shehe Hamad rudia swali.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante. Swali langu ni hili.

Wasaidizi Wahasibu katika Wizara waliopo Pemba wapo ambao tayari mishahara yao wamerekebishiwa, lakini kuna Wasaidizi Wahasibu ambao nao vile vile wanazo *VOTE* hawajarekebishiwa mishahara yao na waliahidiwa kwamba watarekebishiwa. Kama vile Baraza la Wawakilishi, Mkurugenzi wa Mashtaka na Tume ya Uchaguzi hawajarekebishiwa.

Ni lini watu hawa nao watarekebishiwa mishahara yao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema ni kwamba tofauti ya mishahara baina ya Wasaidizi na Wahasibu inatokana kwa sababu Wasaidizi wana *VOTE* (wana fungu), na kwa namna hiyo wana dhima. Dhima ndiyo iliyowafanya mshahara wao uongezeke na uwe tofauti na wasaidizi wao.

Kwa Wahasibu waliopo Pemba sidhani kama wana *VOTE*, hawana *VOTE* (hawana fungu), lakini kama wapo walioongezewa mishahara kwa namna moja au nyengine na wengine kukosa. Naomba Mhe. Naibu Spika, suala hilo nilichukue na nilifuatilie na baadae nitampa maelezo Mhe. Mjumbe.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Japokuwa alikiri katika majibu ya swali la msingi kwamba hawa Wahasibu pamoja na wakaguzi wakuu wa serikali wote ni watu muhimu na wanafanya kazi za msingi sana.

Nilitaka kujua kwa sababu hawa ndio wanaosimamia masuala ya malipo na fedha. Ni utaratibu gani wa kiushauri alioupanga juu ya wizara yake, kwa sababu hawa wanalipa fedha kutoka maeneo tofauti, pale wanapotaka kuhakikisha ushauri wao baina ya wao hadi katika wizara kufika kwako wewe Mhe. Waziri juu, wale wana mawazo husika mbadala, kwa sababu hawa ndio wanasimamia fedha, ndio wanaolipa na ndio wanaoorodhesha.

(b) Pia hawa Wahasibu kuna maeneo huwa wanasimamia katika masuala ya kulipa fedha wakati mwengine kwa *cash* na wakati mwengine wanasimamia kwa kupitia *account* na *cheque*. Lakini bado lipo tatizo tunatumia katika masuala haya katika semina kulipa fedha kwa mkononi.

Je, wizara yako imejipangaje kuwalinda maisha yao hawa watu, pale ambapo unatokezea ujambazi na kuathirika katika maisha yao, juu ya mwenendo wa kazi zao nzima katika kulinda taifa hili na kulisaidia. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba lile swali la (a) alirudie.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai Mohamed rudia swali lako.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika. Namuomba Mhe. Waziri basi aliandike swali ili anifahamu vizuri.

Swali langu ni kwamba, hawa wahasibu wanacheza na mapesa mengi, wanalipa, wanakagua. Kwa mfano, labda Mhe. Waziri atanifahamu. Tunapotaka kununua gari, tunanunua gari kama Prado kama milioni 200 au milioni 150. Kwa mfano, gari hizi zinafanyiwa *service* kwenye gereji za serikali, kwa sababu gereji za serikali zimekufa. Kwa hivyo, haya malipo wanayofanya hawa wakaguzi wanaona siri za nchi jinsi gani malipo yanavyofanywa.

Kwa hivyo, nimemuuliza Mhe. Waziri ni utaratibu gani ameupanga ndani ya wizara yake ambapo hawa watu wanafanya malipo tofauti, yale mawazo yao na fikra zao zinaweza kumfikia yeye kama waziri hapo juu, ili aweze kuyatekeleza katika kazi nzima na maisha yake. Ni ushauri anautumiaje yeye kama waziri, kwa sababu hapa kuna fedha nyingi zinatoka. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika,

(a) Kwanza niseme kwamba ndani ya serikali upo utaratibu wa mawasiliano katika ngazi zote na mawazo ya wafanyakazi ndani ya utaratibu huo wa mawasiliano, basi yanawafikia Waheshimiwa Mawaziri. Vile vile mawazo hayo na fikra hizo kupitia utaratibu huo wa ndani basi yanafika serikalini kwa ajili ya kuzingatiwa. Kwa hivyo, hilo nimtoe wasi wasi, mawazo ya wahasibu na wasaidizi wao yatamfikia Mhe. Waziri pale inapohitajika kufanya hivyo.

(b) Jinsi ya kulindwa. Mhe. Naibu Spika, upo utaratibu wa wazi wa kisheria unaowaongoza katika malipo, iwe malipo ya fedha taslim, lakini iwe malipo kwa kupitia utaratibu wa kibenki. Pale linapotokea tatizo, basi vyombo vinavyohusika vya ulinzi na usalama vinafuatilia matukio hayo. Iwapo mfanyakazi huyo hatokuwa amehusika, basi sheria ipo inamlinda na iko wazi.

Waheshimiwa Wajumbe, tuzingatie sheria katika masuala haya ambayo yako wazi kabisa, na wafanyakazi hawa wanalindwa kupitia utekelezaji wa sheria hizi.

Nam. 24

Tatizo la Upatikanaji wa Kipimo Cha *CT Scan*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Wananchi walipata faraja sana baada ya Serikali ya Awamu wa Saba kuleta vipimo vya kisasa, lakini upatikanaji wa kipimo cha *CT Scan* imekuwa haupo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa muda mrefu na kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi masikini wanaoshindwa kupata huduma katika hospitali binafsi. Kwa kuwa kipimo hichi ni muhimu sana kwa watu wanaopata ajali barabarani, watu wenye magonjwa makubwa yanayohitaji uchunguzi wa kina na kutopatikana kwa uhakika kwa huduma hizi.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kukosekana kwa kipimo hicho inachangia vifo kwa watu wanaohitaji huduma za uchunguzi wa kipimo hicho kwa kuzikosa

(b) Iko wapi faida baada ya Serikali kutangaza huduma hiyo ipatikane bure kwa wananchi wakati huduma hiyo haipatikani.

(c) Kwa nini katika hospitali binafsi vipimo hivi vinasimamiwa vizuri mashine zake, na zinapoharibika kutengenezwa kwa wakati, wao wanaweza vipi huku Serikali inashindwa, na hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji dhamana

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma za afya ipasavyo, ikiwemo huduma za uchunguzi. Kukosekana kwa kipimo cha *CT Scan* hakupelekei moja kwa moja vifo kwa watu wanaohitaji, kwani idadi kubwa ya magonjwa yanayoweza kugunduliwa kupitia kipimo cha *CT Scan* pia yanaweza kutambuliwa kwa kutumia kipimo cha *X ray*, ambacho kilikuwa kikitumika pekee kabla ya kupatikana kwa kifaa cha *CT Scan* zaidi ya miaka 50. Hata hivyo, tunakiri kwamba kifaa hichi ni cha hali ya juu na matokeo yake ni ya kuaminika zaidi na yanayoonesha undani wa baadhi ya mishipa ya binadamu.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuharibika kwa kifaa hicho haina maana kwamba hakuna faida ya tangazo lililotolewa na serikali ya kutoa huduma hizo bure. Naomba kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba hospitali imeshuhudia ongezeko la wagonjwa wengi sana wanaohitaji huduma hii mara baada ya tangazo hilo za serikali ambapo wastani wa wagonjwa 371 hufika hospitali kwa mwezi kupatiwa huduma hiyo, ukilinganisha na wastani wa wagonjwa 120 kwa mwezi kabla ya tangazo hilo.

Huduma hii ya bure imeleta mfumko wa idadi kubwa ya watu. Serikali itahakikisha kwamba kifaa hicho kinafanyiwa matengenezo haraka iwezekanavyo, mara tu fedha zitakapopatikana na kuendelea kutoa huduma hiyo bure kwa wananchi.

(c) Mhe. Naibu Spika, kikawaida mashine hizi za *CT Scan* huwa zinasimamiwa katika utaratibu ila hitilafu za umeme yaani *low voltage*, pamoja na kuhudumia watu wengi sana, ndizo zilizopelekea kuharibika kwa kifaa cha *IRS*. Hata hivyo, wizara imeona umuhimu wa kufanya kazi kwa kifaa hicho, Wizara imeshatenga jumla Tsh milioni 32.7 za matengenezo ambapo nusu ya fedha hizo tayari zimelipwa kwa kampuni ya *Pacific* ya Afrika Kusini. Ni matarajio yetu kwamba bajeti ya mwaka 2016/2017 ya Wizara ya Afya baada ya kupitishwa tu, itaweza kukidhi matengenezo ya kinga, *preventive maintenance*, kila baada ya mzunguko wa wagonjwa 2,000. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kuwaonea huruma wananchi wake wa nchi hii na kutoa huduma za afya muhimu bure kwa wananchi wake au wananchi wetu. *(Makofi)*

Pili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, mara nyingi panapotokea haja maalum ukiwatafuta kwa njia yoyote ukiwapata watakueleza wapi uende ili ufanikiwe tatizo lako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tuliokuwemo humu sote ni waheshimiwa tunawaongoza wananchi wetu wa Zanzibar, na kila mwenye matatizo yake pa kukimbilia atapajua na anapotanzwa mwananchi wetu utajua nani wa kumtafuta, hasa waziri ama naibu waziri kwa sababu ndio wasemaji wetu wa mwanzo.

Mimi kwa kuzingatia hayo, je, hawa wasimamizi wa *CT Scan* kweli ni waaminifu baadhi yao. Kwa sababu kubwa linalotokea hapa, kama limetokea tatizo kwa mwananchi wangu, nikimpigia simu Mhe. Waziri akinielekeza nenda kwa mtu fulani, anafanyiwa matibabu mtu yule bila ya matatizo. Mimi nataka kuuliza tu, hawa wafanyaji kazi wetu katika taasisi hizi kweli waaminifu. Mhe. Naibu Waziri atoe kauli hapa na wananchi wasikie?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, tunakiri na tunawathibitishia kwamba wafanyakazi wetu wa Wizara ya Afya ni waaminifu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuajiriwa mfanyakazi anahakikiwa sio afya tu, lakini pia anahakikiwa kwenye vyeti alivyosoma pamoja na baadhi ya tabia

zake. Tukiwaangalia wafanyakazi wa Wizara ya Afya ni wafanyakazi wa muda mrefu, hasa katika kitengo hiki cha *CT Scan/X-Ray* na pamoja na vitengo vyengine. *(Makofi)*

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kama jibu alivyolijibu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa kipimo cha *CT Scan* kwamba ni kipimo muhimu sana kwa Pemba. Je, serikali haioni haja ya kupatiwa kipimo hiki kwa Pemba, ikiwa wananchi…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, endelea, lakini kiutaratibu hatutakiwi kusoma. Kwa hivyo, ukiuliza swali la nyongeza, unauliza bila ya kusoma.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Haya. Nauliza je, serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa wananchi wa Pemba kupatiwa kipimo hiki kama Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, serikali inawajali sana wananchi wake, na serikali maana yake inawaongoza wananchi wa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, inaona haja kubwa ya kuweka kipimo hicho katika Kisiwa cha Pemba, na *In sha Allah* Mwenyezi Mungu akipenda tunatarajia ifikapo mwezi wa Septemba tutafunga kipimo hicho katika Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani. *(Makofi)*

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniona kutaka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali ambayo tumekuwa tukishuhudia sasa hivi, ni kwamba wananchi wetu wameshajihika sana katika kujitokeza kutumia vipimo hivi ambavyo Mhe. Naibu Waziri ameweza kujibu, kwamba mashine hizi ni kuwa watu wameona kuna umuhimu mkubwa na wamekuwa wanajitokeza sana.

(a) Je, serikali imezingatia kwamba vipimo kwa baadhi ya wataalamu wanasema kwamba kuna athari. Je, serikali ina mpango gani katika suala zima la kutoa taaluma juu ya matumizi ya vipimo hivi.

(b) Mhe. Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba sasa hivi Baraza na wananchi pia wanapiga kelele kuhusu suala zima la vipimo hivi au mashine hizi ambazo zinaonekana ni ghali sana. Lakini kwa sasa Hospitali ya Micheweni kuna mashine ya *X-Ray* ambayo imefungwa takriban miaka

mitatu sasa na haijawahi kutumika hata siku moja, na inasemekana kwamba haina mtaalamu, naiuliza serikali kwa kupitia wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliza swali. Enhe. Uliza swali maelezo yametosha.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba wizara ina kauli gani ya kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuwa inatoa ahadi gani au inatoa kauli gani juu ya kuwepo kwa kadhia hii ambayo imewakumba wananchi wa Wilaya ya Micheweni. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika,

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kutokana na huduma hii kutangazwa na serikali kuwa ni bure, kuna mfumko mkubwa wa wananchi ambao wanaitumia nafasi kwa kupata huduma hii. Wizara imejipanga kutoa elimu ya kutosha kwa kupitia nyinyi Wawakilishi wenzetu ambao mna majimbo. Pia kwa kupitia kwa masheha na kupitia vituo vya afya ambavyo vimo katika sehemu zao.

Hata hivyo, napenda nichukue nafasi hii kuwatahadharisha wananchi kutoendelea kukitumia kipimo hiki bila ya sababu maalum na maelekezo thabiti ya madaktari. Utafiti tulioufanya umeonesha kwamba wengi wanaokuja katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kupata kipimo hiki wanatoka katika hospitali za *private*. Tukumbuke kwamba hospitali za *private* wanachokijali ni pesa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mgonjwa anapokweda pale ukimpa tu ushauri daktari kwamba nataka nifanyiwe hivi na hivi au nipimwe hivi na hivi, yeye kwa sababu anaitaka pesa na anaiona hali yako umemuinamishia shingo kwamba ni mgonjwa sana, basi atakuandikia kipimo. Wasipoangalia wanaweza wananchi wetu wakapima vipimo hivi mara tatu au mara nne kwa mwaka, kitu ambacho kina athari na kitawaletea usumbufu mwingi baadae, kwa sababu ile ni mionzi ambayo inapita ndani ya miili yetu. Kwa hivyo, Wizara ya Afya inatoa tahadhari kwa wananchi kwa kipimo hicho.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwamba Micheweni kipo kipimo cha *X-Ray* na kimekaa muda wa miaka mitatu hakifanyiwi kazi. Mimi napenda nikuombe Mhe. Mjumbe ukirudi upite katika Hospitali ya Micheweni ili uulizie zaidi. Kipimo hiki hivi karibuni kimeshaanza kazi na wataalamu wanaotumika ni wataalamu kutoka katika Hospitali ya Wete, na kwa baadhi ya siku ambazo zimepangwa maalum. Wanakwenda siku ya *clinic* wanawahudumia wagonjwa baadae wanarudi.

Kweli Hospitali ya Micheweni hakuna wataalamu ambao wameajiriwa pale kwa kufanya kazi hii, lakini wanatoka Hospitali ya Wete kwa siku ambazo zimepangwa wanatoa huduma na kurudi. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nauliza swali hili ni kwamba nilishafanya uchunguzi, kwa sababu ni juzi tu katika ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwepo jimboni kwangu, niliweza kufika na nilimchukua mtaalamu ambaye ni Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi tulikuwa katika ziara hiyo pamoja na tulifika tukawahoji wafanyakazi walioko pale na walitupa majibu ambayo yalikuwa ni sahihi.

Kwa hivyo, naomba nimueleze Mhe. Naibu Waziri kwamba sijaletewa *message*, nilifika mwenyewe nikazungumza na wafanyakazi na wakanipa uthibitisho huo. Ahsante Mhe. Naibu Spika, *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, hatuna haja ya kuvutana, naomba nilichukue hili nilifuatilie. Lakini utaratibu uliopo, wakati nilipotembea ziara ya mwezi uliopita nilikuta hakuna na nikatoa ushauri, na juzi Afisa Mdhamini kanijulisha kwamba kuna wataalamu ambao wanakwenda kwa siku ambazo ni *clinic* ya kufanya *x-ray*.

Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kumwambia Mhe. Mjumbe kwamba nitalifuatilia na kama halijafanyiwa kazi, basi tutalipatia ufumbuzi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana mahiri ya Mhe. Naibu Waziri, ambaye anafanya jitihada kubwa ya kufika sehemu zote zinazouliziwa maswali, naomba sana kuendelea kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi, kwa maswali yao mahiri ambayo yanatufanya sisi serikali tuweze kusimamia kazi zetu vizuri zaidi, nawapongeza sana kwa hili.

Pili Mhe. Naibu Spika, nimefurahi sana na nimefarijika sana kwa kauli ya Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa kutoa kauli na kufanya uamuzi kwamba huduma hizi za *CT Scan* pamoja na huduma nyenginezo za vipimo zitakuwa zinatolewa bila malipo Zanzibar.
Zanzibar ni miongoni mwa nchi tano tu duniani ambazo zinatoa huduma hizi bure bila ya malipo. Nchi nyengine ni Norway, Denmark, Cuba na *United Arab Emirates*, baada ya hapo Zanzibar nayo inaingia, kwa hivyo naomba nipongeze

sana na nilikuwa natarajia Waheshimiwa Wawakilishi wangelipongeza sana hili jambo hususan kwa kuzingatia kauli ya Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, katika swali alilouliza Mhe. Shamata alizungumzia pia kuhusiana na athari ni vyema kutoa kauli ambayo itakuwa haileti utatanishi wowote, athari ya mionzi huwa inampata zaidi pale mama mjamzito anapokuwa keshatunga ile mimba ama ule ujauzito, pale ndipo athari za mionzi zinatokezea, na ndio maana kabla ya mwanamke kufanyiwa vipimo hivi huwa anaulizwa mara kadhaa na wakati mwengine hubidi afanyiwe *test* ya mkojo kujulikana kama ana ujauzito au hana ndipo aweze kufanyiwa vipimo hivyo. Kwa hivyo hiyo Mhe. Shamata kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ndio athari mojawapo ambayo huwa tunachunguza.

La pili Mhe. Naibu Spika, *field* hii ya *radiology* ni *emerging services* ni taaluma ambayo ina *demand* kubwa duniani sasa hivi, mpaka sasa hivi hapa Unguja sisi tuna *radiology* mmoja Dkt. Salum ambaye anapatikana pale ghorofa ya kwanza ambaye anafanya mambo ya *CT Scan* na *Scan* zile nyengine pamoja na kushughulikia *x-ray* pamoja na wasaidizi wawili Ndugu Ali Khamis na yule Shehe Mohammed.

Sasa tunaendelea kuwa-*train* vijana wetu; wako vijana watatu sasa hivi wako masomoni, lakini tatizo kubwa tunalolipata sisi kama Wizara ya Afya wakirudi tu wale vijana huwa wakitua tu hapa huwa wanapewa ofa kutoka Tanzania Bara ambazo ofa nyengine kubwa sana ambazo kama Mhe. Waziri alivyoulizwa leo asubuhi ni nje hata ya *Scheme of Service* ya Serikali.Kwa hivyo tuna changamoto ya kuwa-*maintain* vijana wetu na uzalendo ni suala muhimu sana, ambalo litaweza kutusaidia kuwa- *maintain* vijana wetu wabakie.

Kwa upande wa Pemba tuna changamoto hiyo Abdalla Mzee keshamalizika tunatakiwa tutafute wataalamu kama 100, maana Hospitali itakuwa kubwa na ya kisasa, nafikiri wale Wawakilishi walioko Pemba wanatembelea ule ujenzi unaoendelea na nilitembelea wiki iliyopita na Mhe. Naibu Waziri nashukuru ameshafika zaidi ya mara mbili pale, pale patahitajika wataalamu wengi, na hiyo ni changamoto ambayo tunaendelea kuifanyia kazi, lakini wakati huo huo. Pia tumezungumza na Serikali ya China juzi wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein akizungumza na Gavana wa kutoka Jimbo la *Jiangsu Province* kule China, suala hili liligusiwa, na Wachina wamekubali kuwa-*train* vijana wetu. Kwa hivyo tunatarajia eneo hili litakaa sawa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Nam. 74

Matengenezo ya Daraja la Tinga Tinga

Mhe. Suleiman Sarahan Said: – Aliuliza:
Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutengeneza barabara nyengine inayoelekea Wesha kutokea Tibirinzi ambayo pia ina daraja la enzi pale Pondeani, badala ya ile ya kupitia katika daraja la Tingatinga ambalo limekatika kwa maji kwa muda mrefu sasa.

(a) Kwa kuwa tunafahamu umuhimu wa eneo la Wesha ukizingatia kwamba ni sehemu muhimu yenye Mitambo ya umeme na vituo vya mafuta, Je, Serikali haioni umuhimu wa kulifanyia matengenezo daraja la Tinga Tinga kabla ya lile la Pondeani halijaanza kuleta madhara.

(b) Kama Serikali haijawa na nafasi ya kulitengeneza daraja hili la Tinga Tinga, kwa nini isifikirie kujenga angalau Daraja la vyuma ili kunusuru maisha ya watumiaji wa daraja hilo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Wizara imeona daraja la Tinga Tinga ni bovu na haliwezi kutengenezeka kwa muda mfupi na linahitaji matayarisho ya muda mrefu, hivyo basi Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliamua kuweka mbadala kwa kujenga barabara ya Chake – Wesha.

Mhe. Spika, katika barabara hiyo ya Chake hadi Wesha, Wizara ilijenga daraja maeneo ya Pondeani. Ili kulienzi daraja hilo Wizara ya Ujenzi imeanzisha vikundi vya usafi na kuhakikisha kwamba daraja hilo linatoa huduma wakati wote. Na napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kuwa vikundi hivyo vya mazingira viko katika maeneo hayo hayo ya Pondeani.

b) Kujenga daraja la vyuma pia linahitaji matayarisho ya muda mrefu na gharama zake ni kubwa zaidi, hivyo tunaomba wananchi waendelee kuitumia barabara ya Chake hadi Wesha ili kunusuru maisha yao.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, na pia kwa idhini yako nimpongeze nilipata salam jana alikwenda Jimboni kwangu alifanya mambo mazuri sana, kwa hivyo nilikuwa nampa pongezi.

Na mimi naomba kuuliza swali moja lenye (a) na (b).

a) Nilikuwa nazungumzia suala la barabara ya Tinga Tinga, je, bado ana mpango nayo kwamba barabara ile imo katika orodha ya barabara za Serikali, kwa sababu sasa hivi naona watu maeneo yale wamevamia kujenga, sasa sijui kama bado barabara imo kwenye mpango wa Serikali.

b) Katika daraja la Tibirinzi niko hapo hapo maeneo ya Pondeani ni kwamba lilikuwa daraja lake linafunga maji na kufungua maji ya bahari ambayo yanaingia kwenye mashamba, na kwa bahati mbaya mashamba yale yamepata athari kwa muda mrefu kidogo wananchi wale hawatopata mpunga au mchele. Je, Mheshimiwa anaweza akaungana na Wizara ya Kilimo na wengine tukaweza kuwasaidia wakulima wale fidia ya mchele kwa kipindi mpaka mashamba yao yatakapokuwa yanajikidhi haja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kwanza nachukua pongezi alizonipa na hizi ni pongezi kwa Serikali yote. Hivi sasa tumeamua kwamba tuwe karibu na wananchi zaidi ili kuhakikisha kwamba kero na matatizo yao tunayatatua kwa mujibu wa Ilani yetu ya uchaguzi ya 2015/2020. Kuhusu kuijenga hiyo barabara ya Tibirinzi kama nilivyomwambia kwamba kipaumbele kwa hivi sasa tumetoa kwa barabara yake inayotoka Hospitali ya Chake Chake hadi tunakokwenda Tibirinzi, ambayo tunaita Barabara ya Kata, kwa hivyo hii ndio barabara iliyopewa kipaumbele kwa hivi sasa, lakini kuhusu wananchi kujenga, hiyo ni kazi au hatua nyengine, kama wataonekana wamejenga katika hifadhi za barabara basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kuhusu huu mlango ambao anauzungumzia ambao zamani ulikuwa unafunguliwa na kufungwa kwa mujibu wa maji kujaa na kupwa, napenda kumpa taarifa rasmi kwamba ule mlango tayari tumeshautengeneza wiki iliyopita, na juzi nilikuwa Pemba nimehakikisha uko tayari na wakati wowote utafunguka ule mlango kwa ajili ya kuondosha zile athari za wale wanaolima mpunga katika zile sehemu zinazohusika. Na umetugharimu kama Shs. 800,000/= katika kuutengeneza ule mlango pale.

Na hili suala lake la kuhusu kuathirika kwa wale wakulima wa mpunga tutakaa na watu wa Mazingira ambayo iki chini ya Wizara ya Ardhi na Kilimo tuangalie namna gani ya kulitatua tatizo hili kwa ajili ya wananchi wetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).
Mhe. Naibu Waziri mbali na majibu yake mazuri, katika majibu yake aliyosema kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliamua kuweka mbadala wa kujenga barabara ya Chake/Wesha na niipongeze Serikali kwa kufanya kazi hiyo nzuri, lakini barabara hii tayari imeshaanza kuharibika kwa kupasuka kwa athari ya maji ya bahari.
a) Je, Wizara ina mpango gani kuifanyia ukarabati barabara hiyo.

b) Kutokana na athari hizo za maji ya bahari pamoja na maji ya mvua barabara nyingi pia za Unguja zikiwemo kama Biziredi pale, Malindi *round about*, *round about* ya Kisauni, barabara hizi zimechimbuka kwa athari za mvua ambazo zilitokea hivi punde katika miezi miwili nyuma iliyopita. Je, Wizara ina mpango gani kuzifanyia ukarabati barabara hizo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Tunajua kwamba maji ni sumu kwa barabara yoyote ile hasa ikiwa maji ya chumvi, sisi tunavyofanya utaratibu wetu ni kuhakikisha kwamba zile sehemu ambazo zinaathirika na maji au tatizo lolote lile tunazifanyia matengenezo, haraka tunaita wenyewe *rotten*, kwa hivyo barabara hizo tumepita na tumeona athari zake, na hizo nyengine alizosema za Biziredi lakini nataka kumwambia kwamba safari hii mfuko wa barabara umetengewa pesa asilimia 85 Wizara yetu katika kutengeneza hizo barabara, tutajitahidi tuhakikishe kwamba hizo sehemu zote tunazifanyia kazi kupitia kitengo chetu cha utengenezaji na utunzaji wa barabara cha *UUB*.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tuna barabara kuu nyingi Zanzibar za kwenda Kaskazini, Kusini, Kutoka Bububu unaelekea zako Kinyasini, Mahonda mpaka Nungwi, pamoja na barabara ya Kama unapita zako mpaka Bubwini kupitia Kiombamvua na Michungwa miwili pamoja na barabara ya Kusini ambayo sasa hivi inatengenezwa kutoka Fuoni kupitia Tunguu mpaka Kusini.Lakini tumekuta kwamba Serikali ikiwa wakala wa wananchi katika kutumia fedha zao na kujenga haya maeneo tofauti imekuwa magari yanayopakiwa mawe na mchanga hasa katika maeneo ambapo kumejazwa matuta, yamekuwa yanamwaga michanga, wakati mwengine uchafu, lakini pia huathiri hizi barabara pamoja na kokoto wanazozibeba kwa muda mrefu.

Ni utaratibu gani wa Wizara hii ya Usafirishaji pamoja na kusimamia kwa ujumla katika hatua za kushughulikia haya magari ambayo yanaathiri hii miundombinu muhimu ambayo imejengwa kwa pesa nyingi kabisa.

Kwa kuwa Mhe. Rais alipokuja kuhutubia Baraza alizungumza katika suala la miji mipya inayojengwa na mmoja wao ni katika Jimbo langu la Tunguu, na tayari wananchi wengi na wananchi wangu hasa wameitikia wito Wazanzibari wenye nia njema kuanza kuimarisha katika mji wa Tunguu kujenga barabara tofauti, nyuma na makazi yao…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Uliza swali.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) Ni utaratibu gani Mhe. Naibu Spika, Wizara husika inajipanga katika kusaidia kuendeleza hizi barabara za ndani katika Jimbo la Tunguu hasa eneo ambalo limetajwa baina ya Jumbi na Tunguu kwa ujumla. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyojibu katika Swali mama la Mhe. Sarahani kwamba hivi sasa kunakuwa na vikundi vya usafi. Vikundi vya usafi hivi wanakuwa wanachukua tenda kwa Halmashauri za wilaya husika au katika barabara zetu wakati wa kufanya usafi wa kuondosha/kukata majani na mchanga, kwa hivyo vikundi hivi pale ambapo vinawezeshwa na wenye tenda wanazozichukua basi wanafanya kazi zao kwa ukamilifu na kwa uzuri zaidi.

Kama nilivyosema juzi tumeenda Pondeani kule tumeona kwamba wanafanya kazi nzuri sana, na kuna vikundi vingi ukipita asubuhi utakuta wanasafisha barabara, vikundi vile ni vya kujitolea haviko chini ya Wizara yetu, lakini sisi tunawapa tenda Halmashauri na Halmashauri wanategemea vikundi hivyo wanawapa tenda ya kusafisha na kuweka barabara ziwe safi.

(b) Barabara zote sasa hivi ukiondoa hizi *Town Roads* ambazo ni barabara kuu zinazopita mfano kwako kule, sisi zile ndio tunakuwa tunaweka alama za kuonesha kwamba gari ya uzito fulani ipite na inayozidi uzito fulani isipite, sasa kama gari hizo zimezidi uzito kuna sheria ambazo tunazichukulia hatua. Lakini magari mengi ya Zanzibar ukiondoa haya magari yanayotengeneza barabara tani zake hazizidi tani 20.

Kuhusu barabara za ndani zote ziko chini ya Halmashauri, kwa hivyo nakuomba upeleke maoni yako Halmashauri ili Halmashauri nao waziweke katika bajeti zao waangalie kama uwezo wanao, basi nina imani kwamba kwa

kushirikiana na nyinyi Wawakilishi wetu zitatengenezwa hizo barabara ili zipitike wakati wote.

Nia yetu ni kwamba wananchi tunawapelekea huduma muhimu za miundombinu ili kurahisisha maisha yao na kipato chao ziweze kukua na kukuza pato la nchi.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Kwa mujibu wa Kanuni ya 37(1) Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa ajibu kwa ukamilifu, usahihi na kwa ufupi.

Swali langu lilikuwa ni kwamba ni utaratibu gani Wizara yake imejipanga katika kuchukua hatua za kisheria katika magari ambayo yanabeba mawe na mchanga yanayoharibu miundombinu ya barabara ambayo Serikali ikiwa wakala, kama wananchi wanatumia fedha nyingi hata kuweza kuzilinda, ni utaratibu nilioulizia, ni swali hilo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Nimemjibu mwanzo hakunifahamu vizuri kwamba magari mengi ukiondoa magari yanayotengeneza barabara uzito wake hauzidi tani 20, magari makubwa ambayo yanatengeneza barabara sisi huwa tunawapa maelekezo kwamba iwapo sehemu waliyofanya ujenzi wa barabara kukaharibika miundombinu ni wajibu wao kutengeneza na sisi tunahakikisha kwamba wanazifanyia ukarabati hizo sehemu. Kwa hivyo kama kuna barabara yoyote ambayo imeathirika kwa wale watengenezaji wa barabara ni jukumu lao kutengeneza.

Lakini kama nilivyosema mwanzo magari mengi yanayopita hapa Zanzibar uzito wake hauzidi tani 20, ukiondoa yale makontena kama nilivyomjibu Mhe. Jazira, yanaathiri mpaka barabara ya Biziredi, tutaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba yale makontena yanayopita njia zile ambayo ni kwa zaidi ya tani zake kuna makontena mengine mpaka 45 uzito wake unakuwa, sasa yale tutaangalia utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba hayaathiri barabara zetu. Na namhakikishia kwamba sheria zipo na kwa mujibu wa sheria kwamba kila mtu anatakiwa azifuate sheria zile kikamilifu, na kama kuna mtu umehisi kafanya jambo ambalo ni kinyume na sheria zetu basi mimi nakuomba uniarifu hayo magari na tutayachukulia hatua. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, naunga mkono vizuri kabisa maelezo na majibu ya Mhe. Naibu

Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na naomba niengozee tu majibu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kikawaida kwa mujibu wa sheria yetu ya usafiri na usalama barabarani, Sheria namba 7 ya mwaka 2003 inaeleza wazi juu ya utaratibu mzima wa usafiri na mwenendo mzima wa huduma za barabara.

Swali la Mhe. Mjumbe alikuwa anaulizia juu ya taratibu na majukumu ya Serikali katika kutoa adhabu kuhusiana na masuala haya. Ni kweli kumejitokeza tatizo kubwa na la msingi na madereva wetu kutosimamia sheria, kanuni na taratibu husika.

Kwa mfano Madereva wamekuwa hawazingatii kabisa sheria za nchi, barabara zetu zipo zenye kuruhusu uzito wa tani tano yanapita magari zaidi ya tani tano, barabara za tani saba yanapita magari ya zaidi ya tani saba, barabara ya tani kumi yanapita magari zaidi ya tani kumi.

Hivyo naomba tu kumjulisha Mjumbe kwamba utaratibu huu ni jukumu la Jeshi la Polisi kuchukua hatua na kuwashtaki katika vyombo vya dola pamoja na kuwafikisha Mahakamani kwani watu hao wamevunja sheria husika sheria namba 7 ya mwaka 2003 inayosimamia suala zima la usafiri na usafirishaji hapa Zanzibar. Kwa hivyo jukumu letu la msingi la Serikali ni kuvitaka vyombo vya dola visimamie sheria husika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa tumemaliza kipindi cha maswali na majibu nataka niwatambue wageni wetu ambao wamefika hapa leo, na wageni hawa ni wa Mheshimiwa Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Konde yeye ametembelewa na bibi Fatma Omar Kombo ambaye ni mama watoto wake. Ningemuomba kama yupo asimame Bi. Fatma karibu sana Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Mhe. Rashid Ali Juma Mwakilishi wa Amani ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Hawa ni Kamati ya Siasa ya Jimbo la Amani, jumla yao ni 9 na wanaongozwa na Katibu wao ambaye anaitwa Bi. Tuwaika Hamad. Wageni wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii naomba wasimame. Ahsanteni sana, karibuni.

Wageni wetu wa mwisho ni wageni wa Mhe. Ussi Yahya Haji, Mwakilishi wa Mkwajuni. Wageni hawa wamekuja ni Kamati ya Siasa ya Jimbo la Mkwajuni, jumla yao ni wanne na wanaongozwa na Mhe. Machano Fadhil Babla.

Waheshimiwa naomba msimame, karibuni msimame wakuoneni. Ahsanteni, karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe pamoja na hayo ninafikiri sote tunafahamu kama kesho tukijaaliwa tunauanza mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na kwa utaratibu tulionao kwamba Ramadhani tunaanza saa 3.00 na tunamaliza saa 8.00 ambayo ni Kanuni ya 23(4) inayozungumzia suala zima la kuanza kwa kazi zetu lakini na muda wa kumaliza. Kwa hivyo kutokana na ratiba yetu Mhe. Spika, kwa busara zake amewaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wakubali kutengua Kanuni kifungu cha 23(4) ili badala yake tumalize saa 9.00.

Sasa nitamuomba Mwanasheria Mkuu atutengulie hiyo Kanuni ili tukijaaliwa kesho tuweze kumaliza saa 9.00 na kumaliza shughuli zetu za Baraza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo umeeleza kesho tunatarajia kuanza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na kwa mujibu wa Kanuni ambazo zinaongoza vikao, Kanuni ya 27(4) kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunaanza saa 3.00 na kumaliza saa 8.00.

Sasa naomba kwa sababu na bajeti hii inaendelea na kuna Wizara nyingi ambazo bado hazijawasilisha hotuba zao za Makadirio, hivyo naomba nitoe hoja ya kutenga kando Kanuni hii ya muda tuanze saa 3.00 lakini tumalize saa 9.00 badala ya kumaliza saa 8.00 kama ambavyo Kanuni inaongoza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshatoa hoja. Sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshida.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa Fedha 2016/2027

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Sasa tutaanza kuendelea na majadiliano lakini Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana wachangiaji ni wengi, wachangiaji mpaka sasa hivi ni 24, lakini leo kwa mujibu wa ratiba tunatakiwa mchana huu tuwe tumeshamaliza Wizara hii, ili jioni Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Michezo na Utamaduni aanze kusoma hotuba yake. Kwa maana hiyo sitokuwa na uwezo wa kuwaita Wajumbe wote ambao wameleta maombi yao hapa mbele.

Naomba sana, si kwa sababu nyengine yoyote isipokuwa kwa sababu muda wetu hautoshi. Kwa hivyo nakuombeni sana wale ambao sitowataja wapeleke maoni yao au wapeleke michango yao kwa Waziri ili na wao waweze kama tunavyosema waweze kupiga buti, au vyovyote au maoni yao yachukuliwe na Mhe. Waziri.

Nafikiri Wajumbe mumenielewa vizuri, si kwa sababu nyengine yoyote nasema tena isipokuwa kutokana na muda tulionao, naomba sana munielewe hivyo. Kwa hivyo nimepata shida sana kutafuta nani nimpe nani nisimpe, kwa hivyo atakayekuwa nimempa ajue ni bahati yake tu kwamba nimemchagua yeye, ninafikiri tumeelewana Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, tunakushukuru sana kwa ushauri wako huo lakini kama unavyofahamu kwamba Baraza letu hili ni jipya na Waheshimiwa wengi ni wapya, na kuna mambo mengi ambayo wanataka kuiambia serikali, na kwa kuwa hii bajeti ni ya Tawala za Mikoa, Tawala za Mikoa mpaka masheha wetu wamo. Kwa hivyo kila mtu anataka kuiambia serikali, nini serikali yetu ije ifanye.

Vile vile ukizingatia Mhe. Naibu Spika, madiwani wetu mpaka leo bado hawajapewa nafasi zao hata ya kuweza kutoa mchango wao wa mawazo. Kwa hivyo tunazungumza yetu na tunazungumza ya madiwani wetu, sasa mimi nilikuwa nina ushauri.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja humu nyingi zinataka maelezo ya kina, kuna *data* kwa sasa hivi Mhe. Waziri tukimwambia hawezi kutujibu sasa hivi tutakuwa tunamuonea, tunahisi sisi sasa hivi tuchangie halafu tumpe nafasi Waziri akakae na watendaji wake aje atuletee maelezo ya kina jioni. Mimi ninaamini Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mimi hoja zangu kama utanipa nafasi nina hoja *specific* nataka Waziri akazifanyie uhakiki wa kutosha, ili nisije nikampa tabu katika kupitisha vifungu.

Sasa mimi ninaomba Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tuache tuchangie, ili tumpe nafasi Mhe. Waziri akakae na watu wake ili wampe jawabu za kutosha, ili anapokuja kutujibu baadae iwe masuala mengi yamepata ufafanuzi na hata hizo buti zipungue tupate tupitishe bajeti yake vizuri.

Kwa ridhaa yako, kwa upendo wetu sisi na wewe Mhe. Naibu Spika, angalia macho ya Waheshimiwa Wajumbe jinsi wanavyotaka kuichangia Wizara hii, uturuhusu hii bajeti tuje tuipitishe jioni.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza inaonekana kama unamsemea Mhe. Waziri, maana Mhe. Waziri yeye hajaomba mwenyewe kwamba anataka apewe muda wa kwenda kujibu hayo maswali. Labda angesema kwamba muda huu wachangiaji baada ya kuchangia apewe muda wa kwenda kujibu maswali, pale ningeona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Lakini niseme hivi kwamba tuna nafasi ya wachangiaji kwa muda ambao nimepanga angalau wapate wachangiaji 10, na ninafikiri itakuwa imetosha kwa wachangiaji 10 kuweza kuchangia na wengine kupeleka michango yao kwa njia ya maandishi.

Nafasi ya wachangiaji 10, Mheshimiwa naomba unikubalie hilo tuendelee ili muda ututoshe kuweza kumaliza siku zetu za bajeti. Hali unaifahamu ilivyo, kwa hivyo nafasi 10 sio kidogo, na ikiwa kwamba muda hautotosha basi tutaongeza muda mchana huu ilimradi tu tumalize, tusije tukafikia mpaka saa kumi na moja lakini nimekusudia tumalize Wizara hii leo hivi mchana.

Kwa maana hiyo tunaweza tukaja tukapindukia zaidi wakati tunaingia kwenye vifungu. Mheshimiwa ninafikiri umenifahamu, ninakuomba na mimi vile vile kama ulivyoniomba wewe, na wewe umo kwenye *list* yangu. Ninakuomba sana tukubaliane hili tumalize ili tuhakikishe kwamba tunamaliza bajeti yetu kwa muda tuliopangiwa. Halafu tusipoteze muda sana wa kuzungumza wakati muda wenyewe tunaouzungumza ndio huu ambao hautoshi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, sijasema hivyo ili nipate nafasi ya kuchangia, nakusudia kuna vitu, kwanza hujajua Mhe. Naibu Spika, nataka kuzungumza nini, nina *data* nyingi na ambazo zinataka zikafanyiwe kazi, ninaamini kwa haraka haraka kwa muda huu hazitoweza kupata majibu ya kutosha. Hiyo ndio hoja yangu, sasa kama Mhe. Waziri atasema kwamba atajibu hivyo hivyo anavyohisi yeye ni sawa tutakujakuangalia tena kwenye kupitisha vifungu. Lakini hili ninahisi linaweza likaja likatokezea tatizo kubwa sana katika kupitisha vifungu, kwa sababu akinijibu sivyo na mimi nitataka kufanya *clarification*, na vile ninavyojua mimi tutakuja kusokotana kwa jambo ambalo si la msingi sana.

Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, tukubalie. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo unaelewa mwanzo tulitenga kando kanuni ya kuchangia kutoka dakika 30 tukaweka dakika 15 na mambo ambayo ameya-*raise* Mhe. Hamza mimi nadhani yana msingi.

Pamoja na kwamba ninamuamini Mhe. Waziri husika kama angeweza kuyabeba yote na akayatolea majumuisho, lakini mimi naomba Mhe. Spika, tukubaliane na hoja ambayo Mhe. Hamza amei-*raise*, ili tutoe muda wa kutosha kwa Waheshimiwa Wajumbe kuchangia na kumpa muda pia Mhe. Waziri kwa kufanya majumuisho yake pale jioni.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa mnapoteza muda na muda muhimu kwenu nyinyi, sasa makofi hayo yanapoteza muda, ninamshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa mchango wake, labda nimpishe na yeye Mhe. Waziri tumpe nafasi yake ili aweze na yeye kutoa mawazo yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nikubaliane na hoja ya Mhe. Hamza na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, sina upungufu wa kutokuielewa wizara yangu lakini kwa sababu ya kuwapa nafasi Waheshimiwa Wajumbe, watoe maoni yao, niko tayari kuwasikiliza na nitakuja kuyafanyia kazi na kuwapa majibu ambayo yanalingana na maswali ambayo wameyauliza. Isipokuwa yapo baadhi ya mambo yamejitokeza katika michango yanayohusiana na masuala ya *security* siwezi kuyatoa *public*, waelewe hivyo Wajumbe. Nitakuwa na mipaka nayo kwa mujibu wa sheria za nchi na Katiba ya nchi.

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru sana Mhe. Waziri na nimefurahi kwamba mwenyewe Mhe. Waziri ameona kuna umuhimu mzima wa kusikiliza hoja za Wajumbe ambao wameleta maombi yao hapa mbele. Mimi ninashukuru sana na ninafikiria sasa tutaendelea, ninaamini kwamba tutaweza kuwamaliza wachangiaji wote iwapo tutaweka wakati kama tulivyoupanga.

Waheshimiwa Wajumbe nianze kwa mchangiaji wa mwanzo kabisa ambaye alikuwa ni Mhe. Shadya Mohammed Suleiman. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Shadya Mohammed Suleiman aliomba achangie wa mwanzo, lakini kutokana na kadhia iliyomfika Pemba kwa sababu ya mchango wake aliochangia kutokana na hoja ya Mhe. Dimwa, Mheshimiwa kidogo hayuko vizuri ameomba ruhusa kwenda Pemba ili kuangalia familia yake kama iko salama. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa tumuombee dua Mhe. Shadya afike Pemba kwa salama na aikute familia yake salama.

Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Mohammed Mgaza Jecha.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa mara yangu ya kwanza kuweza kuchangia Wizara hii.

Kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchaguliwa kwake akiwa kama ni Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kama hivi ndivyo wakati sasa hivi Rais anasifiwa mpaka *BBC* ambapo sisi tulikuwa hatutegemei kama mpaka Rais wetu wa Zanzibar atasifiwa katika chombo hiki cha nje. Kwa hivyo sasa mimi nawaomba wale wasomi wa Zanzibar waweze kumtungia kitabu Rais wetu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada yake kubwa anayoifanya kwa maslahi ya nchi yetu.

Jambo jengine nilikuwa naomba vikosi vyetu viendelee na tunawapongeza kwa jitihada kubwa kwa kupitia serikali yetu kwa kuilinda nchi yetu.

Jengine nitalolielekea kuhusu masuala ya usumbufu mkubwa wa stendi yetu ya Chake Chake imekuwa ni hatari kubwa sana, sasa usumbufu umekuwa mkubwa, magari yote yanayotokea njia zinazotokea Mkoani wanakuja kuweka stendi pale magazetini na wengine wanaotokea Wete na Chake wanaweka kule maeneo ya Benki. Kwa hivyo nilikuwa ninamuomba tu Mhe. Waziri suala la stendi ya Chake Chake alifanyie ufumbuzi kwa haraka.

Jengine mimi leo sitokuwa na mambo makubwa sana kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, na sehemu yangu nyengine nataka nimwachie baba yangu Mhe. Hamza ili ile nafasi ambayo ataipata za dakika nitamuomba Naibu Spika, amuongeze kwa sababu pengine itakuwa muda wake yeye ni mdogo. Kwa hivyo leo sina makubwa sana, mimi nachangia hivyo, naomba kukaa kitako. *(Makofi).*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ninashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia asubuhi hii ya leo. Mimi kwanza niseme hizi hotuba kusema la ukweli kila inayokuja inamshinda mwenzake kwa uzuri na kwa ubora na kwa umakini zaidi. Ninawashukuru wale wote walioshiriki kwenye kutekeleza na kupanga mipango mizuri ya kuipanga hotuba hii ikapangika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina maswali matatu hapa ya kuchangia kwanza kuhusu suala la magendo. Niwapongeze sana vikosi vyetu wale KMKM kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kudhibiti magendo kule Pemba na hata huku Unguja ninawapongeza sana sana kwa jitihada zile wanazozifanya, kwa sababu kuna watu ambao hawaitakii kheri nchi hii, kuyatoa mazao yetu ya karafuu na mazao mengine katika nje ya nchi. Kwa hivyo nawashukuru na ninawaomba wazidi kuimarisha ulinzi zaidi na wananchi walioitakia kheri nchi hii na kuipatia mapato nchi yetu wawafichue wahalifu hawa wahujumu wa uchumi, wanaotoa karafuu na mazao mengine kupeleka nchi nyengine za nje. Niwatake wananchi washirikiane, wawe kitu kimoja kulijenga taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, hapa hapa kwenye magendo Mhe. Waziri nataka anisikilize kwa makini, Mhe. Waziri sitaki nikufiche kuna mtu yuko ndani ya wizara yako unamlipa mshahara, ndani ya wizara analifanya suala hili la magendo kama sio yeye basi anawabeba watu kufanya suala hili la magendo.

Mhe. Naibu Spika, nina ushahidi kamili, sitokwambia hapa lakini nifuate nitakueleza huyu mtu ni nani na ushahidi upo wa kutosha, kwenye masuala ya magendo ya mafuta.

Mhe. Spika, niende kwenye suala la mapato ya madiko. Mhe. Waziri nikuombe kwenye masuala haya kwa Wilaya yetu ya Chake-Chake kule Ndagoni watu wengi sana asilimia 90 ni wavuvi, wavuvi wale wanapata tabu kupeleka samaki wao Wesha. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri ahakikishe kwamba kule Ndagoni ili mapato yetu yaongezeke, basi iko haja ya kujenga soko la uuzaji wa samaki kule, kwa sababu kuna wengine hao samaki wao hawapeleki Wesha kutokana na usumbufu wanaoupata, na usafiri siku nyengine wanarudi baharini

muda ushakuwa wa jioni na upepo unakuwa mkali. Kwa hiyo, Mheshimiwa ipo haja ya kuweka soko la samaki kule Ndagoni ili yale mapato yetu yasipotee.

Mhe. Naibu Spika, ukizingatia kule kule Ndagoni kuna masuala yale ya madagaa, sasa hivi dagaa lina bei kusema kweli inashinda hiyo karafuu. Kule Ndagoni kuna Wakongo wamehamia na hata kule jimboni kwako Fungurefu wako kule jamaa zangu wa Ndagoni wanazalisha. Kwa hiyo, Mhe. Waziri ipo haja ya kuhakikisha kwamba kule Ndagoni kunawekwa soko hilo ili kudhibiti mapato yetu yasipotee.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la bandari bubu. Mhe. Waziri bandari bubu kusema la ukweli imekuwa ni mtihani sana hususan kule Pemba. Jimbo langu la Ziwani limepakana na Mhe. Khadija Kibano, lakini na hapa nikuombe Mhe. Waziri madiwani wetu na masheha wawe kitu kimoja kushirikiana kuhakikisha bandari bubu hizi kila kijiji chenye bandari bubu basi zinafichuliwa, na wala masheha wasiwe wakaidi kufichua kadhia hii. Kusema la ukweli bandari bubu zinatupotezea mapato sana. Kwa hiyo, Mhe. Waziri nikuombe ipo haja ya kukaa nao madiwani na masheha na wananchi kwa ujumla, tutahamasisha majimboni mule kuhusu suala hilo la bandari bubu, watakapoona masuala yale ya kupitisha mizigo basi taarifa zile zitoke na masheha wasiwe wakaidi watapopewa taarifa nao waifuatilie pamoja na madiwani washirikiane na wananchi ili kuzifichua bandari bubu.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi, mchango wangu ni huo, na Mhe. Waziri nakuomba uufanyie kazi na hilo suala la huyo mtu anayechukua masuala hayo ya kuwabeba watu wa mafuta ya magendo nakuomba Mhe. Waziri unifuate nikwambie na ushahidi upo wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais alisema hapa kwamba tutatumbua majipu na mioyo tutaitoa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri nakuomba hili ni jipu, tena jipu hili halihitaji mkasi wala kiwembe, mwiba wa mchongoma tu unavunja shoka Mheshimiwa nalichukua kabisa kwa sababu limo katika wizara yako. Kwa hiyo, nakuomba suala hilo ulifanyie kazi na ninaiunga mkono hotuba hii asilimia 125. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi hii nikaweza kusema machache.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa tukiwa wazima wa afya

njema, hii si kwa juhudi zetu ila ni uwezo wa Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuwezesha.

Mhe. Naibu Spika, pili niendelee kuwapongeza wale wote ambao walichaguliwa Mawaziri, Manaibu Waziri na Wawakilishi wote wa majimbo ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu kwa leo nataka nianze kwenye Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi kule Pemba miji yetu mikuu ni Chake-Chake na Wete, lakini tunajivunia na sisi kwenye sehemu nyengine kama vile Konde. Hapa ninachotaka nikiseme ni kuhusiana na habari ya *parking*, pale Konde ndio *stand* yetu kubwa kwa kule Kaskazini tunajivunia, na sisi tunaona sote pale magari jinsi yanavyosongamana, nafasi ni ndogo na hasa kukitokezea misafara ya Mawaziri au Manaibu Mawaziri au ya serikali kwa mfano Rais na wajumbe wake inakuwa ni tabu. Kwa hiyo, nataka nimuombe Mhe. Waziri na hili na sisi kwa upande wa kule Kaskazini hususan pale Konde apaangalie sehemu ya *parking* ni mbaya sasa hivi miji inakuwa.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kwenye mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ambao tunaingia, mtihani uliopo ni kwamba watu pale misongamano inakuwa ni mikubwa na hasa wakati huu wa sikukuu unaokuja, Mwenyezi Mungu akitujaalia tukifika salama, watu wote pale ndio wanapopahitajia kwa kutafuta matumizi. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri aangalie kwa kina eneo lile kuona kwamba magari yanawekwa sehemu nzuri na wananchi wanapata sehemu za kufanya shughuli zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwenye Chuo cha Mafunzo na Uokozi. Kisiwani Pemba hususan ndani ya Wilaya ya Micheweni hiki kituo kwenye Wilaya yetu ya Micheweni tuliambiwa kuna sehemu tayari imeshapatikana ambayo itasaidia kuendeleza yale matatizo ambayo yanatokezea ndani ya jimbo.

Sote ni mashahidi kila baada ya muda hutokezea harakati za kuunguliwa moto, moto ambao unatokezea ama kwenye vijiji au kwenye sehemu zetu za misitu.

Mhe. Naibu Spika, najua hii sehemu tayari ilishatayarishwa na serikali, lakini napenda nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba atwambie ni muda gani wa kile kituo pale kitakuwepo na kuanza taratibu zake za kufanya kazi, kwa sababu kila siku husikia tayari kiwanja kishapimwa, pameshapelekwa watu lakini bado

hali inakuwa inaendelea tu kubakia kuwa hivyo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atwambie ni muda gani au ni mwaka gani kile kituo kitakuwa tayari na tukizingatia kwamba haya mambo yanazidi kujitokeza muda mpaka muda.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije kwenye sehemu zetu za vikosi vyetu vya SMZ ambao hawa watakuwa ni KMKM. Sote ni mashahidi na wenzangu wa Kiwengwa walilisema kuhusiana na habari ya zile sehemu ambazo kuna bandari bubu kwa upitishaji wa magendo, lakini vile vile kwa kulinda usalama wa nchi yetu na wananchi wanaoishi maeneo yale.

Hawa KMKM kuna kipindi wanakuwa wanakuwepo ama kipindi cha uchaguzi au kipindi kingine ambacho kitakuwa kuna hofu ambazo zinaweza zikajitokeza. Mimi nimuomba Mhe. Waziri kupitia kitengo hiki kwamba ndani ya Wilaya ya Micheweni najua kipo Msuka, lakini kuna haja ya kuiangalia sehemu ya Tumbe, Micheweni na Kiuyu Mbuyuni kwa kupatikana ofisi maalum na kituo maalum kwa ajili ya hawa KMKM kuwepo pale. Kwa sababu na humu namo ni sehemu ambazo wananchi wanazitumia, lakini vile vile wahalifu wetu pia na wao wanaweza wakajitokeza kwa ajili ya kujipenyeza penyeza.

Mhe. Naibu Spika, kuna kipindi kimoja nilishasahau lakini nilisikia kuliingia Wasomali kule wakaja wakaegesha kwenye maeneo ya Maziwa Ng'ombe, waliowakuta ni watoto wadogo wakawaambia hebu tuagizeni sehemu tuombe moto, lakini baadae wale watoto baadhi yao wakaona wale ni watu wa ajabuajabu ikabidi wapandishe juu kwa usalama wao wakaenda wakamwambia sheha, na sheha akafanya utaratibu nasikia wale watu wakapatikana na baadae serikali ikafuata utaratibu wake unaohusika kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi zaidi.

Kwa hiyo, hili tulione kwamba si kipindi hicho tu na kipindi chengine kinaweza kikajitokeza kwa ajili ya uhalifu au kwa kufanyika masuala haya ambayo sio mazuri katika nchi yetu, na wananchi wanaoishi ndani ya jimbo.

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi siku ya tarehe 05/04/2016 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitoa hotuba yake kwenye Baraza lako tukufu na kusema kwamba miongoni mwa sekta ambazo atazinyanyua kwa ajili ya nchi kuongezea mapato yake na kuwafanya wananchi wapate ajira. Alisema kwenye suala la uvuvi kwamba atawapatia wananchi vyombo vizuri vya kuvua kwa kuwapelekea kwenda sehemu za maji mengi, kupata zana nzuri ambazo zitawapatia samaki hao. Lakini sio samaki tu na sehemu ambayo itapatikana kwa ajili ya soko la kuuzia.

Mhe. Naibu Spika, la kusikitisha sote ni mashahidi kwenye Jimbo langu la Tumbe kuna soko kubwa limejengwa nusu ya hili Baraza lako…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika tatu kumalizia.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, soko lile limekaa mpaka leo hakuna kinachofanyika, kwa hiyo niiombe wizara na nimuombe Mhe. Waziri aliangalie lile soko, najua changamoto zipo zilizojitokeza pale, lakini afanye jitihada zake za juu kushirikiana na waziri wa masoko kwa kushirikiana na waziri wa uvuvi ili waone soko lile linatumika kwa ajili ya wananchi kupata mahitaji yao pale, na serikali kupata mapato yake, kwa sababu lile soko halikuwekwa pale kama maonesho, limewekwa pale kwa ajili ya serikali iendelee kupata mapato yake.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tukizingatia kama mle ndani ya soko kwa wale ambao hawajapata kufika kuna mkahawa mkubwa, kuna sehemu kubwa za kufanya biashara, kwa sababu lile soko limeandikwa soko la samaki na mboga mboga. Kwa hiyo, kule mtakuwa mna mapato mengi ambayo tunayapata, wananchi wamekaa na soko lile limekaa, kuna wakulima wadogo wadogo wa mwani baada ya kwishaanika mwani wao hulitumia kwa ajili ya kuhifadhia mwani wao jambo ambalo sio lengo. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina, ili lile soko lipate kutumika na sisi kuweza kupata chochote.

Mhe. Naibu Spika,…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia na mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja, *inshaallah*. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa mimi nitaondoka sasa hivi na nitampisha Mwenyekiti atakuja kuendelea na majadiliano, na baada ya kuondoka mimi wanaofuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Hamza Hassan Juma, na Mhe. Omar Seif Abeid.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kuweza kunipa nafasi asubuhi hii nikaweza kuchangia maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutufikisha hapa tukiwa wazima na hii leo tuko mbele yako kuendeleza mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote wa Pemba, Wakuu wa Wilaya wote, Wakurugenzi wote wa Pemba pamoja na Makatibu wote wa Halmashauri za Pemba. Nawashukuru sana kwa kufika hapa wao ili kuja kuendelea na shughuli zetu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia niwape pongezi sana kwa utekelezaji wao wa majukumu yao ambayo wanaendelea nayo katika Kisiwa chetu cha Pemba wakiwa katika hali ngumu ya uendeshaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niendelee katika hotuba yetu. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Mgaza na yeye kwa kusimama leo kuanza kuchangia hotuba hii, nampongeza sana, sana, sana.

Vile vile na mimi nimuunge mkono kwa kituo chetu cha daladala kilichopo Chake-Chake, Mhe. Waziri tunaomba hili sote kwa pamoja Wawakilishi tulioko Pemba ulitilie mkazo suala la kituo cha daladala kiliopo Chake-Chake, Konde pamoja na Wete.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wao sisi kutoka Pemba ni mashuhuda tulivyomuona Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba jinsi alivyopambana na madereva waliojikusanya katika Mji wa Chake-Chake, kwa umakini wake na ujasiri wake mzuri alitumia hekima, busara alizopewa na Mwenyezi Mungu akaweza kuwaondosha madereva wale na kuwapa maelekezo mazuri. Kwa hiyo, tunakuomba Mhe. Waziri utakapofanya majumuisho yako utwambie ni mwezi gani ambao utaweza kuondolewa mzozo ule pale katika Mji wa Chake-Chake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niko katika vianzio vya mapato. Katika Halmashauri yangu ilioko Mkoani pale kuna kianzio cha mapato ambacho ni kikubwa na kiko katika diko la Likoni Kengeja.

Mhe. Mwenyekiti, pale wananchi wale wa Kengeja Likoni, barabara yao ni chafu na wao wenyewe wananchi wale wanastahiki sifa kubwa sana kwa

sababu yale mashimo ambayo hayapitiki basi hutia kifusi wao wenyewe ili kuondosha yale matatizo madogo madogo. Kwa hiyo, ningeomba Mhe. Waziri utujuulishe ile barabara inayotoka Ole/Kengeja inakwenda mpaka katika lile diko liliko Kengeja/Likoni au barabara ile haiko kwenye mpango huo? Na kama haiko kwenye mpango huo, basi tunakuomba Mhe. Waziri uwaambie wananchi ni vipi utawasaidia juu ya mpango wa barabara hiyo inayokwenda Likoni katika diko liliopo Mbuyuni.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea ni kwamba tuna tatizo katika diko letu la Wambaa, tungekuomba ukaenda kutembelea kile Kijiji cha Wambaa kwa sababu kuna matatizo tunayaona ni madogo, lakini mwisho wake yatakuwa ni makubwa.

Tunamshukuru kwanza Katibu wetu wa Halmashauri alifanya juhudi kubwa sana kwenda kutoa suluhu kule katika hilo diko kwani wananchi walikuwa wanahitilafiana aidha kama ni kisiasa au kijiji kwa kijiji. Lakini pia hivyo alichukua juhudi ya kwenda kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Wilaya alikwenda akafanya hekima zake, akafanya busara zake pale walimsikiliza lakini hatima yake mpaka jana tunapigiwa simu bado tatizo lile lipo. Kwa hiyo, tunakuomba Mhe. Waziri pamoja na Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa uunganishe kwa pamoja ili waende kuwaona wananchi wa Wambaa na kuweza kulitatua tatizo lile la diko liliopo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nije katika soko letu la Mkoani. Soko letu la Mkoani Mhe. Waziri ukiingia utaliona lile soko lina mapato makubwa sana, lakini Mhe. Waziri lina tofauti. Pale mapato yake sana yanapatikana katika uuzaji wa samaki pamoja na mnada. Lakini katika upande wa matunda lile soko limeanguka sana, matunda pale hayaji kama yanavyokuja kwa wenzetu wa Mji wa Chake-Chake.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Waziri wale wanaokuja pale na zile biashara zao za matunda wanaingia ndani wakanadishiwa kama hawakupata bei wanatoa nje na kuuza mbele ya soko. Je, Mhe. Waziri hii kuuza pale nje ya soko mtu ameshakuja kunadisha ndani hakuuza hatukupata chochote sisi pale, karani akimuendea anaanza kumdharau na kumtolea maneno machafu. Kwa hiyo, tungeomba Mhe. Waziri tupate sheria, uwape makarani wa Baraza la Mji waliopo pale sokoni ili na wao wasipate usumbufu mkubwa. Sheria ikiwepo tayari mfanyabiashara itaanza kumbana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna wafanyakazi wetu ambao wapo kazini kwa muda mrefu, na wengine wameshatimiza miaka kumi na tano kazini, wale

ilikuja taarifa ya kwamba wataongezewa posho fulani katika mishahara yao. Lakini mpaka hivi sasa hatujui kama tayari wameshaongezewa au laa, hawa wafanyakazi baadhi yao Mhe. Waziri wanapoambiwa suala kama hili basi wao huwajengea chuki na fitna Makatibu wa Baraza kuona kwamba hawawalipi haki zao, lakini kumbe bado pengine utata upo ndani ya Serikali.

Mimi ningeomba Mhe. Waziri, uwaelekeze vizuri wafanyakazi ili waweze kujua tatizo lilobidi kutokupewa zile hati mpaka hivi sasa, au kama wako tayari ambao wameshapewa zile haki zao basi vile vile ni vizuri wakajuilishwa ili kuondosha utata kwa wale wakurugenzi wa mabaraza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, katika Mabaraza yetu ya Miji Pemba, katika kuangalia kwangu bado sijaona askari wa mabaraza pamoja na zile Mahakama. Tungeomba na wao kule Pemba wakatengewa wale askari maalum wa mabaraza pamoja na Mahakama zao ili kuondosha usumbufu kwa wale wakurugenzi wa Mabaraza ya Mji.

Kama tunavyojua watu wetu ni wakaidi, wengine wanatupa taka ndani ya misingi wakati ziko sehemu maalum ambazo zimetengwa kwa ajili ya kutupa taka, lakini mtu yule akionekana analeta dharau, analeta jeuri. Mhe. Waziri, naomba uwafikirie sana Makatibu wa Mabaraza ya Mji kuwapatia askari pamoja na Mahakama zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niko katika Kikosi cha Zima Moto. Pale Mkoani ukiangalia bado wale askari wa Zima Moto hawajapata makaazi mazuri. Tungependa Mhe. Waziri, kuwafanyia makaazi mazuri ili na wao wakajiona kama wale ni askari wanathaminika na wanahitajika kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa leo nitamalizia hapo, ahsante sana, nakushukuru sana na mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bahati, sasa anafuata Mhe. Ame Haji na baadaye ajitayarishe Mhe. Hamza. Inavyoelekea watu hawa hawamo, kwa hivyo atafuata Mhe. Omar Seif Abeid akifuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajitayarishe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumza machache katika Wizara hii, Wizara ambayo ndiyo baba wa nchi, imetubeba sote kuanzia Serikali Kuu mpaka Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda nawapongeza wote kwenye Wizara kuanzia Mhe. Waziri mpaka watendaji wake wote wa chini kabisa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja katika mchango wangu nitaanza katika Idara ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika eneo la utawala.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri, atakapokuja basi aje atueleze ni lini Madiwani wetu watapata nafasi ya kuanza shughuli za Mabaraza ya Manispaa pamoja na Mabaraza ya Miji. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hivi nchi yetu inakabiliwa na maradhi ya kipindupindu, na maradhi haya yanahitaji usimamizi wa karibu sana wa masuala ya usafi, sisi pamoja na jitihada ambayo tunaifanya lakini na Madiwani na wao wana nafasi kubwa.

Vile vile ukiangalia mwezi mtukufu wa Ramadhani, Madiwani hawa wanatakiwa wawe karibu sana na wananchi wao, ili kuweza kutekeleza yale majukumu ambayo waliwaahidi wananchi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba tumejaribu kitabu kuna miradi mingi ambayo iliyopangwa programu mbali mbali za ujenzi wa barabara, usafi wa miji, lakini nasikitika sana labda pengine kwa kuwa Madiwani wangu hawajapata nafasi ya kushiriki katika kuandaa hii bajeti nadhani ndio maana kuna baadhi ya programu hazikuingia.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulipitisha sheria ya Serikali za Mitaa, na sheria ya Serikali za Mitaa inatakiwa kwamba sasa hivi tutakuwa na Meya wa Jiji, huyo Meya wa Jiji hapatikani mpaka aweze kuchaguliwa na madiwani katika Halmashauri mbali mbali. Lakini jambo lililokuwepo Mhe. Mwenyekiti, moja katika vigezo vya mji kuitwa jiji basi kuwe na miundombinu ambayo iliyokamilika, barabara zilizo safi, mabustani, lakini vile vile mpaka zile barabara za ndani yaani *feeder roads.*

Mhe. Mwenyekiti, kuna barabara ambayo niliipigia kelele kwa muda mrefu sana, barabara ya Kwa Abasi Hussein, Shaurimoyo, Mboriborini mpaka Daraja Bovu. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii niliibana sana Wizara ya Miundombinu, walikuwa wanasema barabara hii ni ya Halmashauri. Kwa hiyo sasa hivi kwa bahati nzuri kwa kuwa sheria ya Serikari za Mitaa ambayo tumeipitisha kwamba hizi barabara za ndani zitasimamiwa na Halmashauri kupitia mfuko wa barabara.

Nilikuwa naomba tu Mhe. Waziri, aje aniambie basi hii barabara ambayo iliyoanza kutiwa lami kipande cha Kwa Abasi Hussein kuendea Mboriborini, Shaurimoyo mpaka Daraja Bovu itamalizwa lini. Kwa sababu nimeangalia katika programu ya Manispaa ya Mjini kwa kweli haimo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile katika eneo hili nataka nizungumze na Baraza la Manispaa. Namshukuru sana Mhe. Rais kwa kututeulia kijana mahiri kabisa, kijana mdogo Mkurugenzi wa Baraza la Mji Zanzibar, kwa kweli tuna matumaini makubwa, mambo mengi yale ambayo yaliyokuwa yanaleta ukorofi katika mji wetu yataondoka. Sasa nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri, aje aniambie hapa atakapokuja, kuna mkataba ambao tuliufunga wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo, kupitia Sheha wa Shaurimoyo na kikundi cha usafi, tulikubaliana na Baraza la Manispaa kusafisha lile soko la pale Saateni. Na tulianza vizuri lakini mambo katikati yakaja yakaharibika, kwamba wananchi wangu walikosa ile kazi na kwa kweli wamevunjika moyo sana.

Mhe. Mwenyekiti, na katika mkataba ule tulikubaliana wale baada ya kusafisha lile soko wasafishe mpaka na ule mtaro ambao unaotokea kwa Kwa Abasi Hussein, Shaurimoyo kuendea mpaka eneo la Sebleni. Kwa hivyo matokeo yake mkataba ule ulivyokatika kwa kweli hata huu mtaro wa Kwa Abasi Hussein uliopita, Shaurimoyo mpaka maeneo ya Amani Fresh kwa kweli mtaro umekuwa mchafu, taka hizi mtu wa kuyasafisha, nilikuwa tu naomba basi kupitia Mkurugenzi wa Manispaa mkataba huu tukae pamoja na Sheha wangu wa Shehia ya Shaurimoyo ili kuu-*review* na kuangalia namna gani tutaweza kuweka safi mji wetu. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la Manispaa ya Zanzibar, mimi nafikiri labda niishie hapo lakini nije katika Idara ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo ambalo sijaridhika na bajeti hii ni eneo moja kwa mawili, na hili ambalo nitataka nilitaje.

Nimejaribu kuangalia katika kitabu cha Mhe. Waziri, ameeleza huu mradi ambao ni wa *CCTV Camera*; mradi huu kwa kweli ulitengewa bilioni kumi kipindi kilichopita, lakini mpaka kipindi hiki tunaambiwa tayari wameshapata bilioni nne, na katika bajeti hii sijui kama imejikanganya au maelezo yanajikanganya lakini yeye atakuja kutupa taarifa, suala zima la mradi huu kwamba umeombewa tena fedha karibu bilioni kumi na nane, lakini ukiangalia kwenye kitabu wanasema bilioni, kwa hiyo maelezo yanajikanganya. Lakini pamoja na kwamba maelezo haya yanajikanganya Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulikuwa ukizungumzwa sana, umekuwa ukizungumzwa sana, na kwa kweli yale mazungumzo yaliyozungumzwa hata na mimi hayajaniridhisha. Na kwa

sababu kwanza ubora wa hiyo kampuni, upatikanaji wa kampuni, lakini vile vile manunuzi na ile ubora wa vile vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha kampeni kulitokezea vurugu nyingi sana, miongoni katika hawa waliopata matatizo kuna kijana wangu mmoja alipigwa vibaya sana akavunjwavunjwa uso, akaburuzwa akapelekwa mpaka Mtendeni, lakini katika kufuatilia katika hizo *CCTV Camera* akaja akaambiwa *camera film* ina kiza haonekani. Sasa mimi sitokubali kupitisha fungu hili Mhe. Mwenyekiti, na vile vile nitaomba kwa ridhaa ya Wajumbe niruhusiwe nitumie Kanuni ya 120, ili Baraza hili liunde Kamati Teule iende ikaangalie ule mradi kuanzia tokea masuala ya tenda, masuala ya *procurement,* lakini vile vile na masuala ya utekelezaji katika shughuli hii ili tujiridhishe katika kupitisha mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, bilioni kumi na nane sio pesa kidogo, hii bilioni kumi na nane imo katika *figure* lakini katika kitabu bilioni kumi, fedha hizi ili tujiridhishe sio kama tunakataa ule mradi, mradi mzuri utaleta usalama katika nchi yetu, lakini lazima tujiridhishe ubora wa hiyo kazi inayofanywa, na turidhike na hiyo kampuni inayofanya hiyo kazi tupate taarifa za kutosha, wamewahi kufanya kazi wapi na wapi duniani ili tupate kuja kuridhia fungu baadaye.

Kwa hiyo mimi nita-*suspend* fungu hili, baadaye baada ya kujiridhisha pengine katika kikao kinachokuja baada ya miezi mitatu tunaweza tukaja Mhe. Waziri, fungu hili akaendelea kulitumia baada ya kuridhika, kama hatukuridhika na ubora wa kampuni na masuala ya *procurement* kama hayakufuatwa suala hili itabidi tuikoseshe kazi, itafutwe kampuni nyengine ambayo itakuwa na uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya si mageni, wenzetu kule Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshaona, kuna kampuni mbali mbali zimeshanyimwa kazi kutokana na kiwango kidogo cha ubora wa kazi zao.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kama nilivyosema natumia Kanuni ya 120 katika kuliomba Baraza lako tukufu baadaye iunde Tume tuende tukachunguze, tukijiridhisha tutakuja kulipitisha fungu hilo, tutamruhusu Mhe. Waziri, aendelee na kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nilikuwa nataka nijue *ZUSP*, mradi wa *ZUSP* nimeupigia kelele sana hapa Barazani. Naishukuru Serikali kupitia Tawala za Mikoa, Mhe. Waziri aliniahidi sana, na sasa hivi namshukuru mradi tayari umeanza, lakini umeanza pembeni pembeni, ule mtaro mkubwa wa Jimbo

unaopitia katika Jimbo la Kwamtipura kupitia Daraja Bovu mradi ule mpaka leo bado haujaguswa, tulikuwa tunaambiwa kuna tatizo la kuwalipa wananchi fidia ili zivunjwe nyumba zao upate kujengwa mtaro, basi Mhe. Waziri, atakapokuja hapa naomba aniridhishe katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nilikuwa naomba, kwa kuwa tumeridhia hii sheria ya Serikali za Mitaa, basi halmashauri sasa zipewe nguvu, Wizara ising'ang'anie sana kila kitu. Kama tulivyosema kuna ugatuzi wa madaraka, sasa hii baadhi ya miradi na ubunifu wa miradi waruhusiwe sasa hivi Makatibu wa Halmashauri waweze kubuni miradi, waweze kuingia mikataba ili tuhakikishe kwamba Halmashauri zetu nazo zinapiga hatua za maendeleo na kutuletea maendeleo katika Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Kituo cha Daladala. Mheshimiwa hili suala bado limekuwa tatizo, kuna vurugu kubwa pale Darajani, pale Ofisi Kuu ya Kisiwandui samahani, kwa kweli bado haliridhishi. Tunaomba Mhe. Waziri, basi aje atupe mpango maalum au mpango mahsusi wa Serikali ni namna gani Serikali yetu itaweza kutuwekea kituo cha daladala katika Mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Idara Maalum. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nimesikitika sana, nimesikitika sana nilipoona ile Tume ya Utumishi wa Idara Maalum katika bajeti iliyopita, walitengewa karibu milioni mia moja thalathini na nane ambazo walizotegemea kutumia katika *OC* zao ni milioni mia moja ishirini katika miezi tisa. Lakini cha kusikitisha kabisa, wamepewa milioni saba tu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili suala mimi kwa kweli sikufurahi nalo, labda Mhe. Waziri, aje atupe basi hiyo sababu, kwa sababu kuna maeneo mengi yametiliwa fedha nyingi karibu asilimia 90 huku wenzetu hawa wamewekewa karibu ya asilimia sawa.

Mhe. Mwenyekiti, na hili Mhe. Mwenyekiti, nafikiri pia moja katika kosa tulilolifanya sisi kwenye Baraza la Wawakilishi, tulivyofanya marekebisho ya Katiba, tulipoiweka ile Ibara ya 116 ya Katiba ya Zanzibar kuweka ile Kamisheni ya Utumishi wa Umma ikawa ni *overall* au *in charge* wa kamati zote zile za utumishi. Kwa kweli inaonesha hata hawa wenzetu Tume ya Utumishi ya Idara Maalum tumeinyang'anya, tumeipunguza nguvu, matokezeo yake maamuzi yao, kwa sababu Tume ya Utumishi moja katika majukumu yake kuhakikisha wanaangalia na kutathmini na kufanya mapitio na kupeleka mapendekezo ya suala zima la *scheme of service* ya Idara Maalum.

Matokezeo yake Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Tume hii inaonesha haikufanya kazi vile ipasavyo hasa kwa sababu hatukuingizia pesa, ndio maana ikafika

pahala suala zima la maslahi ya askari wetu wa idara maalum ndio maana ikafika pahala Mhe. Rais, ikabidi alitolee kauli wakati wa kampeni.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Tume hii kama ingelikuwa inafanya kazi vizuri ingekuwa imewezeshwa vizuri wangelipendekeza maslahi ya askari wetu wa Idara Maalum ili wapate maslahi yaliyo bora.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani iko haja ya kufanya marekebisho katika kifungu kile na Tume ya Utumishi sasa isiwe juu ya hizi Tume nyengine ambazo hapo mwanzo zilikuwepo vile vile kisheria. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, suala zima la askari wetu kuwalipa vizuri kwa kweli huo ndio tunajihakikishia ulinzi wa kutosha na umakini katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Idara Maalum nilikuwa naomba sana Mheshimiwa katika hili zoezi la ukamataji wa ng'ombe na mbuzi na paka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi nilikuwa naomba tu makamanda wajaribu kuwaambia vijana wetu wasitumie nguvu kubwa sana ya kupita kiasi. Kitendo kilichofanyika hivi karibuni katika eneo la viwanda vidogo vidogo, pale pana ulinzi wa Serikali, na ulinzi ule umewekwa kwa sababu mule ndani muna maeneo mbali mbali ya uwekezaji, makampuni mbali mbali yamewekeza pale pale. Sasa Mhe. Mwenyekiti, wanapokwenda bila ya kushauriana na walinzi, wakaenda wakavamia mule katika lile eneo, kwa kweli hili jambo kwa kweli lilikuwa halikupendeza sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sasa nitaomba niende katika fungu D06 Kikosi cha Valantia. Mimi kwanza navipongeza vikosi vyetu vyote vya SMZ, kwa kweli vinafanya kazi vizuri sana, lakini nitaomba katika kile kifungu kile cha 120 nitaomba niunganishe na suala hili twende tukalifanyie utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna matumizi mabaya ya askari na kuna matumizi mabaya ya rasilimali za Idara ya KVZ. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema ilikuwa kuna vitu nitavitaja ili Mhe. Waziri, aje anipe zile taarifa za uhakika kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nitaomba nitaje namba za gari halafu nije nipewe maelezo gari hizi ziko wapi na zimefanya nini na zinatumika vipi. KVZ 001, KVZ 002, KVZ 003, KVZ 005, KVZ 007, KVZ 105 na KVZ 108, lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna matumizi mabaya ya askari, askari nitakaowataja

hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na nidhamu ya kiaskari sitawataja majina, lakini nitaomba nitaje namba zao kwa sababu Mhe. Waziri na yeye mwenyewe ni Kamanda nikitaja namba yeye mwenyewe atawajua, nataka nijue hawa, hivi sasa hivi tunavyozungumza wapo wapi na hiyo kazi wanayoifanya kama kweli wametumwa na kikosi.

Mhe. Mwenyekiti, askari MV 0271, MV 0386, MV 0609, MV 1216, 0420, MV 0873, MV 1139, Askari MV hawa wote ninaowataja ni MV wanaanzia, 0404, 0408, 03048, 0699, 0510, 0619, 0406, 0318, MV 0619, 1281, 0410 na hawa wengine kuna hawa askari ambao wanafanya kazi za *welding* nitakuja kumtajia majina katika wakati muafaka lakini vile vile na huyu mmoja ambaye anakata majani.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umemaliza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema maelezo yangu mengine Mhe. Waziri nitampelekea kwa maandishi, ili baadaye nije ufafanuzi kwenye vifungu. Mhe Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote nashukuru kunipa nafasi hii muda mdogo lakini tutakwenda mbio mbio Mheshimiwa.

Kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri, Waziri mahiri. Lakini pamoja na hayo sambamba nachukua nafasi hii kuwapongeza kama kawaida yangu, viongozi wetu wote Wakuu wa Nchi, Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamo wa Pili wa Rais, Waziri wa Fedha, Mwanasheria Mkuu na Mawaziri wote wa Serikali hii na Manaibu Waziri wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo kwa sababu ya muda naomba niende mbio mbio ili nipate kuchangia kwa kadiri nitakavyoweza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi napenda kuchukua nafasi hii kuuzungumzia mji wangu wa Konde. Kama tunavyoujua mji wa Konde katika miji ya Pemba ni mji unaokua kwa kasi sana, katika programu ya kufunga taa za barabarani sioni Konde kwamba imo katika miji itakayofungiwa taa hizo, ukizingatia kwamba Konde ni mji wenye vianzio vingi vya mapato.

Sisi Konde pale tuna mahoteli ya kitalii kwa eneo la Makangale, tuna ufukwe mzuri wa Vuma Wimbi, tuna Msitu wa Ngezi na mambo mengine. Kwa hiyo,

kukosekana kufungwa taa za barabarani ikaondolewa kwenye ile programu ya miji itakayofungiwa taa jambo hili linasikitisha.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atapokuja anambie ni lini au na mimi mji wangu huo utaingizwa katika miji itakayofungiwa taa za barabarani, ijapokuwa najua mambo haya yanatokana na ufadhili, lakini waziri auone mji wa Konde kama ni mji muhimu kwa Pemba.

Jambo la pili namshukuru Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe kwa kunisaidia kazi ya kuitaja *stand* ya Konde. Lakini mimi sitaji *parking* nataja *stand.*

Mheshimiwa kama unavyofahamu Konde ndio inachukua miji yote ya Wilaya ya Micheweni, magari yote ya Micheweni yanakusanyika Konde, lakini jambo la kushangaza ni kwamba hatuna *stand*. Kwa hiyo, naiomba wizara ikishirikiana na halmashauri kutafuta eneo ambalo litakuwa na *stand* ya kudumu ya magari. Ukitilia maanani kwamba *stand* ya Wete sasa hivi pana ujenzi wa soko la kisasa, unawahamisha *stand* ya Wete, ina maana hapatakuwa na eneo la kuweka magari. Sasa tujiulize gari za Wete zitasimama wapi? Hivyo, naiomba wizara pamoja na Halmashauri ya Wilaya kuliangalia hili ili kupata nafasi ya kujenga *stand* nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, niende mbio mbio nije kuhusu habari ya ujenzi wa mji wa Konde. Mheshimiwa ni jambo la kusikitisha kuona kama mji wa Konde sasa umeanza kupoteza haiba yake ya ujenzi, kwa sababu mji ule inaonekana kwamba toka mwaka 1965 ilianzwa kuingizwa katika ramani ya mipango miji. Lakini leo mji wa Konde umekuwa unajengwa holela pamoja na kwamba serikali inafanya bidii kubwa ya kuupima mji huo na kuuweka katika ramani, lakini mpango huo unaonekana hautekelezwi. Kwa hiyo, naiomba wizara pamoja na Halmashauri ya Wilaya ikishirikiana na Idara inayohusika ya Mipango Miji iliangalie kwa kina na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaovunja sheria za ujenzi wa mji.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu barabara za ndani ambazo zitakuwa chini ya Halmashauri. Kama nilivyoeleza kwamba Mji wa Makangale ni mji muhimu, barabara hii inaingiza watalii wengi wanaopita katika Msitu wa Ngezi. Lakini ukipita katika Msitu wa Ngezi katikati pale utakuta ni sawasawa kuna watu wanaotoka Makangale na wanaotoka Konde, mvua zikinyesha huwa hapapitiki.

Zamani kulikuwa na utaratibu wa kutaka kuijenga ile barabara japo kwa kiwanho cha kifusi iwe wakati wote inapitika kutoka Msitu wa Ngezi hadi Mnarani. Kwa hiyo, pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aniambie na yeye

barabara ile ya kutoka mwanzo wa msitu mpaka Makangale lini itajengwa, japo kwa kiwango cha kifusi ili iwe inapitika kwa wakati wote, ukitilia maanani barabara ile ni muhimu, ina wageni wengi, watalii, lakini usalama ni mdogo, hata viongozi wetu wa kitaifa wakipita pale mimi sidhani kama kuna usalama. Kwa sababu msitu ulioko pale ni mkubwa, barabara ni mbovu zinajaa mashimo. Kwa hiyo, waziri atakapokuja na hili aniwekee wazi.

La mwisho ni ufufuaji wa mitaro iliyoziba katika mji wa Konde ambayo mitaro hii imejengwa toka enzi za Ukoloni.

Mhe Mwenyekiti, pia nataka ufafanuzi wa mitaro hii kama bado halmashauri inaitambua kama kuna mitaro ya asili pale Konde. Kama wanaitambua vipi wanaitunza, kwa sababu sioni matunzo yaliyopo ya mitaro hiyo watu wanaijenga wengine wameanza kuiziba kabisa ina maana maji hayaendi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kwenye mji wangu nakimbia mbio sasa nataka niende kwenye Vikosi Maalum vya KMKM. Mheshimiwa mimi nina ombi maalum kwa Mhe. Waziri, nataka hili alitizame kwamba kambi ya KMKM iliyopo Msuka iko hatarini. Kambi hii miaka 15 iliyopita ilikuwa si chini ya mita 300 kutoka kwenye bahari, sasa hivi labda kama inazidi ni mita 40. Bahari imeanza kuichukua kwa kasi ardhi hiyo, na sasa hivi wavuvi wanafanya kazi yao kwenye kambi ya KMKM si zaidi ya mita 30 kutoka ilipo kambi hiyo, jambo hili ni hatari kwa usalama wa kambi.

Kwa hiyo, naiomba serikali kupitia wizara hii ione jambo hili na ichukulie hatua za dharura, kwamba ili kuilinda kambi ile ni lazima hatua za dharura zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kuzuia mmong'onyoko wa kambi ile kwa eneo lile la kambi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio hilo tu, sambamba na kuwahamisha wavuvi na wachuuzi wanaofanya kazi pale wawapeleke kwenye soko lililojengwa. Kwa hiyo, naiomba Halmashauri ya Wilaya na wizara wafanye kila linalowezekana kuhakikisha kwamba soko lile linamaliza ndani ya mwaka huu, na wavuvi na wachuuzi wanafanya shughuli zao ndani ya soko lao ili kuipa uhuru kambi kuweza kufanya mambo yake ya ulinzi. Kwa sababu siamini mimi pale kama itatokea vurugu yoyote au kuna askari wataweza kujitayarisha hata kuilinda ile kambi, kwa sababu wavuvi na wachuuzi sasa hivi wapo si zaidi ya mita 30 kutoka kwenye kambi, tena mbele ya kambi sio mita 30 ubavuni, ni mbele ya mlango kwa upande wa baharini.

Mhe. Waziri naomba akija hili anithibitishie lini kazi hii itafanywa na naamini nitapata majibu ya kuniridhisha, sina wasiwasi wa hilo. Lakini ili roho yangu iridhike nataka nisikie ili na mimi nijiridhishe na watu wangu pia.

Pia kuhusu kambi hizo hizo za KMKM kambi ya Msuka inatumia boti itakapotokewa na dharura, lakini tujiulize kama itatokea dharura bahari imechafuka mahitaji yako Wete vipi wataweza kufika. Kwa hivyo, naiomba wizara kwenye bajeti ijayo iangalie kambi hiyo kwamba ni jambo la muhimu kuwapatia gari, kuweka gari moja pale kwa ajili ya dharura inapotokea askari waweze kuitumia kwa mahitaji yao. Sambamba na kambi hiyo, pia napendekeza na kambi ya Gando na Sengenya, sina uhakika kama kambi ya Sengenya wanayo gari au vipi, kwa sababu naijua na zamani nilikuwepo pale kwa hiyo nayo naomba waziri alichukue hili aone kama ni jambo la muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Idara ya Vizazi na Vifo. Idara hii imekuwa kuna changamoto kubwa hasa kuhusu upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Pamoja na mambo yote hata wale watoto wanaozaliwa hospitali wazazi wao wanaweza kuchukua mpaka mwaka mmoja kupata vyeti. Kwa sababu waziri ametwambia kuwa kuna mpango wa kutoa vyeti kwa njia za elektroniki, nataka akija anambie lini mpango huu utakamilika kwa ajili ya mikoa yote ya Zanzibar na wilaya ili kuondoa tatizo la vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama tujuavyo kuwa cheti cha kuzaliwa ndicho kinachokupa wewe kuwa na haki ya uraia. Pamoja na mambo mengine kuwa yapo, kwa sababu unaweza kuwa raia wa kuomba ukupata, lakini uraia wa kuzaliwa kwa sasa hivi ni kuwa na cheti cha kuzaliwa, ukifika umri wa miaka 18 utapata kitambulisho chako cha Uzanzibari na Utanzania. Sasa kinapokosekana cheti cha kuzaliwa ndio mwanzo wa kumkosesha raia haki yake ya uraia. Kwa hiyo, mimi naomba sana kwamba suala la vyeti vya kuzaliwa kwa watoto lichukuliwe uzito unaostahiki.

Sambamba na hilo lakini kuna tatizo jengine ambalo nimeliona na linaigusa jamii kwa hali ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Aaa, Mheshimiwa naomba tena tano unipe. Kuna tatizo la vyeti vya kuzaliwa hata kwa watu waliozidi miaka 40. Tunawashuhudia watu wengi wanaotaka kwenda Hijja kutengeneza *passport* inawawia vigumu kuipata. Sasa mimi namuomba waziri kwamba suala la vyeti vya kuzaliwa kwa watu wazima waandae utaratibu maalum kuwatambua wale

wenye umri zaidi ya miaka 40, ambao hawana vyeti, wapatiwe vyeti ili inapotokea haja ya muhimu kwenye vyeti vya kuzaliwa waweze kuvipata kwa urahisi. Kwa sababu unapotaka kutengeneza *passport* kama huna cheti cha kuzaliwa hata kama unataka kwenda wapi inakuwa ngumu kwako. Kwa hiyo, namuomba waziri hili alitazame sana.

Mwisho ni ombi langu la kupandishwa vyeo kwa askari wetu walio chini. Mheshimiwa namuomba Mhe. Waziri hili alichukulie kwa uzito unaostahiki, la watumishi wetu kuwaongeza vyeo, japokuwa ni mzigo lakini kwa sababu ni haki yao ya kisheria waongezwe vyeo kwa mujibu wa muda wao unapofika, ili kuondoa manung'uniko ya baadhi ya watendaji wetu hasa kwenye wizara hii kwamba wanacheleweshwa kupandishwa vyeo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nasema naunga mkono hoja hii, lakini pia namuomba Mhe. Waziri atapokuja anipe majibu mazuri ya maelezo yangu haya. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kukupongeza kwa kuwa Mwenyekiti kuendesha kikao hiki.

Pili naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kaka yangu Mhe. Haji Omar Kheri kwa kuleta bajeti yenye kuweza kutekelezeka na mimi namuamini anaweza kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu lakini kabla sijatoa naomba ifahamike kwamba, lengo kuu la mchango wangu utakuwa ni kukumbusha uwajibikaji, matumizi bora ya fedha, huduma bora kwa wananchi, wakulima na wakwezi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia. Mheshimiwa nchi yetu ni Zanzibar, inaongozwa na Serikali ya Mapinduzi. Nchi hii imepatikana kwa njia ya Mapinduzi, Rais wetu anajulikana kama ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Serikali zinazoongozwa Kimapinduzi duniani ziko sita kama sikosei moja ikiwa ni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Zanzibar ni nchi ya Mapinduzi, mambo yake yote yatakuwa ni ya Kimapinduzi. Sasa kwa hapa naomba kusikitika, niliwahi kumsikia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akisema kwa kauli kubwa ya kimapinduzi kwamba hataki kuwaona ng'ombe mjini. Ni

kipindi kisichopungua au kuzidi miaka mitatu sasa hivi bado ng'ombe mjini wapo, wanyama wapo, na hili ni agizo la Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi.

Ni jambo linaniudhi, linaendelea kuniudhi, linanikera na niliwataka waheshimiwa wenzangu kwa hili, kwamba hii kauli ya Rais wa Mapinduzi haijatekelezwa basi twende kwenye kura. Lakini juzi nilipokuwa jimboni kwangu niliona imeanza kutekelezwa kauli hii. Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri, hivyo kwa nini kwa kipindi chote kauli ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo inakuwa ni agizo imechelewa kutekelezwa? Namuomba Mhe. Waziri aje kunijibu, kwa sababu kitu hiki kuchelewa kutekelezwa kimeleta *bad image* kwa jamii ya wanamapinduzi, wakwezi na wakulima wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kumuuliza Mhe. Waziri kuwa lini zoezi hili la ng'ombe litakamilika mjini, nimeliona limeanza lakini lini wanyama hawa tutakuwa hatuwaoni tena mjini, hasa ukizingatia ni agizo la Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mchango wangu wa pili utakuwa ni kuhusu usafi wa mji. Mheshimiwa tunajua umuhimu wa usafi katika maendeleo ya mji wowote ule, katika watu, jamii ya aina yoyote, lakini sio siri mji wetu wa Zanzibar ni mchafu, bado usafi wake hauridhishi na sisi tunategemea. Ndio maana maradhi ya kipindupindu na mengine hayeshi kutujia kwa sababu mji huu hauridhishi usafi wake.

Pia tunategemea watalii katika kupata pesa za kuishi kila siku za maisha yetu, na watalii wanahitaji mazingira mazuri ili waweze kumsifia mtu mwengine. Tembelea Zanzibar kwa sababu Zanzibar ni safi, nzuri, lakini unapokuwa mji mchafu kama hivi mtalii anashindwa kumsifia mtu mwengine kwamba tembelea Zanzibar, kwa sababu mji wake ni msafi, bali hapo anakuwa anaficha anasema kwa mfano, *it's okay,* inakuwa haitoshi anatakiwa aseme msafi tembelea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri maswali yangu yafuatayo anijibu. Je, kuna majaa mangapi katika Manispaa ya Zanzibar na yana utaratibu gani wa kusafishwa kila siku na kuchukuliwa taka, mara ngapi kwa siku? Vipi utaratibu wanaoutumia kuziangamiza hizo taka, kwa sababu tuna wasiwasi utaratibu wanaoutumia kuangamiza taka hizo ni mbaya na mbovu haufuati *policy* ya *Waste Management* ya dunia na unasababisha maradhi, sasa anijuze ili nifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo nitahamia katika mchango wa *CCTV Camera*. Kwanza nimsifu sana, nimpongeze tulipofikia dunia nzima sasa inalindwa na uleo, *CCTV Camera.* Uingereza wamefanikiwa sana hata ufanye jambo lolote baya kichochoroni watakukamata kwa sababu wana *better CCTV Camera System.*

Dunia nzima, mimi nimpongeze sana kama ilivyokuwa mji wetu una watalii lazima tuulinde kwa *CCTV Camera*, lakini sisemi uongo mimi ni mwananchi mwana Mapinduzi nawapenda sana wakulima na wakwezi wenzangu wa nchi hii, pesa ni nyingi mno.

Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri maswali yangu, je, utaratibu gani uliotumika kumpata yule aliyepewa hii *tender* ya kusambaza au ku-s*upply CCTV Camera* hapa Zanzibar? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili, naomba kujua kampuni mbili au tatu zilizoshindana na kampuni hiyo mpaka ikafikia kampuni hiyo kuwa kampuni bora na kupewa *tender* hiyo.

Swali langu la tatu, kampuni hii imefanya kazi wapi ya kufunga hizi *CCTV Cameras* duniani au Afrika kwa jumla.

Swali langu la nne je, kampuni hii imetoa *warrant* au *guarantee?* Hizi *International Companies* zinapokuja kufanya kazi nchi za Kiafrika lazima zitupe *warrant*, zina *warrant* wa miaka mingapi kwa hizi *CCTV Camera* kama zikiharibika bado liwe jukumu lao kututengenezea kamera zetu, anambie *warrant* ni miaka mingapi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa nne utakuwa ni taa za barabarani. Kwanza niipongeze sana wizara hii, mji wetu umeanza kung'ara. Miaka ya 1980 ulikuwa unang'ara na sasa hivi umeanza kung'ara. Lakini mimi nina wasiwasi, taa za barabarani hizi ndio kwanza zimefungwa juzi lakini zinasinzia, na nyengine zimeshaanza kuwa mbovu, ukiuliza waliokuwa si wataalamu wanakwambia kwa sababu siku za wingu. Nchi za baridi mimi nimetembelea kidogo unazikuta kuna taa zinaendea *solar power*, lakini miezi minane yote ni baridi na taa zake zinafanyakazi kama kawaida.

Hizi zetu je, kwa nini ziko hivyo na hizi zina *warrant* wa miaka mingapi kwamba zikiharibika bado waweze kututengezea tuliowapa fedha hiyo. Kwa sababu nina wasi wasi maneno ya watu wa mjini ikawa tumeshapigwa *changa la macho* hapa.

Kwanza niwasifu sana makamanda hawa wa Vikosi vya SMZ wao wanatakiwa kunipa saluti mimi lakini mimi nitawapa wao, wanafanya kazi kubwa sana nzuri.

Tukianza na kikosi cha KMKM napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Komodoo wa Kikosi cha KMKM. Mkuu wa Utawala, na Wakuu wengine wote wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Pia Mkuu wa Chuo cha Mafunzo; Kamshina anafanya kazi nzuri sana namuomba aendelee. Mkuu wa KVZ anafanya kazi nzuri sana, Mkuu wa JKU anafanya kazi, Zima Moto wanafanya kazi nzuri sana. Mhe. Spika, naomba watu hawa waendelee kufanya kazi, kuwatumikia wakwezi na wakulima, wanamapinduzi wa nchii hii.

Lakini ukikaa na maaskari baadhi yao kuna haki zetu, tunanyimwa, tunanyang'anywa, tunadhulumiwa, ni ndugu zetu na jamaa zetu. Naomba Mhe. Waziri akae atizame kama zipo haki hizo wanazonyimwa na kudhulumiwa kama wanavyolalamika baadhi ya maaskari wapewe, hawa ni watu muhimu, watu hawa tunawahitaji, tunawategemea.

Pia Mhe. Rais aliahidi kuwaongezea mshahara. Namuomba Mhe. Waziri ajitahidi kila uchao watu hawa awaongezee mshahara ili walingane na Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya Tanzania kama alivyoahidi Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba hawa vikosi hebu tubadilishe sera jamani na sheria. Mfano KMKM waweze kujiunga na kampuni binafsi ya uvuvi iwe nchi hii Kampuni ya Uvuvi kwa mfano ya Japan imeshirikiana na KMKM. KVZ waweze kutoa ulinzi tumechoka na hawa wa *KK security* wanachukua mapesa mengi bila ya mafanikio na vikosi vyetu vipo.

Mhe. Mwenyekiti, tuanze kubadilisha sera za vikosi ili waweze kuingia katika *PPP*. Nchi kama Marekani, Canada, Ghana vikosi hivi vimefanya na vina maendeleo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakuja kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Sheria namba 8 kama sikosei inaweka uwepo kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa, namba 14 ya sheria hiyo inawazungumza Wakuu wa Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya ni watu muhimu na nawapongeza wote, na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kaka yangu Ayoub na Wakuu wa Wilaya wote nawapongeza hawa na Makamadoo tunawahitaji wafanye kazi.

Lakini hawa hasa hawa Wakuu wa Wilaya jamani magari hawana, mabovu, yanatia aibu, ukiambiwa hii ni *DC,* Mkuu wa Wilaya hili gari lake, ni hili bovu linatia aibu. Mhe. Waziri nakuomba wape gari nzuri zinazolingana na hadhi yao. Lakini hawa Wakuu wa Wilaya hasa Mkuu wangu wa Magharibi "B" gari yenyewe hana. Wapewe gari kulingana na cheo chao. Lakini pia wapewe na pesa basi, kwa sababu hawa ndio huduma ya kwanza kwa hizi wilaya; mtu aliyeibiwa, aliyekamatwa na polisi, mtu aliyeingiliwa na nyumba anakimbilia kwa Mkuu wa Wilaya na akifika huko kwa Mkuu wa Wilaya shilingi mwenyewe hana, wawezeshwe wao na kijimfuko pale *cash cash* ya kuwasaidia wale waliopata maafa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye ile Mamlaka ya kutoa vyeti vya vizazi na vifo. Mhe. Mwenyekiti, wana *special storage* kule kwao ya kuweza kuhifadhi vile vyeti na zile kumbukumbu ya vile vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna *AC* kule, na vile vyeti kule vinatakiwa kuwa na *AC* ili viweze kuishi kwa muda mrefu. Tumetumia pesa nyingi kujenga nyumba, tumetumia mambo mengi kuweka kila kitu, lakini baadae kwa sababu tunakosa kitu kidogo kinaitwa *AC* vile vyeti vinaharibika. Madhali tumethubutu kufanya hivi hebu tumalize jamani ili tuweze kwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi leo lakini naomba kusema kwamba mambo yote haya niliyoyaeleza Mhe. Waziri aje kunijibu kwa kina, kama nilivyosema mwanzo na muda wangu bado ninao unaniruhusu nilikuwa nimejipanga kuzuia shilingi dhidi ya kuchelewa kutekelezwa agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar kwamba hataki kuwaona ng'ombe na niliwaomba wenzangu wamenikubalia. Kwa sababu nimeona opresheni imeanza anijibu tu halafu sitozuia shilingi kama nitajibiwa. Lakini yote haya niliyoyasema leo kama sikujajibiwa kwa kina kabisa na ikiwemo siasa ndani yake kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibari leo sitokuwa mkali lakini nitafanya kazi yangu kwa mujibu wa Katiba ibara ya (88) (c).

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika napenda kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Waziri na Mawaziri wote sisi *backbencher* tunapowauliza wasinune, kwani tunafanya kazi yetu kwa mujibu wa Katiba, wala wasi- *mind,* lengo kuu ni kujenga nchi kwa maslahi ya wananchi. Nchi ya wakwezi na wakulima, waliotupatia nchi, wazee wetu kwa njia ya kupindua. Kuna jukumu la kuwatetea wananchi wakwezi na wakulima hawa ndio waliotuleta humu. Mimi nimeletwa na wananchi wa Welezo wameniagiza nije kuwatetea.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo leo sina mengi mambo yangu ni hayo kidogo, lakini nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri na wengine wasinune tufanye kazi kwa kushirikiana, lengo ni moja tu, kujenga na kuleta maendeleo kwa wananchi wakwezi na wakulima wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake na kwa kuja kuwasilisha katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mimi kama wenzangu walivyotangulia kuchangia nitaomba kwanza ufafanuzi. Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi katika kitabu chake cha hotuba ukurasa wa 82 kiambatanisho namba 6 kuna miradi ya maendeleo ambayo iliyofuatiliwa kwa kipindi cha Julai 2015 mpaka Machi 20126.

Miradi hii waliyoitembelea ipo katika mikoa mbali mbali na ikiwemo katika Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja, na nimeona kwamba baadhi ya miradi iliyotembelewa ikiwemo baadhi ya uchimbaji wa visima 17 katika Mkoa wetu wa Kaskazini ikiwemo katika Shehia ya Pangeni na Shehia ya Upenja na Shehia hizi ziko kwenye jimbo langu. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anitolee ufafanuzi visima hivi vimechimbwa kupitia Halmashauri au wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea nitazungumzia suala zima la ajira. Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar yaani JKU linaelimisha na kutoa elimu kwa vijana wetu ambao wanajitolea au wanajenga Taifa kwa kipindi cha miaka mingi. Namuomba Mhe. Waziri kwanza atizame kwa kina kwamba vijana hawa ni wengi kila mwaka wanakusanyana. Kwa hivyo, kumekuwa na mrundikano wa vijana wengi na umri wao sasa hivi umekuwa mkubwa, na kwa kuzingatia kwamba vijana wengi wanakwenda JKT na wengine JKU, lakini unapofika wakati wa ajira basi vijana wale wanaambiwa wamepita umri.

Je, kwa vijana hawa si tunawavunja moyo kupitia serikali yao na hatuoni kwamba tunasababisha mrundikano wa vijana ambao wasio na ajira katika serikali yetu, na wanaweza kujitumbukiza katika mambo mbali mbali ya kuhatarisha amani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie suala jengine la Vikosi vyetu. Kwanza nivipongeze sana kwa kazi nzuri ambazo wanazozifanya na kutuwekea katika mazingira yetu tukiwa katika hali ya amani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kikosi hicho cha kuzuia magendo, mimi naomba atakapokuja hapa anieleze ni watu wangapi ambao wamekamatwa waliopatikana na makosa ya kufanya magendo katika nchi yetu na hizo kesi zilizokamatwa ni ngapi zimeshughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye Halmashauri au Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa Madiwani waliokuwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" na mpaka sasa kwa mwaka huu nashukuru Mwenyezi Mungu wananchi wangu wa Jimbo la Kiwengwa wameamua kunichagua kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri naifahamu sana na Halmashauri zinafanya kazi kubwa sana, huwa wanasikitika wanapokuja hapa Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anapoulizwa maswali ya kuhusu barabara za ndani anazitupia Halmashauri. Ukitizama Halmashauri barabara ziko nyingi, na Halmashauri hizi zinakuwa hazina pesa za kujenga hizi barabara ambazo zipo katika maeneo yao ya wilaya, na kwa kuwa Halmashauri zinajiendesha wenyewe kupitia michango au ada za leseni, ada za majengo na mambo mengine.

Serikali yetu kupitia ukusanyaji wa mapato kuna mgongano wa ukusanyaji wa mapato, Halmashauri wanakwenda humo humo serikali yenyewe husika inakwenda humo humo hatuoni kwamba Halmashauri tunazibebesha mzigo mkubwa. Namuomba Mhe. Waziri alitizame suala hili kwa kina ili Halmashauri zetu ziweze kujiendesha vizuri na kuleta maendeleo katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala jengine la muundo huu mpya wa serikali za mitaa. Hadi sasa tuliambiwa kwamba kuna sheria mpya ambayo inazungumzia muundo wa Serikali za Mitaa. Kutakuwa na Mabaraza ya Shehia, Mabaraza ya Wadi pamoja na baraza lenyewe la Wilaya. Mpaka sasa hakuna suala lolote linaloendelea kupitia mabaraza na Halmashauri kwa jumla.

Kwani kama wenzangu walivyotangulia kusema mwazo kwamba tumewawekea mzigo mkubwa Halmashauri mpaka sasa Madiwani wetu, hawana posho, wanashindwa kufanya kazi, lakini wananchi wanasema

tumewachagua nyinyi pamoja na Wawakilishi pamoja na Wabunge wetu. Je, Mhe. Waziri ni lini watu wetu hawa wataweza kufanya kazi kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye hatima ya Madiwani. Naomba nimuombe Mhe. Waziri Madiwani nao wana kazi kubwa sana za kuendesha shughuli nzima za wananchi katika Wadi zao na wao baadae kuteletea sisi Wawakilishi na Wabunge pamoja na Halmashauri yenyewe kwa jumla. Lakini Madiwani hawa wanapomaliza muda wao wanashindwa kitu cha kujiendesha katika shughuli zao za maisha wakirudi kumaliza kazi hizi za udiwani.

Mhe. Waziri nakuomba sana wizara yako ilitizame kwa kina suala hili la hatima za Madiwani. Kwani Madiwani wana kazi kubwa sana na wao ndio muda wote wapo na wananchi wetu. Ile miradi ambayo ya maendeleo kupitia Halmashuri fedha zile ni kidogo. Kwa hiyo, naomba sana watizamwe Madiwani hawa kwa kina, lakini pia wathaminiwe.

Madiwani wetu wa Zanzibar tafauti na Madiwani wa Bara, Diwani akitoka hapa Zanzibar anavuka tu pale anafika akifika Dar es Salam akisema mimi Diwani basi haaminiwi kuwa Diwani. Kwa hiyo, naomba sana Halmashuri pamoja na Wizara yako Mhe. Waziri basi muwape mafunzo na muwathamini kwamba hawa nao ni viongozi wa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine la ukataji wa mipaka. Suala hili limeathiri katika Wilaya yetu ya Kaskazini "B", kila Wilaya kuna skuli zile za Sekondari zimejengwa. Lakini ukataji wa mipaka huu katika skuli yetu ya Wilaya ilikuwepo Donge Muwanda, katika ukataji wa mipaka Mhe. Waziri Skuli ile iko katika Jimbo la Tumbatu Wilaya ya Kaskazini "A". Kwa hiyo, kwa sasa Wilaya ya Kaskazini "A" ina skuli mbili ambazo hizo za Sekondari zilizojengwa. Mhe. Waziri naomba ulitizame sana suala hili kwa sababu ndani ya Wilaya yetu hakuna skuli ya sekondari kwa sasa.

Mhe. Waziri kuna suala jengine hili la ukosefu au upatikanaji wa hati miliki za Halmashauri. Maeneo mengi ya Halmashauri wanapokwenda kuomba hatimiliki za maeneo yao basi inakuwa ni vigumu kupatikana. Mimi mwenyewe nikiwa shahidi wakati Diwani wa Wilaya ya Kaskazini "B" kuna maeneo yameombwa hatimiliki mpaka sasa hawajapata hati hizo. Nakuomba Mhe. Waziri uwasimamie na zile Halmashauri zote ambazo wanahitaji hati miliki ya maeneo yao waweze kupatiwa.

Mhe. Waziri na mimi niseme kwamba niungane na wenzangu katika kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye kipengele hichi cha Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM. Mhe. Mwenyekiti, kikosi hichi kinafanya kazi kubwa ya kuweza kulinda bahari zetu ambazo tunazo katika sehemu zetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba kwa ajili ya Kikosi hichi cha KMKM hasa katika Jimbo langu la Gando, kikosi hichi tunaiomba wizara iwajengee Hospitali ambayo itapata kuwasaidia wanapopatwa na matatizo yao. Vile vile wizara hii iwapatie gari ambayo inaweza kuwasaidia katika shughuli zao ambazo wanazitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kipengele cha suala la Madiwani. Na mimi nieleze suala hili kwa ajili kwenye jimbo langu ninao Madiwani ambao wanalalamika wanataka wajijue kwamba mpaka sasa wanawekwa na serikali yao katika kipengele gani. Hivyo, naiomba wizara hii, Madiwani wetu iwaangalie kwa jicho la kina, kwa sababu sasa hivi wanalalamika kwamba Wawakilishi wao sehemu wameshapata lakini wao hawajawekewa sehemu yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, niende kuhusu suala la barabara za ndani. Kwa kweli katika jimbo langu zimo barabara za ndani ambazo hata vifusi hamna, barabara hizi ni mbaya sana. Naiomba serikali katika Jimbo langu la Gando lizione barabara za ndani ambazo zimo katika jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala la kuwekewa *CCTV Camera* katika kisiwa chetu cha Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba wizara hii kuliangalia sana suala hili la kuwekewa *CCTV Camera*, kwa sababu kisiwa chetu kinaingia watu wahalifu, wanaingia wageni ambao wanatokea Somalia huko wanaingia katika kisiwa chetu cha Pemba.

Tunaiomba sana serikali iangalie suala hili la kuwekewa *CCTV Camera*, ili chombo hichi kiweze kutusaidia kwa ajili ya usalama wetu na usalama wa nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kuchangia ila ni hayo. Hivyo ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Maryam kwa mchango wako. Mhe. Abdalla Maulid Diwani jitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Awali ya yote ninapenda kumpongeza sana Mhe.Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba uliojaa mambwembwe, madaha na mambo mengi mazuri yalikuwemo kwenye kitabu hiki. Ninamwambia Mheshimiwa hongera sana. Vile vile ninawapongeza watendaji wake kwa kutuletea bajeti hii ambayo ni mtazamo mzima wa nchi yetu.

Bila ya kupoteza muda ni-*declare interest.* Mimi ninasimama hapa baada ya nafasi yangu ya Uwakilishi ni Mwenyekiti wa *Group* ya *G-One*, hapo ndiyo kwanza ambapo jana tu tulifanya usafi katika mji wetu wa Zanzibar na kuonesha mfano kwamba wengine tutashindana nao. Ninapenda kuwapongeza wale walioshiriki katika usafi kupitia Mkuu Mkoa wa Mjini/Magharibi, Mkuu wa Wilaya, Mstahiki Meya na wengine. (*Makofi*)

Nafasi ya pekee ninapenda sana kumpongeza Mkurugenzi wa Manispaa Bwana Aboud Hassan Serenge. Kwa kweli siwezi kumwita jembe, kwa sababu jembe lina matatizo yake mpaka liwekwe vitu nyuma ndiyo lifanye kazi. Ninapenda kumwita kama ni *bulldozzer*, kwa sababu tulishirikiana naye kwa hali na mali kuhakikisha kwamba lile lengo letu linafikiwa. Ni kweli ni mchapa kazi ambaye asiyechoka. Ninashukuru sana Mhe. Serenge aongeze bidii ili kuhakikisha mji wetu wa Zanzibar unakuwa na safi na sehemu nyengine. *(Makofi)*

Vile vile nikitoka hapo kwenye Manispaa Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia suala zima la Mhe. Meya wetu jamani. Tunajua Meya ni msimamizi wa Baraza wa Manispaa kwa Madiwani. Hajawezeshwa, ile gari aliyokuwa nayo hivi Mhe.Mwenyekiti, haifai. Gari ya Meya imeshachoka. Ni ya muda mrefu. Mimi ninakumbuka ile gari ni zaidi ya miaka kumi hivi sasa. Sasa ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amuangalie basi na yeye ajisikie kwa sababu Meya ni mtu mmoja muhimu sana na hususan huko tunakokwenda sasa hivi katika kumfanya Meya wa Jiji la Zanzibar. Kwa hivyo inshaallah tujitahidi sana tumuwezeshe na yeye ajisikie, kwamba na yeye akisimama na watu wenye gari za uongozi na yumo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza bajeti yako kwa kuniona Mhe. Waziri Jimbo la Jang'ombe kupitia barabara yangu ya Kidongo Chekundu. Ninakupongeza sana Mhe. Waziri lakini nikitaka kujua zaidi je, hii ni barabara ya Kidongo Chekundu mpaka wapi. Kwa sababu sijajua inapoanzia wala inapomalizia. Hivyo Mhe.Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri naomba anifahamishe ili watu wangu kule waone kwamba wanafanyiwa kazi ipasavyo.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia juu ya kadhia iliyotukuta katika Wilaya yetu ya Mjini juu ya nafasi za JKT. Nafasi hizi Mhe. Mwenyekiti, imekuwa jipu kwa Wilaya ya Mjini na kwa taarifa zilikuja nafasi zaidi ya mia tatu kwa Zanzibar, lakini mgawanyo wake kama sisi ni viongozi wa wananchi wa majimbo hatuzijui zilipoanzia wala zilipomalizia. Hivyo naomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri atueleze japo kidogo zile nafasi zimekuwa vipi na kwa Wilaya ya Mjini zimekuja ngapi na zimetumika vipi. Kwa sababu imekuwa tatizo kubwa sana kwa watu kutuuliza kila *time.*

Nikiendelea mbele nitazungumzia suala zima la Kikosi cha Kuzuia Magendo. Hapa nina kumbukumbu ya barua ambayo nitaomba niiosome Mhe. Mwenyekiti, ambayo inasema KM/HQ/SP/31/09. Hii ni kuachishwa kazi kwa askari mwenye namba K/11/22/C 1.

Masikitiko ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, huyu ni mtumishi aliyefanya katika Kikosi cha Kuzuia Magendo kwa miaka ishirini. Lakini cha kusikitisha ni kwamba baada ya kuachishwa kazi, kumeletwa mkataba yule mtu hakukuwa na njia yoyote ya kupatiwa pencheni yake ya kila mwezi. Sijui kuna utaratibu gani kwamba askari anayefanya kazi zaidi ya miaka ishirini anapomaliza mkataba wake anakuwa hayumo katika kiinua mgongo. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba atakapokuja anieleze.

Si hivyo tu hata kuna malalamiko kwa baadhi ya askari wanaokwenda mafunzo kule, wanalipishwa elfu sabini za magodoro. Lakini cha kushangaza baada ya kumaliza mafunzo yale mbona yale magodoro hawapewi wenyewe na tayari wameshayalipia au yameshakatwa. Ninafikiri kule KMKM inaongoza kwa kuwa na magodoro mengi sasa hivi. Kwa sababu kila kozi inayokwenda wale askari wanakatwa kiasi cha shilingi elfu sabini kwa ajili ya magodoro. Sasa sijui utaratibu huu. Itabidi kupitia serikali nitaomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie vile vile.

Mengine mengi ambayo ninataka kuzungumza yameshazungumzwa na wenzangu, lakini pamoja na hayo, bado nitabakia pale pale juu ya suala zima la

CCTV camera. Kwa kweli hii *CCTV camera* zinatupa mashaka juu ya utekelezaji wake, toka muundo wake ilipoanza tenda mpaka ikafikia hapo ilipo.

Katika kitabu kikuu cha serikali imepigwa bajeti bilioni kumi na nane, lakini ulivyotusomea Mhe. Waziri juzi ni bilioni kumi na tano, umeshapewa milioni mia nne na kumi na mbili ninafikiria. Sasa hizi kidogo ninataka ufafanuzi wa kina ili tujiridhishe kwa sababu kuna mambo mbali mbali. Kweli hizi *camera* zimefungwa kwa nia safi kabisa kuisaidia Zanzibar katika masuala ya ulinzi. Lakini malalamiko mengi hata na miundo mbinu ya taa za barabara ambapo tumepata msaada kutoka *World Bank* ninafikiri. Zile taa kusema kweli zinanisikitisha. Zinafanya kazi muda mdogo sana, si zaidi ya miezi mitatu zile taa ndiyo zimesimama. Sasa hivi eneo kubwa ukitembea kwenye mji wa Zanzibar zile taa haziwaki. Sasa sijui kuna tatizo gani kwamba hata na hawa wawekaji walishinda shinda vipi *tender* ya kuweka zile taa na pengine walikuwa na mkataba kiasi gani au *guarantee* kwamba hizi taa ziwake zaidi ya miaka mitatu au miaka miwili. Tujue kwamba kama kuna tatizo lolote lililotokezea basi hawa wawekaji wa hizi taa wamefikia hatua gani.

Kwa sababu malalamiko yamekuwa mengi na inaonekana kama rasilimali za serikali zinapotea bure ambapo zile taa pesa nyingi zimetumika. Lakini matumizi yake yamechukua muda mdogo sana. Kwa hivyo ni masikitiko ijapokuwa na wenzangu wengine wameshalizungumzia hilo.

Jengine ninalozungumzia ni suala zima la kuapishwa Madiwani wetu, imekuwa kero. Hata mimi jimboni kwangu Madiwani wangu na wamenituma hasa nije kuwasemea, nimuulize Mhe. Waziri, ni lini Madiwani watamaliza matatizo yao ili wao na waanze kazi. Kwa hivyo na mimi ninapenda kuwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi ijapokuwa na Wawakilishi wenzangu wameshalizungumza hilo. Naomba jibu *atleast* wasikie na wao wenyewe waone kwamba kile walichonituma nimekifanyia kazi.

Mwenyekiti, ninapenda kurudi nyuma kwamba tumefanya usafi kwenye Mji Mkongwe, lazima sisi miongoni mwetu sote tuwe wachukia uchafu. Ninafikiri serikali kupitia Manispaa iwe kali kidogo. Iweke faini za papo kwa papo. Ijapokuwa nimeweza kutoa shukurani kwa Mhe. Mkuu aliyezungumza pale jana, lakini uwepo utaratibu *atleast* watu wote wanaochafua mji kwa makusudi basi wawe wanapigwa faini papo kwa papo, kukomesha kadhia ile.

Kama unavyofahamu Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mji Mkongwe ni kitovu cha biashara kwa Zanzibar na kivutio cha wageni kutoka sehemu mbali mbali, wanapokuja hapa *atleast* waondoke na sifa ya usafi katika mji wetu, kwenda

kuwashawishi wengine ili na wao wawe na hamu ya kuja kuitembelea Zanzibar.

Ninafikiri Mhe.Mwenyekiti, mimi mengi ambayo niliyotaka kuyazungumza, wenzangu wameshazungumza, haina haja ya kuyarejea. Mengine nimeshamuandikia Mhe. Waziri ili kwa kuokoa muda, ninafikiri nimezungumza hayo machache na ninasubiri maelezo mengine ya Mhe. Waziri zaidi. Itakapokuwa maelezo mazuri basi mimi sina matatizo, nitaunga mkono hoja. Lakini kama sikupata majibu ya kuridhisha basi nitakuwa na nguvu ya kumuuliza mpaka aniridhishe na majibu yangu, basi nitaunga hoja kwa wakati huo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Diwani. Sasa anayefuata Khadija Omar Kibano. Na baadae atafutia Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nikapata kuchangia kidogo katika Jimbo langu Mtambwe.

Katika Jimbo langu la Mtambwe, kwanza nipo katika Kikosi Maalum cha KMKM kwa upande wa rada. Rada hii iliyokuwepo pale kwenye Kituo cha KMKM Mtambwe upande wa Sengenya. Rada hii zamani ilikuwa ikifanya kazi zake kwa ukamilifu. Lakini hivi sasa haifanyi kazi kama inavyopaswa.

Ninachomuomba Mhe. Waziri. ashirikiane na serikali ili rada hii ifanye kazi askari hawa wafanye kazi zao kwa ufanisi. Kwa sababu hivi sasa kinachopita kwenye bahari hakionekani. Zamani kilikuwa kikipita katika bahari tayari chombo kinakuja kama kuna mambo yaliyokuwa hayastahiki ile rada inakuwa inazungumza. Lakini sasa hivi chombo hiki hakifanyi kazi. Hivyo ninamuomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anisaidie hili suala.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye suala la upande wa barabara. Barabara katika Jimbo langu la Mtambwe; nina barabara zangu za ndani tayari zimekuwa na usumbufu wa usafirishaji wa bidhaa pamoja na usafirishaji wa watoto wanapokwenda skuli. Barabara hizo zilikuwa katika kipindi cha mvua zina tope nyingi, wanafunzi wanakuwa wanateseka sana kwenda katika eneo la skuli kusoma.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri anisaidie katika suala langu hili la barabara za ndani na barabara hizi naomba Mhe. Mwenyekiti, nizitaje kama zifuatazo; Kwanza ni kutoka barabara ya Miembemizizi Chanjaani, Mpaka Njia Kia Paka, Kia Paka Kirumbe, Uwondwe Nyali mpaka Kilingoni, Uwondwe Kele na Uwondwe Jambaji.

Barabara hizi zinakuwa zina usumbufu mkubwa kwa wanafunzi zaidi kwa sababu sasa hivi wanafunzi ikifika kipindi cha mvua zaidi wanakuwa wanapata dhiki kwa kwenda kusoma. Hawapati elimu yao msingi. Wanafunzi hawa wakati huo ikifika inakuwa wao wako katika hali ya kuroa maji, matope mengi, fomu zinaharibika, mabuku yananyambuka, wakifika skuli wanakuwa hawapati kukaa kitako vizuri. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hili suala alifanyie kwa uangalifu inavyopasvyo.

Naomba niende sehemu yangu ya Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo. Ofisi hii kuna suala la mambo ya ndoa, talaka pamoja na vifo vyenyewe na vizazi. Mhe. Mwenyekiti, takwimu hizi nimezipata katika kitabu hiki cha bajeti. Ni kuwa takwimu hizi hazipo sahihi.

Kwanza kwa suala la ndoa. Suala la ndoa kabisa wameweka wenyewe wao hapa, katika hili kuna ndoa mia moja na ishirini na tano, ni ndoa zilizokuwa zimepitishwa kwa kusajiliwa kwa ukamilifu. Kuna ndoa nyingi sana zinapitishwa hasa ndoa za mkeka. Hizi ni ndoa zilizokuwa hazisajiliwi kwa ukamilifu, kwa sababu ndoa zinapitishwa kienyeji enyeji sio kirasmi. Kwa hivyo naomba hapa kwanza ipatikane elimu kwa wananchi na jamii ili wafahamu. Ndoa yoyote itakayoitishwa kwa Sheria ya Mwenyezi Mungu kama ndoa ile ipo sahihi ipitishwe kwa Mrajis Mkuu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la talaka. Talaka zipo nyingi sana na hizo haziripotiwi kwa ukamilifu. Kwa sababu sisi wasimamizi wa wanawake na watoto.

Talaka hizi kwa kipindi hiki cha uchaguzi tu, nikikuhesabia kuna talaka zisizopungua mia tano mpaka laki. Watu wengi wamekosa haki zao za msingi kwa kipindi hiki cha uchaguzi hawathamini kazi. Talaka hizi kumi na sita zilizoandikwa katika bajeti hii. Mimi naona ni talaka zilizopitishwa kwa Mrajisi mwenyewe na kuna talaka zile zilizoamuliwa na Kadhi mwenyewe. Lakini siyo talaka sahihi zilizo pale.(*Makofi*)

Kwa hivyo ninaunga mkono hotuba hii asilimia mia. Kwa leo sina mengi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwanza kwa kuokoa muda ili wenzio na wao wapate wachangie. Mhe. Ame Haji Ali na Mhe. Mussa Foum Mussa ajitayarishe.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha asubuhi hii kupata nafasi hii kwa nia ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kwa leo. Lakini moja kwa moja nianze na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa maamuzi yake sahihi ya kutuwekea kituo hiki katika Jimbo langu. Ninaishukuru sana lakini kwa mawazo yangu na maoni yangu, kwa kuwa eneo letu linapanuka kila siku, basi kituo kile kimefika wakati kiongezewe vifaa ili kiweze kutuhudumia vizuri katika eneo ambalo ni kubwa na lina raslimali nyingi za kitalii.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka nilizungumze kwa haraka haraka ni eneo la Kituo cha KMKM Kibwengo. Hiki kituo Mhe.Mwenyekiti, kipo Kibwengo lakini kile kituo Mhe. Waziri ninakuomba sana ukiangalie sana, kwa sababu kile kituo kipo lakini kimekosa huduma kama kituo. Kile kituo hakina maji, hakina umeme. Hata lile jengo wanalokaa wale watu kama walinzi wetu haliridhishi hata kidogo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba sana aliangalie sana jambo hili ili kituo nacho kiweze kutizamwa kwa jicho la huruma.

Eneo la tatu ambalo mimi nilitaka leo nilichangie Mhe. Mwenyekiti, ni eneo la Halmashauri. Kwa zaidi kwa leo ninakwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya "A". Kwanza ninawapongeza, wamejipangia kukusanya milioni mia tano na hamsini. Ni pesa nyingi lakini Mhe.Mwenyekiti, Mhe. Waziri utakapokuja mimi naomba tu nipate ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo, kwa sababu mimi ni mgeni katika shughuli hizi.

Maana kati ya pesa hizi wamesema shilingi milioni mia tatu na thalathini na tano zitatumika kwa miradi ya maendeleo. Sasa mimi nilikuwa na maswali katika eneo hili. Je, hii miradi ya maendeleo sisi kama Wawakilishi tunashirikishwaje. Hili suala langu la kwanza.

Lakini suala langu la pili au kama sisi Wawakilishi katika miradi hii tunaweza tukaibua yepi na tukawapelekea au wanaibua wenyewe, halafu wanasaidia moja kwa moja.

Suala langu la tatu ni vigezo gani Halmashauri zinatumia katika kutumia hizi pesa za hii miradi ya maendeleo. Mimi nilikuwa naomba haya nipate ufafanuzi kwa sababu ni vyema, Wawakilishi wa wananchi tukajua kwamba kama kuna mifuko hii ya maendeleo inatumika basi na sisi tuna nafasi gani katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, eneo ambalo zaidi limenifanya leo nisimame katika kuchangia hotuba hii ni eneo la Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kilichopo Nungwi. Hiki kituo kipo Nungwi Mnarani. Mhe.Mwenyekiti, kile kituo kizuri mno na lazima niipongeze serikali kwamba kile kituo ni kizuri. Lakini leo nilikuwa ninatafuta nafasi hii ambayo nitakuwa karibu na serikali moja kwa moja kuzungumzia baadhi ya mambo ya kile kituo.

Mhe.Mwenyekiti, tukubaliane kwamba eneo peke yake ambalo lenye bahari kali katika visiwa vya Unguja na Pemba ni eneo langu la mkondo wa Nungwi. Na ni kweli kwamba ajali zote zinazotokea mwanzo wake zinaanzia pale. Sasa kama ajali zote zinaanzia pale Mhe.Mwenyekiti, kama serikali tunahitaji tuwe na juhudi maalum katika kuzikabili. (*Makofi*)

Sasa mimi wazo langu. Kile kituo kwa sababu kina wapiganaji wetu. Ningeiiomba sana serikali itenge kwa makusudi kabisa na kwa jitihada kabisa wawapatie boti moja kubwa sana ambalo litatumika pale kwa kazi ya uokozi.

Mhe. Mwenyekiti, nimejifunza katika ajali zilizotokea, miongoni mwa mambo ambayo yalikuwa yanatupelekea kupoteza watu ni kwamba hatuna matayarisho ya kutosha katika kuwaokoa. Sasa tunachotegemea ni kwamba taarifa hizi zikishapatikana za tatizo ndiyo tuanze kuzishughulikia na wananchi walio karibu pale waende katika uokozi.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, ninahisi si jambo sahihi. Naiomba sana serikali tutafute boti moja kubwa pale, liwepo pale kituoni na liwezeshwe kupatikana vifaa ili itakapotokea tatizo, basi wao wawe ni watu wa mwanzo kufika, halafu na wananchi wengine basi watashiriki katika kuhakikisha kwamba wanashirikiana na vikosi hivi. Tukifanya jambo hili tutakuwa tumesaidia sana wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, tusichukulie tu kwamba labda hizi ajali zinatokea kwa vyombo vikubwa tu, hapana. Ajali nyingi zinatokea hasa kwa vyombo vidogo. Pale kwa sababu kazi yetu kubwa ni uvuvi, kuna mitumbwi na vyombo vyengine hivi vyote vinaenda baharini. Basi mara nyingi hupata matatizo lakini ninahisi kwamba kama tutakuwa na chombo kile ambacho kipo pale, kilicho tayari basi kitasaidia sana kunusuru maisha ya watu na mali zao.

Kwa hivyo, mimi naiomba tu serikali ilione hili na ilichukulie hatua. Lakini si tu katika njia hiyo, hawa ni watu ambao tumewapa kazi ya bahari na mali zetu na kuzuia magendo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunaposema kwamba wanalinda na kuzuwia bahari wao hawana hata mtumbwi, hiyo bahari vinavyotokea kule wanavikabili vipi. Mimi naiomba sana serikali ilione jambo hili kwa maslahi ya Wazanzibari sote na watumiaji wa bahari. Maana mimi kule kwangu ndiko wanakopitia wote. Wapemba lazima wapite pale, Watanga na Wadarisalamu. Sasa tukifanya hivi tutakuwa tumewasaidia watu waliowengi katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mimi leo hii ni siku yangu ya kwanza kusimama katika Baraza hili kuchangia, basi naomba nitumie muda wangu huu kutoa shukrani kwa baadhi ya watu ambao nimewahisi leo nitumie nafasi hii kuwashukuru.

Mhe. Mwenyekiti, wa kwanza ambao nataka niwashukuru ni viongozi wangu wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Wilaya zake zote mbili, kwa kufanikisha kwa kiasi kikubwa katika zoezi la uchaguzi na kutufanya sisi leo tusimame katika chombo hiki.

Shukrani zangu za pili nataka niwashukuru viongozi wangu wote wa Jimbo, pamoja na kamati zao zote, kwa kweli wamefanyakazi kubwa katika kuhakikisha kwamba uchaguzi unakwenda vizuri na sisi leo tunasimama katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, wa tatu nataka nizishukuru kamati zangu zote ambazo zilinishauri na zilishirikiana na mimi vyema sana katika kuhakikisha kwamba ushindi huu unapatikana. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, wengine ninaotaka kuwashukuru leo ni familia yangu, nianze na mama yangu mpendwa ambaye kwa wakati wote amekua akinishauri na wakati wote amekua akiniombea dua kila asubuhi ninaponyanyuka kuja kwenye Baraza hili, namshukuru sana mama yangu. *(Makofi)*

Pia niwashukuru na watoto wangu wote, niwashukuru na wale wote ambao nilikuwa nao kwa usiku na mchana katika kazi hii kubwa na ngumu. Lakini kipekee niwashukuru wake zangu. Wake zangu wote wawili Fatma na Fatma, hawa ni kiyoo changu Mhe. Mwenyekiti, wamenisaidia sana katika kufanikisha kazi hii na kwa kweli hadi sasa ili kuweza kufanikisha majukumu haya vizuri na kuwa mtulivu katika chombo hiki, kwa kweli msaada mkubwa wananipa wake zangu, nawashukuru sana na waendelee na kazi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nawashukuru zaidi pale ambapo wananistahamilia. Unajua wakati mwengine hapa tunafika mpaka saa 5:00 au saa 6:00, lakini wanastahamili kuona kwamba kumbe kweli niko katika utumishi na wao wako vizuri kunisubiri ili kuona nimerudi hapa salama nikaungane nao.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho katika mchango wangu leo nitoe wito kwa wanajimbo wote wa Jimbo la Nungwi. Nawaomba watambue kwamba uchaguzi sasa umekwisha, na mwakilishi halali wa Jimbo la Nungwi kwa mujibu wa ibara zote za katiba na sheria ni Ame Haji Ali. Hakutakuwa na mwakilishi mwengine mpaka muda kama Mwenyezi Mungu atanihitaji au mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nawaomba waache waliyonayo ili tushirikiane katika kutatua changamoto ambazo mimi naamini ni nyingi sana katika jimbo hili, lakini wakinipa ushirikiano wa kutosha naamini tutaweza kufanya kazi hiyo vizuri na tutalipeleka jimbo hili mahali ambapo tunapategemea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu leo hii ni siku yangu ya kwanza na hata hivyo leo sikuamka vizuri kiafya, naomba basi mimi huu uwe ndio mchango wangu. Mwisho niseme tu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wana jimbo la Nungwi, tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ame Haji Ali. Samahani Mhe. Mussa Foum nilikutaja, lakini nilikuwa naziba kiporo kidogo hapa cha Mhe. Ame Haji Ali katika orodha kuu. Kwa hivyo, ataendelea Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kuchukua nafasi hii. Karibu Mhe. Dimwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana kwa kunipa imani hii. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake bora, lakini nimpongeze sana Katibu Mkuu na timu yake yote waliyotayarisha bajeti hii, bila wao Mhe. Waziri asingefanya kazi hii imara sana.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais. Nataka niseme tu imani yetu kubwa kwao na wao ni wafanyakazi wazuri na hatuna wasi wasi na uteuzi wao, tumpongeze Mhe. Rais sana kwa hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Manispaa yetu ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya wenzangu walisema wanataka kuona *public toilet* au vyoo vya serikali. Nimeangalia vingi na nimeona bado vipo, lakini Mhe. Waziri atakapokuja hapa atutajie vimebaki vingapi, kwa sababu katika utafiti wangu nimeona vingine vimetengenezwa vyoo sijui vya watalii, vyengine vimetengenezwa ofisi.

Kwa hivyo, tunapenda kujua ni sababu gani zilizofanya vile, lakini na vyengine vimebaki vingapi katika mji huu, kwa sababu mji huu tumekabiliwa sasa na watalii wengi, lakini tukiangalia vile vile kipindupindu kilituathiri kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, pale kwenye jimbo langu kuna mambo mawili; moja kuna bustani ya *botanic* tulikuwa tunaiita *prince* au *president*, shamba lile la Rais wa zamani sana. Rais wa mwanzo aliweka shamba katika eneo la Migombani. Lakini nataka kusema kwamba nimpongeze sana Mkurugenzi wa Manispaa kwa hatua kubwa aliyoichukua, lakini bado nataka kujua kwenye shamba lile limegeuka chaka la wahalifu usiku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilete ombi, Mhe. Waziri naleta ombi kwamba wale vijana wetu, kama shamba hili bado halijataka kutumiwa, vijana wetu wanaofanya bustani wanaopanda ile miche basi waweze kuhamia pale, lakini hata na wale polisi jamii wetu au askari shirikishi waweze kulinda gari eneo lile kwa sababu halina eneo la kutosha. Nimesema kuna chaka la wizi au vibaka, wananchi wengi sana wanapata usumbufu nyakati za usiku hasa akina mama, kukamatwa, kubakwa na vitu vingine vyote vinavyohusiana na hivi. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja na mimi nampa hayo mapendekezo ambayo ya kuona hali halisi ya pahala pale tunaishi kwa usalama zaidi.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye hizi *parking* zetu, ningependa kujua hasa katika eneo lile la Malindi *parking* ile nani ambaye anashughulika nayo. Pana ulinzi shirikishi pale, lakini hatujui kwenye mji huu tuna-*park* wapi na tunakaa wapi, wewe utakapokaa tu umekumbana na lile chuma, hata ukiwemo ndani ya gari hujulikani una-*park*, au hujulikani umesimama mara moja. Wewe ukisimama tu unashtukia na ukiangalia macho tu tayari tairi la mbele limetiwa mnyororo. Kwa hivyo, ndio tunataka kujua ni

kigezo gani ambacho wamepewa pale walinzi shirikishi na wamesomeshwa sheria gani hizi za kuweza kujua hapa *parking* mtu huyu amesimama au vipi. Ninavyojua mimi *parking* ume-*park* na umetoka, lakini hata ukiwa ndani ya gari umekaa muda mdogo sana, basi unaweza ukakumbana nao ule mnyororo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nirudi tena kwenye mradi huu wa *ZUSP*. Mhe. Mwenyekiti, moja katika majimbo yaliyo athirika na mafuriko makubwa ni Jimbo langu la Mpendae, na kwa sababu hiyo basi ningeiomba serikali sana ifanye jitihada ya kumaliza ule msingi. Kuna msingi mara moja niliupigia kelele ambao ulichimbwa na Wizara ya Mawasiliano, kutoka Mchina Mwanzo kuelekea Kwa Binti Amrani; msingi ule sasa umekua unaathiri sana. Nimekua nikiwakimbia hata wananchi wangu wakati wa mvua. Wengine wamebomokewa, wengine vyoo vimekatika kwa sababu haukufika popote na msingi ule unatiririka maji katika nyumba za watu. Mhe. Waziri, ningeomba sana, hili naleta ombi rasmi ili tumalize mambo yale kwa wakati ili wananchi wangu wasipate kadhia hii kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye nyumba za maendeleo Kilimani. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kipindupindu kimetuathiri, lakini nina hofu kubwa sana sasa na majumba yale ya maendeleo ya Kilimani, ukiangalia karo zake ziko chini majumba na maji mengi yanafurika. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri atakapopata muda tuende tufanye ziara ya pamoja, Mstahiki Meya, pamoja na watu wake wa afya tukaone njia gani za kuwasaidia watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Halmashauri ya Magharibi. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Magharibi, lakini nataka nimkumbushe kuwa Mpendae ipo kwenye Manispaa, Mpendae haiko kwenye Halmashauri, Mpendae bado ni mjini, nataka nimkumbushe hilo atakuwa yeye mwenyewe anafahamu, asije akakusanya kodi kule sio zake.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua kwenye kitabu hiki kikubwa kwenye fungu D10 nataka ufafanuzi tu. Nitakwenda haraka haraka ili na wenzangu angalau wawili wapate nafasi. Ukurasa wa D149 na ukurasa wa D151, nimeangalia mikoa mingi, mikoa yote mitatu ya Zanzibar inaleta mapato. Lakini sijaona hata pamoja tangu mwaka jana, mwaka huu na mwaka uliopita Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Kaskazini Pemba kama umechangia, hakuna mapato na wameanza moja kwa moja kwenye matumizi. Sasa nilikua namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa nataka kuona kwenye fungu D10 hili au nataka nimuulize mpaka Wakuu wa Mikoa wameanza kugoma, hawataki kuchangia. Pengine tusione tu wananchi wao ndio wanaoambiwa

wagome, labda mpaka Wakuu wa Mikoa wameanza kugoma. Nataka aje aniambie hili ili niweze kuona mchango wao ni upi katika kuweka mapato haya.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ile pamoja na Mwenyekiti wake kwa jitihada kubwa ambazo wanachukua. Lakini kuna wale waanika madagaa wa Fungu Refu, Mhe. Mwenyekiti, wanapata tabu sana, nilijaribu kwenda mara tatu kuwatembelea, lakini barabara yao chafu sana. Kwa hivyo, ningewaomba tu watayarishe ile barabara angalau kwa kifusi, ili serikali ipate mapato na wao wenyewe wanapata mapato, lakini kusiwe na usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara ya Zimamoto. Kwanza niwape pongezi kubwa sana makamanda hawa wote wa Kikosi hiki cha Zimamoto. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunatumia sana vifaa chakavu, Zimamoto tuwahurumieni vifaa vyao viko chakavu sana, hata tukipata dharura wakati mwengine wanashindwa kufanya kazi ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, hata kwenye ofisi zetu, pengine hata kwenye hili Baraza lako kuna *fire extinguisher*. Lakini maofisi mengine ukiangalia *fire extinguisher* zimepita muda yaani zime- *expire*. Kwa hivyo, natoa ombi rasmi kwa serikali kuweza kuwatumia wataalamu hawa na kuweza kuona.

Mhe. Mwenyekiti, lakini si hilo tu kwa hizi *fire extinguisher*, wafanyakazi wapatiwe mafunzo maalum ya kupigana na moto, *fire fighting*. Kwa sababu wengine pengine wanazo tu na wanaziona, lakini hata matumizi yake hayawezi kujulikana.

Mhe. Mwenyekiti, niseme Zimamoto wanafanyakazi kubwa, lakini niwahurumie sana Zimamoto wa pale Pemba Wete. Wanakaa katika hali ngumu hata majengo hawana, vifaa hawana. Tunataka kamanda wetu mkuu wa vikosi vyote hivi Mhe. Waziri aliangalie kwa huruma sana. Mimi leo nilikuwa nashauri tu ili tuweze kuona jinsi gani hawa wapiganaji wetu wanaishi katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi vyote kamanda wao ndiye mpiganaji wetu mkuu Mhe. Haji Omar Kheir, waziri. Nataka kumwambia vijana wetu hawa angalau serikali iwaone kuwapatia *health insurance*. Wanakaa katika sehemu mbaya na wanafanyakazi kubwa vikosi vyote hivyo na tunaiona kazi yao. Lakini wanaondoka hawana hata *health insurance*, wanaweza kufika nyumbani wao wako kwenye kazi kubwa, pengine pesa hakuna. Kwa hivyo, tujitahidi sana kuwapa angalau *health insurance.*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Fungu D3 Chuo cha Mafunzo. Kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Kamishna na watendaji wake wote. Mhe. Mwenyekiti, nimesoma kwenye fungu hili na bajeti yao, wana bajeti ya shilingi bilioni 7,586,600,000/- hizi ni pesa za mishahara. Pesa za kuweza kujikimu ni shilingi bilioni 1,383,400,000/-. Mimi nasema hizi ni pesa ndogo sana kwa kujikimu, kwa pesa ya matumizi ya kawaida ya jeshi lile ni ndogo mno, serikali ifikirie kama kuna popote iweze kuwasaidia kuweza kuwachangia.

Nataka nimshauri Mhe. Waziri, tuna bonde au bahari kubwa sana katika bahari ya Bumbwini, tunaweza tukafuga samaki wengi mno na hivi vyuo vyote vya mafunzo vikatumia samaki hawa, tusiliache tufanye kazi kwa bidii ni zuri mno na linavutia sana. Mhe. Waziri kama hujenda huko, nenda kaangalie utaona jinsi gani samaki tutakavyofuga kwa wingi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, baada ya hii miembe ya serikali labda au miti mingine ya matunda wasiikodishe Magereza, wawe wanachukua kuweza kuwalisha wafungwa ili zile OC ziweze kutumika kwa mambo mengine, kwa sababu hizi ni pesa ndogo sana, sidhani kama anaweza kuzitumia.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Ofisi ya Usajili wa Vitambulisho. Nataka nimpongeze sana Mkurugenzi na watendaji wake wote, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi huyu alipata hati bora na vitambulisho vyetu vilikua bora katika *East Africa*. Tuchukuwe fursa hii kumpongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya, nasema yale maneno yote anayoyasikia kwa wapinzani au kwa watu wengine asivunjike moyo, afanyekazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili ya Vizazi na Vifo. Nimpongeze Mkurugenzi kwa kazi kubwa anayofanya. Vile vile niwapongeze wafanyakazi wake, kuna vijana pale wanafanyakazi kwa bidii zaidi, wanastahiki sifa na wanafanyakazi imara zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikua nitoe mchango huo mdogo kwa sababu wengi wamezungumza. Kwa hivyo, nasema tu naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 50 na asilimia 50 nataka nizichukuwe mwenyewe mpaka nipate ufafanuzi wa haya mambo ambayo nimeyasema hapa, ili niweze kuunga mkono hotuba hii, nitakuwa sina wasi wasi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa). Sasa anafuata Mhe. Mussa Foum Mussa na kama muda utaruhusu basi Mhe. Yussuf Hassan Iddi ajitayarishe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nikupongeze kwa kunipa fursa hii wakati huu na mimi kupata nafasi kidogo ya kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika mada. Mimi nitaanza kuchangia katika Manispaa ya Zanzibar hasa katika vituo vya daladala zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wananchi wetu juu ya vituo vyetu hivi vya daladala, imekuwa ni kero kubwa na imekuwa ni gumzo kubwa kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, vituo hivi vimewekwa kwa majaribio, lakini muda umekuwa mkubwa sana wa majaribio, sasa tunachokiomba kwamba ni vyema kutafutwa sehemu ambazo zitaepusha zile kero, kwa sababu ukiangalia pale Kisiwandui kiukweli pamekuwa na tatizo kubwa sana, kituo chenyewe kipo kwenye barabara, magari hayawezi kupita vizuri kiukweli inakuwa ni tatizo.

Kwa hivyo tunakuomba Mhe. Waziri kwamba ni vyema tukatafuta sehemu ambazo zitaepusha zile kero ingawaje hiyo sehemu nayo kuipata ni tatizo kutokana na mji wetu ulivyo hivi sasa, lakini ni vyema tukatafuta sehemu ambazo zitasaidia kwa yule mpita njia. Kwa yule ambae hangojei abiria gari ambazo zinakwenda na shughuli zao. Kwa hivyo ni vyema tukakiangalia zaidi kituo kilichopo pale na pale kiukweli pamekuwa na tatizo kubwa hata kwa ile ofisi yetu ya Chama. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba je, bado tutaendelea kubaki pale pale au kuna mpango wa kutafuta sehemu nyengine ili tuondokane na pale.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuzungumza Mabaraza ya Miji, kwanza niyapongeze kwa jitihada zao kubwa na yale malengo ambayo wamejipangia ili kuyatekeleza, zaidi niende katika Baraza la Mji la Mkoani, Baraza la Mji la Chake Chake na Wete. Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba nikumbushe suala hili la vituo vya kuwekea magari kwamba bado miji yetu zaidi ukiangalia Mji wetu wa Mkoani haujakumbwa sana na hizi *stand* za magari, lakini ukiangalia Chake Chake hivi sasa gari zimekuwa nyingi, gari zinawekwa kwenye barabara wakati mwengine kuna usumbufu mkubwa wa kupita. Kwa hivyo nayaomba haya Mabaraza kwa mfano Baraza la Mji la Chake Chake weshaanza

kutengeneza kule Qatar lakini pia watengeneze sehemu nyengine, kwa sababu kila tunakokwenda watu wanaendelea kuleta magari ya binafsi. Kwa hivyo itafika pahala gari katika Mji wa Chake Chake, hazina *parking* kwa sababu mji wa Chake tunajenga vizuri. Watu wameibuka vizuri kujenga. Lakini tunasahau sehemu za kuwekea magari.

Kwa hivyo nayaomba Mabaraza haya na vile vile Baraza la Mji la Mkoani nalo litafute mapema sehemu za *parking*, kwa sababu wananchi wetu wameibuka na ari ya kununua gari ya kutembelea lakini anapofika mjini hajui aiweke wapi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote kwa kuchaguliwa kwao, wale watakaokuwa wanaendelea na wale wapya, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, pia vile vile niendelee kuwapongeza zaidi Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wa Pemba. Mhe. Mwenyekiti, sote tunakumbuka au tunafahamu katika kipindi kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi mpaka hivi sas kiukweli tumekuwa na matatizo makubwa ya kisiasa Pemba, lakini kwa ujasiri wao mkubwa Wakuu wetu wa Mikoa na Wilaya wamekuwa wakichukua jitihada kubwa sana za kuweka hali ya utulivu katika kisiwa chetu cha Pemba na tunamshukuru Mwenyezi Mungu, mpaka hivi sasa hali si nzuri vizuri, lakini ni kwamba mpaka hii leo tunajivunia kwamba kisiwa chetu kiko salama. Hakuna mtu aliyepoteza maisha kwa masuala haya lakini tuendelee na mashirikiano na wakuu wetu hawa pale panapotokea jambo tuwe tunashirikiana ili tuone kwamba Kisiwa chetu cha Pemba nacho kinapata utulivu ulio mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na vifo; wenzangu wengi wameelezea juu ya suala hili, ambalo limekuwa gumzo kubwa kwa wananchi wetu imekuwa ni tatizo kwa muda mrefu sana miaka mingi sana, vyeti vimekuwa ni tatizo upatikanaji wake, vijana wetu wanafika umri wa kwenda skuli wengine hata wa kuolewa bado mtu hajakipata cheti. Imekuwa ni tatizo kwa wananchi wetu kufuata kwenye Wilaya zetu, kwa sababu kubwa ukifika utambiwa magamba hamna. Sasa mimi nielezwe tu Mhe. Waziri ameeleza kwamba kuanzia kipindi kilichopita na hiki kijacho mambo haya yatakuwa yamewekwa vizuri na itakuwa upatikanaji wake utakwenda vizuri. Kwanza nimpongeze kwa hatua yake hiyo nzuri na niseme kwamba tumshukuru Mwenyezi Mungu atujaalie kwamba suala hili liende vizuri ili hili tatizo la upatikanaji wa vyeti lipungue, ili wananchi wetu na wao waondokane na tatizo la kufuata vyeti kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo niende vilevile katika Idara zetu maalum za SMZ; kiukweli tuwapongeze vikosi vyetu vyote vya SMZ kwa

jitihada zao kubwa wanazochukua kwa kuilinda nchi yetu ya Zanzibar, kwa sababu ingalikuwa vikosi hivi havipo basi kiukweli hii leo tungekuwa tunazungumza mengine. Kwa hivyo ni vyema tukavipongeza. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kiukweli vikosi vyetu baadhi yao vimo katika matatizo, kwa mfano nizungumze katika jimbo langu, mimi ninacho kikosi cha JKU pale Mwambe lakini kiukweli pale hapapo katika hali nzuri, ukiangalia umeme hapana, maji hapana vizuri. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Waziri hiki kikosi ukitupie macho ili tuone na wao wanajisikia vizuri katika kituo chetu kile kilichopo pale Mwambe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi naomba nifikie hapo kwa sababu dakika zilizobaki angalau apate na mwenzangu mmoja na yeye achangiye kwa sababu tuko wengi. Kwa hivyo mimi sina mengi isipokuwa naiunga mkono hotuba hii, atakapokuja tu Mhe. Waziri atueleze zaidi katika suala la vituo vya daladala katika Mji wetu huu wa Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo nasema naiunga mkono mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipa fursa hii japo ya dakika kumi na kuweza kuchangia. Kwanza kabisa nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri, namna alivyowasilisha, niwapongeze watendaji wa Wizara hii kwa kumsaidia vizuri Mhe. Waziri, kwa vile muda ni mdogo sana mimi nitakwenda kwa kasi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Mhe. Waziri alitangaza Shehia mpya na katika Jimbo langu la Fuoni bahati mbaya zote ni shehiya mpya na Shehia hizi hadi leo hazina masheha. Je, ni lini Mhe. Waziri atatangaza Masheha kwa zile Shehia mpaya zikiwemo shehia za Jimbo langu la Fuoni, lakini vile vile kuna kilio kikubwa cha Waheshimiwa Masheha hawa wa sasa wana hamu kubwa ya kuonana na Mhe. Rais, kama Mhe. Rais anavyonana na makundi mbali mbali katika nchi yetu. Kwa hivyo hili wazo nimepewa na masheha, kwa hivyo nakuletea kwako Mhe. Waziri ili ujumbe huu uufikishe kwa Mheshimiwa ili na wao wapate fursa Masheha hawa wa kuonana na Mhe. Rais.

Vile vile nije kwa upande wa Vikosi vya SMZ, mwaka jana vile vile mwanzo Wizara ilitagaza nafasi mbali mbali katika Vikosi vyetu vya SMZ na kuna vijana wengi walioshiriki, muda ulikuwa umemaliza wakaongeza tena siku zile za kwenda kujisajili katika Wilaya zetu, lakini mpaka leo Mhe. Waziri tunaona kimya, vijana wako kimya na hata sisi wazee tunaona kimya. Kwa hivyo tunaomba Wizara itupe ufafanuzi nini kimetokezea hadi mpaka leo ikawa kimya.

Vile vile niende kwenye kitabu kikubwa hiki fungu B02 JKU baraza lililopita lilipitisha Sheria ya kuanzishwa Shirika la ulinzi la JKU, sasa tunataka tujue tu tupate ufafanuzi. Je, Shirika lile limeshaanza rasmi au bado ikiwa bado ni kwa nini na ikiwa tayari limeshaanza kazi hili shirika, kwa nini basi kwenye kifungu cha ada ya ulinzi kifungu D0201 page 31 chini huku ada ya ulinzi ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zimewekwa Milioni kumi na nane, hizi pesa ni kidogo kama hili shirika limeshaanza kazi.

Nizungumzie kuhusiana na suala la barabara kwa vile barabara hizi za ndani (*feeder road*) ziko katika Halmashauri ya Wilaya, sasa nimesoma kitabu kwa bahati mbaya katika Wilaya yangu ya Dimani na hasa katika jimbo la ngu la Fuoni sijaona barabara hata moja, kwa sababu kuna barabara Mashine ya Maji, Mambosa, Kidarajani, kuna Mashine ya Maji/Nyarugusu, kuna Fuoni kwa Mabata/Mambosa, kuna fuoni Maharibiko/Kidarajani, kuna Fuoni/Kiembeni kuelekea nyumba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kuna njia ya Fuoni/Melisita/Msikiti wa Waarabu hadi Chunga. Najua Mhe. Waziri ni msikivu na ukiombwa unaombeka nakuomba sana barabara hizi nilizozitaja basi na mimi niweze kupatiwa matengenezo japo barabara mbili kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye fungu P03 Chuo cha Mafunzo ukurasa wa 48, tunajua kwamba Chuo cha Mafunzo kina vyanzo vingi vya mapato, lakini ukiangalia kwa mwaka wa fedha 2016/2017 chanzo kile cha mapato ya mifugo, naona kiko sufuri, sasa tunataka tujue kwa nini wale ng'ombe wamekufa au kuna tatizo gani hapa.

Vile vile ukija kwenye ukurasa wa 50 kwenye matumizi naona fungu hili pesa nyingi zimepelekwa kwenye utawala na uendeshaji ambapo asilimia 90 ya matumizi yamekwenda kwenye Utawala na Uendeshaji na asilimia 10 tu ya matumizi ndio yamekwenda kwenye huduma za urekebishaji wa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo. Kwa hivyo tulikuwa tupate uhakika hapa, kwa nini pesa nyingi katika hichi Chuo cha Mafunzo zimekwenda kwenye utawala, lakini katika eneo la urekebishaji wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kuna asilimia ndogo tu ya pesa hizi.

Nakuja katika ukurasa wa D04 ukurasa wa 58 mimi leo nita- *base* zaidi kwenye kitabu kikubwa hiki, kwenye ukurasa wa 58 kuna idadi ya matukio ya wasafirishaji wa magendo kwa mwaka 2015/2016 kuna matokeo manane, sasa hapa Mhe. Waziri nataka kujua katika haya matukeo manane ni watuhumiwa wangapi wamepelekwa Mahakamani na kesi zao zimefikia hali gani.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 60 hapa hapa kwenye KMKM mwaka jana kulikuwa kuna upungufu wa daktari wa uchunguzi anayetumia vifaa vya kisasa katika hospitali yetu ile ya KMKM, sasa je, yule mtaalam amepatikana au bado hajapatikana kwa hivyo tutaomba ufafanuzi kwa sababu hospitali ile inasaidia sana wananchi wetu…..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Muda upo karibu na kukutoka kwa hivyo malizia.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Kwa vile naheshimu kiti na kwa vile nilikuwa na michango mingi basi nitamuomba tu Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho basi anjibu hayo na mimi sina matatizo na bajeti hii ya Mhe. Waziri na naunga mkono kwa asilimia mia moja Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe kwa michangio yenu na utulivu wenu, sasa kwa kuwa muda ushakuwa karibu na kumalizika, naomba niwataje Waheshimiwa ambao hawakupata kuchangia waweze kuchangia kwa maandishi. Waheshimiwa wenyewe ni Mhe. Said Omar Said, Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Mhe. Shaibu Said Ali, Mhe. Masoud Abrahman na Mhe. Miraji Khamis. Hawa nitawaomba wachangie kwa maandishi kwa sasa na wakati wa jioni watakaopata nafasi ni Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri.

Kabla ya kuahirisha kuna tangazo limeletwa hapa; Katika semina yetu ya juzi Jumamosi kuna kitu kimeokotwa, hakijatajwa ni kitu gani, yeyote anayejijua katika waliohudhuria kule kama amepoteza amuone Mhe. Hidaya Ali Makame kwa kupata kitu hicho. Hilo ni tangazo moja tu baada ya hapo naomba kuchukua fursa hii kuliahirisha Baraza hadi wakati wa Jioni mnamo Saa 11.00. Ahsanteni.

(Saa 12.53 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 110.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum: (Mhe. Said Soud Said): Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nilikuwa nataka niseme kwamba bajeti iliyoletwa ya Wizara ya Katiba na Utawala Bora inamaanisha wazi kwamba ina malengo ya kuwafanya wazanzibari waweze kufikia pale ambapo panatakiwa. Inasikitisha sana kuona kwamba walio wengi wameshindwa

kuheshimi sheria na taratibu kwa visingizio mbali mbali, lakini vikiwemo vile vya kwamba miaka 5 iliyopita kulikuwa na watu wamo ndani ya Baraza hili na walikua ni Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, lakini walithubutu kusema kwamba wao hawajapata serikali.

Sasa kimsingi katika kipindi hicho walidhoofisha nguvu za serikali na hatimae leo hii tumefikia watu wanadai mambo mbali mbali kwamba hayakufanyika na hata taratibu za kisheria hazikufatwa na mambo mengi tu yalifikia pahala pa kuborongwa borongwa. Lakini kimsingi ni lazima tukubali kwamba nchi hii ina Katiba na ina sheria na lazima tuheshimu utaratibu tuliojiwekea wa vikosi vyetu vya Jeshi la Wananchi kutulinda vikiwemo Jeshi la Polisi, Vikosi vya SMZ. Hii inaonekana wazi kwamba huu ni utawala wa sheria na ni utawala ambao unaheshimu Katiba.

Sasa kimsingi akitokea mtu akisema kwamba kuna vikosi vinatumia nafasi yake vibaya basi atakuwa anasema tu, lakini yeye atakuwa ni mtu wa kwanza kukiuka sheria. Kwa sababu iwapo Polisi watakusimamisha au Vikosi vya SMZ vitakusimamisha ukishakujitangaza wewe ni nani ninaamini kwamba hawachukui hatua zisizofaa juu yako. Lakini kama utaleta za kuleta bado naendelea kusema kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako na baadae utafahamu kwamba hii ni nchi ya sheria na Katiba.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika kipindi cha miaka 5 iliyopita Wizara hii ya ambayo ilikuwa inaongozwa na Mhe. Haji Omar Kheri tunakubali wazi kwamba alikuwa anajitahidi kiasi cha kutosha kuendesha harakati zake katika Wizara hii lakini alikuwa anpigwa vita na wale waliokuwa hawatambui serikali iliyopo madarakani, pamoja na kwamba wao walikuwa ni wajumbe lakini walifikia pahala pa kusema wao hawajapata serikali. Sasa walidhoofisha nguvu za jeshi la SMZ. Walidhoofisha nguvu za wizara hii zikiwemo Tawala za Mikoa, wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani wao walikuwa ni watu ambao walitumia nafasi hiyo kwa misingi tu ya nguvu zao walizonazo. Sasa tunazungumzia kwamba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, tunaelewa wazi kwamba hawa watu wanahitaji kupewa nguvu na vyombo vyote vinavyohusika.

Sasa ni wajibu wetu sisi kama Wawakililshi tuliotoka katika majimbo na wale tulioteuliwa na Rais kutumia nafasi hii katika kuonesha mfano hai wa miaka 5 hii na sio kuja humu tukalaumiana, jambo ambalo lilikorogwa na watu wengine tukawavisha watu shida katika kipindi hiki. Wizara hii ni Wizara mama kwa sababu watu wote wanalala usingizi kwamba wanalindwa, wanahudumiwa na matatizo yao mbali mbali yanaepukika kwa sababu vikosi vya SMZ

vimejipanga imara katika kulinda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwalinda wazanzibari wenyewe na kama kutakuwa na mtu hajaliamini hilo maana yake ni kwamba yeye halali huyo. Mtu usiku kucha anakaa macho lakini kama anapata usingizi basi ahesabu kwamba Jeshi la Polisi na Vikosi vya SMZ vinamlinda, ndio akapata usingizi na kutoa maamuzi yake.

Mhe. Naibu Spika, ningetaka niseme kwamba wakati umefika wa kukubaliana na bajeti hii na kuipitisha kwa moyo safi ili kuweza kumfanya Mhe. Waziri afanye kazi yake inavyotakiwa na aweze kuwatendea wazanzibari haki kwa mujibu wa Katiba. Sisi kama serikali tunaamini wazi kwamba tutakuwa tayari kuhakikisha kwamba kila aina ya jipu lilipojitokeza kulipasua na kuwafanyia wazanzibari haki. Tunawashauri wananchi wa Zanzibar wapenda amani waweze kuendelea kuheshimu sheria na utawala, kuheshimu Katiba na Kanuni zake ili tuweze kufika pahala, tujenge nchi yetu bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hiki tunachokwenda nacho ni kipindi ambacho wenzetu wengi wanaangalia kwamba kweli itawezekana, lakini sisi tunawaambia kwamba itawezekana zaidi na zaidi kuliko vile walivyokuwa wakitaka wao. Kwa sababu nchi hii haikuwa na hati miliki ya CUF kwamba lazima waingie wao katika Baraza hili ndio mambo yaende. Nchi hii ina vyama vingi 22 kwa mujibu wa Katiba na Kanuni na ndivyo vyenye usajili wa kudumu, kwa vile kikikengeuka kimoja, viwili, vitatu, vitano, kumi basi nchi hii inaendelea. Tunasema wazi kama sisi ni serikali tutahakikisha kila lililokuwa limeharibika kulisimamia. Serikali inatoa wito kwa watendaji wabovu wote wajirekebishe, vyenginevyo tutapasua majipu yao hadharani na tunasema hivyo kwa sababu sisi tumeingia humu kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi ndio walioamua kutukubali na wakatuamini kwamba tutasaidia kutetea na kulinda Katiba ya Zanzibar.

Sasa mimi sitokuwa tayari kumuona mtu anavurunga kwa makusudi eti kwa sababu tu yeye anaongoza Taasisi, kama yeye anaongoza Taasisi mimi ni Waziri nitatumbua jipu lake popote atapolificha na nitamsaidia Rais usiku na mchana kuhakikisha kwamba nchi inakuwa salama na amani. Ninasema hivi kwa maana kuna watendaji katika kisiwa cha Pemba wamejifanya wao kwamba eti hawajapata serikali ya kuitumikia. Sasa mimi natoa salamu na natoa wito kwao wajue kuwa kwamba serikali iliyopo madarakani sasa hivi, inaongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein kama Rais wa Zanzibar na tayari Baraza lake la Mawaziri lipo, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapo, Manaibu Waziri wapo, Wakuu wa Mikoa wapo, Wakuu wa Wilaya wapo. Sasa serikali kamili ipo na kwa maana hiyo hatutomuonea haya mtu, tutakuwa tayari ama atakubali au ataacha kazi afanye shughuli zake.

Huo ndio wito wangu na ninawaomba wawakilishi, mimi naunga mkono bajeti hii na nawaomba wawakilishi tuunge mkono bajeti hii ili tuweze kuendelea na utaratibu wetu wa miaka 5 ijayo ili kuifanya serikali iweze kufanya wajibu wake kama vile wananchi wanavyotaka. Nataka niseme wawakilishi tafadhalini musifiche kila mnaloliona, semeni ili kuwafanya wananchi waliowachagua wajue kama kweli mmekuja kuwasemea na kuwatetea. Hakuna maana kwamba nyinyi muje humu mufunge midomo mutie zipu, semeni na sisi tuko tayari kuwajibu hoja zenu ili wananchi wasikie kwamba tunawafanyia kazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, nimemaliza, naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nami sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutukutanisha jioni hii tukiwa wazima bukheri wa afya ili kuweza kushirikiana pamoja katika kulijenga taifa letu hili lende mbele kimaendeleo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hapa tokea juzi bajeti hii adhimu ambae imekusanya mambo mengi tu yatotusaidia sana mustakbali wa nchi yetu.

Baada ya kusema hayo machache sasa niende moja kwa moja kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na wajumbe wako watukufu kuhusu masuala mbali mbali yanayohusu sekta ya ujenzi, mawasiliano na usafirishaji. Wajumbe wameelezea kutokana na hamu yao na ari yao ya kuona kwamba barabara hizi ambazo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inahakikishwa kwamba zinajengwa ili na wao wawakilishi wapate kuona kwamba kweli serikali yao inakusudia au ina nia ya dhati kabisa katika kuwaletea wananchi maendeleo yao.

Mimi napenda kuwatoa shaka wawakilishi walioko ndani ya Baraza hili tukufu kwamba serikali ina nia ya dhati katika kuhakikisha kwamba inaondosha kero zote zile za wananchi wetu hasa katika hii sekta ya miundombinu ambayo ni sekta ya kiuchumi, ili kuwawezesha wanachi kufanya kazi zao kwa urahisi ili wajipatie kipato chao. Zimezungumziwa barabara hizi kwamba halmashauri wataweza kuzitekeleza peke yao, mimi kama ninavyosema siku zote kwamba wawakilishi wasiwe na wasiwasi kuhusu suala hili, kwani kama halmashauri wao kazi yao kubwa itakuwa ni ku-*outsource* maana yake kuwapa watu wa nje au kutoa tenda ili hizo kazi zifanyike.

Wizara imepangiwa bajeti yake lakini sio hivyo pale ambapo itaonekana na sisi kama wizara tuna haja ya kushirikiana nao basi hatutosita kufanya hivyo kwani

ni hii *teamwork* ambayo sote tunafanya kazi moja ya kuhakikisha kwamba ilani ya uchaguzi ya CCM inatekelezwa ipasavyo, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaendelea kuwa na imani na Chama cha Mapinduzi na chama chetu hiki kinaendelea kutawala milele na milele.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe waliulizia hapa kuhusu hizi barabara, kama nilivyosema kwamba barabara hizi zitajengwa awamu kwa awamu na katika kila kama walivyosema wenzangu kupanga ni kuchagua, zitachaguliwa barabara ambazo bajeti zake zitakidhi kutengenezwa kwa kipindi hicho na kipindi chengine kama zitabakia basi tuna imani kwamba Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi wa namna gani barabara hizo zitajengwa.

Mhe. Bahati aliuliza kuhusu barabara ya Ole Kengeja, kwamba je, itafika mpaka kule Likoni kunakouzwa samani. Mimi nataka kumwambia tu kwamba Mhe. Mwakilishi ile barabara haitopita kule lakini Mhe. Rais kama alivyokuwa akifanya hapo kabla anaangalia vile vile mahitaji muhimu ya wananchi katika kutekeleza ilani ya CCM. Ninampa mfano mzuri wa barabara ya Chwale Kojani, ile barabara ilikuwa haifiki mpaka kule chini pwani, lakini kwa hekima za Mhe. Rais alituagiza sisi ile barabara mpaka kule chini Likoni na matokeo yake barabara ile tumeipeleka mpaka kule Likoni.

Vile vile kuna barabara ya Raha/Ukunjwi ilikuwa hadi kwenda Likoni kama kuna mita 400 Mhe. Rais akatoa ahadi kwa wananchi wa Jimbo la Gando na matokeo yake ile ahadi tumeitekeleza na barabara ile imefika mpaka kule chini Likoni na hivi sasa wananchi wa kule wamesema kwamba tuipitishe chini kule kabisa kwenye bahari kama ilivyofanywa ya Kojani na hili tutakaa sisi kuliangalia pale hali ya fedha itaporuhusu ili kurahisisha usafiri na vile vile kazi za uvuvi ziende kwa haraka.

Vile vile tuliulizwa kuhusu vituo vya daladala; kama tunavyojua Wizara hii ya Mhe. Haji Omar Kheri wao huwa wanaangalia vile vituo na baadae kuja kutoa ushauri kwetu sisi. Baadae hapo sisi hukaa pamoja na wao na kuangalia uwezekano je, hivi vituo kweli vinafaa kuwekwa? Baada ya kuangalia na kutathmini ndio baadae linatoka tangazo la Mhe. Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji kuhusu uthibitisho wa vituo hivyo. Kama walivyosema kuna vituo vimeuliziwa hapa vya Konde, kituo cha Chake Chake cha pale stendi na vile vile wameulizia wengine kituo cha Wete.

Nataka kusema kwamba tuna kamati zimeundwa kamati hizo zinajumuisha pia Wizara ya Tawala za Mikoa na Wizara ya Ardhi ili kuangalia kutafuta maeneo mengine ambayo tunaweza kuweka vituo vile ili kuondosha usumbufu kwa

wananchi wetu. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawapati kero hizo za kusafiri masafa marefu ndio maana tunahakikisha wakati wowote kwamba vituo hivyo vinakuwa karibu ili kuondoa ile kero ya mtu akitaka kushuka kutembea masafa ya mbali zaidi wakati barabara zetu zinaruhusu kwa mujibu wa sheria, kuwepo na vituo ambapo pale inaonekana vinaweza kukaa hivyo vituo.

Kwa hivyo, tunawaambia kwamba wasiwe na wasiwasi kamati zinafanya kazi zake vizuri na zinafanya uchambuzi yakinifu na baada ya muda kamati hizo zitatoa taarifa nzuri tu katika vituo hivyo ambavyo sisi tumekusudia kuvifanyi kazi. Kwa hivyo ninawaomba wananchi kupitia Baraza lako tukufu wawe wastahamilivu mpaka hapo tutapomaliza kazi hiyo na baadae kupeleka katika hatua zaidi ya utekelezaji wake.

Mwisho kabisa naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuipitishe bajeti hii kwani bajeti hii ni robo ya nchi yetu inakusanya mambo mengi tu; mambo ya ulinzi, mambo ya usalama pia yako huku, mambo ya miundombinu na mambo mengine Mtambuka. Kwa hivyo muone umuhimu wa wizara hii ambayo ukiangalia kwa kiasi kikubwa serikali imekuwa ikiwatilia bajeti fedha kila wakati kwa kutambua umuhimu wake. Mimi niishukuru sana Wizara ya Fedha kwa kutambua umuhimu wa wizara hii na kuwaunga mkono na nina imani kubwa wawakilishi wenzangu wataendelea kuiunga mkono hotuba hii ili tuendelee kuwatumikia wananchi wetu.

Baada ya kusema hayo machache mimi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi ninaiunga mkono hoja hii na kuwaomba sana waheshimiwa wawakilishi waiunge mkono ili tupate kuitekeleza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ipasavyo ya kuwaletea wananchi maendeleo yao. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa bajeti nzuri aliyoisoma vizuri lakini pia nipongeze kwa utekelezaji mzuri pamoja na changamoto mbali mbali zinazoikabili wizara hii. Niwapongeze watendaji Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na niwapongeze pia wakuu wa Vikosi vyote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mhe. Naibu Spika, nina maeneo machache niliomba nichangie na kuna maeneo mengine nitatoa ufafanuzi.

Eneo la kwanza ni kuhusiana na taa za barabarani ambalo sana eneo hili lilizungumzwa sana na Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi wa jimbo la Jang'ombe na yeye alitaka kujua iwapo sheria ya manunuzi ilifuatwa katika kumpata mjenzi au mfungaji wa taa hizi. Nieleze tu kwamba Sheria ya Manunuzi Nam. 9 ya mwaka 2005 ilifuatwa kikamilifu, na mwekaji wa taa hizi ilikuwa ni Kampuni ya **Centro** ambayo ina makao makuu ya Dar es Salaam. Ilifanywa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi, na barabara zilizohusika naomba nizisome Mhe. Naibu Spika kupitia Mradi wa *ZUSP*; barabara zilizohusika katika uwekaji wa taa za barabarani ni barabara inayotoka Kwabiziredi hadi pale makutano ya barabara ya Amani *round about*.

Njia ya pili ilikuwa ni hii inayotoka Amani *round about* mpaka Mwanakwerekwe *round about* ambapo kwa kiasi kikubwa imekamilika. Lakini na nyengine inatoka Mwanakwerekwe *round about* inapita njia ya Kwa Boko hadi Kariakoo, na vile vile njia ya Vuga inayopita Serena mpaka kwenye jengo la Wizara ya Ardhi. Lakini pia taa hizi zinawekwa katika maeneo ya Mji Mkongwe kwa asilimia 75 ya eneo lote la Mji Mkongwe, lakini pia zitawekwa katika Bustani ya *Victoria*, bustani ya Jamhuri *Garden* na pale eneo la wazi *African House.*

Mhe. Naibu Spika, kimsingi ni kwamba taa zote hizi hakuna taa hata moja iliyokuwa haiwaki, lakini inaweza Mhe. Mwakilishi aliona labda kuna baadhi ya taa haziwaki, lakini hiyo ilifanyika makusudi kwa sababu ilikuwa kwenye majaribio. Ziko taa ambazo zilizimwa makusudi kwa ajili yaku-*test* uwezo wa zile betri wa ku-*recharge*. Kwa hivyo, kama aliziona hizo taa haziwaki ni kwa sababu hiyo, lakini taa hizi zinatumia mifumo miwili. Mfumo mkuu ni mfumo ule wa *solar*, lakini vile vile zimeunganishwa na nyaya za kutumia umeme wa kawaida. Kwa hivyo, bado tuziamini taa, ziko vizuri, mjenzi huyu ni makini na amechaguliwa kwa mujibu wa taratibu zote za kisheria.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, lilikuwa ni ujenzi wa misingi ya kutolea maji ya mvua (*store motor drainage system*). Hili lilizungumzwa na Mhe. Hamza na yeye alitaka kujua ni lini ule msingi kutoka Kwamtipura kwenda Darajabovu utajengwa. Hapa nieleze tu kwamba ni kweli misingi yote ambayo imo ndani ya mradi huu, ambayo inahitaji fidia misingi hiyo bado haijaanzwa kujengwa. Misingi iliyoanzwa kujengwa ni ile misingi ambayo haikuhitaji fidia. Nasema hilo kwa sababu tayari serikali imeshachukua hatua na hili nililieleza Mhe. Naibu Spika, wakati nilipokuwa nawasilisha Bajeti ya Serikali, kwamba fidia hii tayari serikali imeshaifanyia kazi, fedha hizi zilishapatikana tunakamilisha taratibu ili tuweze kuwalipa fidia zao wananchi watakaohusika na kulipwa fidia

katika ile misingi ambayo itahitaji kulipwa fidia. Mhe. Naibu Spika, mmoja wapo utakawa ni msingi huu wa Kwamtipura na Darajabovu.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi bilioni sita zitahitajika na niseme tu wakati wowote kuanzia mwezi wa Julai, Mwenyezi Mungu akipenda huenda shughuli hii ya ulipaji wa fidia itafanyika.

Eneo la tatu lilikuwa ni eneo la uvujaji wa mapato hasa katika suala zima la magendo ya mafuta. Nikubaliane na Mhe. Suleiman Ali Makame wa Jimbo la Ziwani aliyesema kwamba yako maeneo ambayo yanatumika katika kupitisha mafuta ya magendo. Ni kweli na hiyo inaikosesha mapato nchi yetu. Na ziko njia tatu watu hawa wanazitumia, njia ya kwanza ni vyombo vyenyewe vinavyochukua mafuta kutoka labda Mombasa au Tanzania Bara, hivyo navyo vinavujisha baadhi yao. Na wanachokifanya ni kwamba wanamuibia hata huyo mmiliki wa meli hiyo, kwa sababu wanachokifanya ni kununua mafuta zaidi ya yale wanayoyahitaji. Katika kukisafirisha chombo kile labda kutoka Mombasa kuja Zanzibar ukiacha yale mafuta yenyewe yaliyochukuliwa wao wanajaza mafuta zaidi ya mahitaji ya ile safari.

Nakusudia mafuta yanayotumika kwa ajili ya safari hiyo, yale mafuta ya ziada ndio yanayotoka kimagendo na kuuziwa watu na kuingia katika soko. Lakini yako mafuta ambayo yanachukuliwa na vyombo vyengine vidogo vidogo, mabumu, majahazi yanachukua mafuta kupitia kwenye madumu. Pia wako watu ambao wanaiba mafuta haya pale kwenye *depot.* Mafuta yakishashushwa kwa kawaida mapato huwa yanakusanywa kwa yale mafuta yanayotoka *depot* kwenda kwenye vituo. Sasa huo ujanja tumeuona na kuanzia mwaka huu wa fedha mafuta yataanza kulipiwa mapato yataanza kukusanywa pale meli inapoingia. Kwa hivyo, inapoingia meli mafuta yatapimwa pale, lakini yatakapoingia *depot* napo tutapima tena kuhakikisha kama kweli mafuta yale yaliyotoka kwenye meli yamefika kwenye *depot* na *charge* ya mapato itaanzia hapo, hatutosubiri yatoke hapo kwenda kwenye vituo.

Mhe. Naibu Spika, chengine katika kudhibiti hili tungeomba sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vinafanya kazi nzuri, lakini wananchi nao wasaidie kwa sababu kuna bandari bubu nyingi ambazo zinatumika katika kupitisha magendo ya mafuta. Wananchi watoe taarifa na siku hizi kuna *incentive* maalum ambayo inatoka, pale mwananchi atakapotoa taarifa basi asilimia 20 ya thamani ya kile kitu alichokitolea taarifa atalipwa yeye. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo tunahitaji tushirikiane sote kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, eneo la nne ni la Mradi wa *CCTV* ambalo katika bajeti hii limeekewa jumla ya shilingi bilioni 18. Mhe. Hamza alilizungumza sana na wapo waheshimiwa wengine ambao walilizungumza hivyo hivyo, naomba niseme tu kwenye hili tayari tulikwishalipitisha katika ile bajeti kuu ya serikali. Lakini niseme tu kwamba *CCTV* imetumika kama jina, lakini ndani ya mradi huu kuna vifaa vingi sana ambavyo ni muhimu vitakavyonunuliwa kwa ajili ya usalama na ulinzi katika nchi yetu. katika hayo yapo mambo ambayo tunaweza kuyasema hapa wazi wazi. Kwa mfano, kuna *scanner* kubwa ambayo *scanner* hii inaweza ku-*scan* gari zima likipitishwa kwenye ile *scanner* linakuwa *scanned*. Lakini ziko *scanner* nyengine ndogo ndogo, pia kuna boti za kisasa zenye *speed* kubwa ambazo zina uwezo wa kwenda *nautical miles 60* kwa saa wanaziita *in the sector*. Kuna magari ya *fire* mheshimiwa yamo humu, kuna mafunzo yatakayotolewa yamo humu, kuna mambo mengi sana.

Hizi *CCTV camera* ni asilimia 10 tu ya vifaa vyote au ya mradi wote unaokusudiwa kutekelezwa. Kwa hiyo, wasiwe na wasi wasi viko vitu dunia nzima nchi nyingi hawawezi ku-*disclose* vitu vyao ambavyo hasa ni vya ulinzi na usalama, na hata huko vinako nunuliwa Mhe. Naibu Spika, ni lazima ipatikane *end user certificate* ihakikishwe kabisa kwamba vifaa hivi havitobadilisha mkono visije vikaingia kwenye mkono wa majangili au wasio stahiki kuwa na vifaa hivyo. Kwa hivyo, lazima itoke hiyo *certificate* na *certificate* hiyo imetoka. Lakini tunazungumzia suala la kwamba je, utaratibu wa manunuzi ulifuatwa? Sasa Sheria ya Manunuzi Nam. 9 ya mwaka 2005 kipo kifungu nadhani kifungu cha 70 na kifungu 67 viko wazi.

Kifungu cha 70 kinazungumzia mambo ya *restricted tendering* iko wazi, na mambo ya usalama haya yako wazi kwamba unaweza kwenda kwenye *single source* umtafute mtu mwenye uwezo na taaluma hiyo, unaweza kununua vifaa hivyo kwa kutumia njia hiyo ya *single source*. Kwa hivyo, hakukuwa na tatizo la kwamba *procedure* haikufatwa na huwezi ukatangaza *tender* kwenye vifaa ambavyo ni vya ulinzi na usalama. Ukianza kutangaza *tender* ina maana hilo jambo tayari umeshaliweka wazi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika kuchangia ni hili la ujenzi wa vituo vya uokozi. Hapa nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri, lakini pia nimshukuru sana Mhe. Rais mwenyewe kwa maamuzi thabiti ya kuanzisha vituo vya uokozi katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Na hili uamuzi huu ulitokana baada ya kutokea zile ajali za meli *MV. Spice Islander, MV. Skagit* na pale serikali ilifanya maamuzi ya kwamba lazima tujenge vituo katika kila Wilaya vituo vya uokozi.

Nashukuru na nampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wote wa wizara hii, kwamba tayari kazi hiyo imeshaanza kufanywa, kituo kimoja tayari kimeshajengwa pale Kibweni na kimeshakamilika. Lakini pia kiko kituo chengine kinaendelea cha Mkoani ujenzi wake umo katika hatua za kukamilika. Lakini katika mwaka huu wa fedha, fedha zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo kama hicho Kizimkazi, Wete, na Nungwi. Kwa hivyo vyote vitakuwa jumla ya vituo vitano. Lakini pia fedha zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa boti zitakazokuwa kwenye vituo hivyo. Kwa hiyo, tutakuwa na boti tano katika huu mwaka wa fedha ambazo zitasaidia sana pale yanapotokea maafa ili wananchi wetu waweze kupata huduma hizo za haraka katika maeneo na vituo *strategic* kama nilivyokwisha kuvisema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kama utaratibu na kanuni na sheria zilivyo za uendeshaji wa Baraza la Wawakilishi, kwamba baada ya mtoa hoja kutoa hoja yake, Waheshimiwa Wajumbe wanapata nafasi ya kuweza kutoa maoni yao, na hatimae anaruhusiwa mtoa hoja kuja kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mwenyezi Mungu muumba wa yote duniani aniwezeshe kujibu hoja hizi bila ya jazba, bila ya kuhisi aliyetoa hoja hii ana jambo. Hata mimi nilikuwa *backbencher for fifteen years* nimekuwa na hakuna waziri yeyote wa serikali hii aliyewahi kunikataza juu ya hoja ambayo nimeitoa, isipokuwa inapofika pahala kwamba hoja niliyokuwa nikiitoa haikuwa sahihi. Nadhani kazi yetu kubwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kuambizana kwamba hapa nadhani si sahihi na usahihi uko huu. Namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kufanya kazi hii kama nilivyokula kiapo kwa dini yangu ya Kiislamu na kumuahidi Mhe. Rais kwamba nitaifanya kazi hii ya uwaziri kwa kumshauri kwa hekima kabisa na kutimiza majukumu yangu kwa mujibu wa Katiba. Bila shaka na wajumbe wengine wamekula kiapo hicho.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni waziri sehemu moja, sehemu ya pili mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na viapo hivyo nimevila. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe msiwe na wasi wasi kwamba pengine nitamuona mjumbe aliyeuliza hoja ni mtu wa ajabu, nikifanya hivyo nitakuwa sifai kuwa

waziri. Ni imani yangu Mhe. Rais nimefanya kazi nae katika kipindi cha miaka mitano, sina hakika vigezo gani ametumia lakini kwa kuniteua kwake mara ya pili ina maana nina uwezo wa kufanya kazi hii ya uwaziri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niwashukuru sana na kuwapongeza sana wajumbe wote ambao wameichangia hotuba yangu ya bajeti, ambayo ilielezea mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016, na mwelekeo wa bajeti wa mwaka 2016/2017. Mchango wao umenipa ujasiri ambao umechangiwa na wajumbe 28 kwa kusema pamoja na mawaziri 3 maana yake ni wajumbe 31 wamechangia bajeti yangu, na wajumbe 9 wamechangia kwa maandishi. Hiyo ni kuonesha kwamba wajumbe wa Baraza hili tukufu wamepata nafasi nzuri ya kuielewa bajeti hii na wameweza kuchangia na nawapa pongezi za dhati kwa michango yao ambayo wameichangia bajeti hii.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, hiyo ilikuwa ni dibaji na mimi nimejiandaa kujibu au kutoa ufafanuzi wa hoja na masuali yaliyoulizwa. Nitayajibu kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi na sheria, sitajibu pengine kwa vile mtu atakavyoona yeye inafaa nimjibu. Sisi tunatoa ufafanuzi kwa utaratibu ambao tumejiwekea sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nawapongeza sana waheshimiwa wote ambao wamempongeza Mhe. Rais, nazipokea pongezi hizo kwa niaba ya Mhe. Rais, napokea pia pongezi kwa wale walionipongeza na wale wasionipongeza. Nawapongeza pia waliowapongeza watendaji wangu kwa kunisaidia kazi hii, ni kweli bila ya timu ya watendaji nisingeweza peke yangu kuja kuwasilisha hotuba hii hapa Barazani. Lakini napokea pongezi za Waheshimiwa Wajumbe walioipokea timu mpya ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya walioteuliwa. Kuna mjumbe mmoja Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) amewaita ni *green tea* kwa hiyo nadhani *green tea* ni kinywaji kizuri kama hivyo ndivyo nilivyoelewa. Lakini kwa ujumla wajumbe wote wamewapongeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya wale walioteuliwa hivi karibuni, lakini hata wale waliobakia maana yake wanaendelea kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba kutoa shukurani za dhati kwa kunipa fursa hii kama nilivyosema mwanzo. Nitumie fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini Mhe. Machano Othman Said. Niwapongeze pia wajumbe wake wote kwa mashirikiano yao mazuri na wameanza na mimi vizuri katika kuipitia bajeti hii,

na kule kwenye kamati hakujitokeza mjumbe yeyote wa kamati kuikataa bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, nasema tena, kwenye Kamati kwa Wajumbe wale wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, hakujitokeza Mjumbe yeyote kuikataa au kuhoji nikashindwa kumjibu hoja yake yoyote ile. Kwa hiyo nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano mazuri ambayo walinipa katika kuipitia bajeti hii na michango yao imeniwezesha mimi kwenda kuiandika na kuiandaa na nikathubutu kuja kuiwasilisha hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo nawashukuru wale wote waliochangia hotuba hii lakini pia kwa Niaba ya Mhe. Rais, nipokee pongezi alizopengezwa kwa kuwateuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji waliochangia moja kwa moja kama nilivyosema mwanzo walikuwa ishirini na nane (28) na Mawaziri watatu wa mwisho wanafanya bajeti hii kuwa imechangiwa kwa kusema moja kwa moja na Wajumbe 31. Na Wajumbe ambao wamechangia kwa maandishi kama nilivyosema ni tisa. Nianze kuwataja:

1. Mhe. Machano Othman Said
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpaka basi)
6. Mhe. Hidaya Ali Makame
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Nassor Salim Jazira
9. Mhe. Bihindi Hamadi Khamis
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Sheha Hamad Mattar
12. Mhe. Abdalla Ali Kombo
13. Mhe. Suleiman Sarahan Said
14. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
15. Mhe. Suleiman Makame Ali
16. Mhe. Ali Khamis Bakari
17. Mhe. Bahati Khamis Kombo
18. Mhe. Hamza Hassan Juma
19. Mhe. Omar Seif Abeid
20. Mhe. Hassan Khamis Hafidh

21. Mhe. Asha Abdalla Mussa
22. Mhe. Maryam Thani Juma
23. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
24. Mhe. Khadija Omar Kibano
25. Mhe. Ame Haji Ali
26. Mhe. Mohammed Said Dimwa
27. Mhe. Mussa Foum Mussa
28. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
29. Mhe. Said Soud Said
30. Mhe. Mohammed (Naibu Waziri wa Miundo Mbinu) na wa mwisho
31. Mhe. Khalid Salum Mohammed.

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
4. Mhe. Mwanaasha Khamis
5. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
6. Mhe. Miraji Khamis Mussa
7. Mhe. Masoud Abrahman
8. Mhe. Mgeni Hassan Juma na
9. Mhe. Shamata Shaame Khamis

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wote hawa wanafanya idadi ya Wajumbe ambao wamechangia hotuba yangu ni arubaini (40). *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe hawa kwa michango yao yote na kama nilivyomuomba Mwenyezi Mungu na ninaendelea kumuomba aniwezeshe kujibu na kutoa ufafanuzi na yale mengine pengine kwa sababu ya wingi kwa maelezo nitawajibu kwa makundi na mengine yale ambayo tumeshauriwa kama pengine sikupata nafasi ya kuweza kuyasema hapa tunayachukuwa kwa ajili ya ushauri kama tulivyoshauriwa. Nataka niwahakikishie kwamba yale yote ambayo tumeshauriwa basi tutakwenda kuyafanyia kazi na hasa kwa kuzingatia kwamba Wajumbe wa Baraza hili tumekula kiapo, tumekuja kwenye kikao cha Baraza la Bajeti hatukuwahi kufanya ile kazi ya utafiti kwa niaba ya Baraza. Sasa nadhani wajumbe wa kamati watapata nafasi nzuri baada ya kwisha kupitisha bajeti hii ya kuja kwenye ofisi yangu na ofisi nyengine za Serikali za Wizara mbali mbali

kufanya utafiti, ili kuona haya tunayoyasema na yale ambayo pengine watayakuta kule kwenye ofisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kutoa michango yao zilijikita katika maeneo mbali mbali yakiwemo haya yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, barabara za ndani za nchi nzima, maslahi, vitendea kazi, maadili ya wapiganaji wa Idara Maalum na utoaji wa ajira kwa Idara Maalum za SMZ. Uwekaji wa CCTV za ulinzi, hatua za kuapishwa Madiwani, mapato kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, maegesho, masoko, usafi wa mji kwa ujumla na utayari wa mageuzi ya serikali za mitaa.

Nyengine ni utaratibu wa utoaji vitambulisho na mikakati juu ya mradi wa ZUSP na utaratibu wa uchelewaji wa *certificate* za vizazi na vifo.

Mhe. Naibu Spika, pia katika mchana huu lilijitokeza suala la uzururaji wa ng'ombe na kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar ambayo ameitoa kwa kipindi kirefu ya kwanini kama nchi ya mapinduzi hatuchukui hatua haraka. Lakini pia na mambo mengi mengineyo ambayo yamewasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Nikianza na Mhe. Machano Othman Said-Mwenyekiti wa Kamati, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nampongeza sana kwa hatua yake nzuri. Alionesha matumaini makubwa ya kuendelea kuimarisha ofisi yetu, kwa niaba ya ofisi tumezipokea pongezi zote walizozitoa katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, aidha nakubaliana na maoni ya Kamati kuhusu hoja zilizotolewa zikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, upatikanaji wa majengo ya ofisi, uingizwaji wa fedha kwa taasisi za ofisi kuu, kuimarisha shughuli za uzalishaji mali kwa Idara Maalum, kutoa utaratibu wa maegesho ya magari kwa watu binafsi, kutoa ajira za kitaalamu kwa mabaraza ya manispaa, mabaraza ya miji na Halmashauri za Wilaya, kuwapatia ajira za kudumu wafanyakazi wa muda waliotumikia kwa muda mrefu katika Serikali za Mitaa, kuziwezesha mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoanzishwa na kuendelea kuwapatia vitambulisho Wazanzibari na wasiokuwa Wazanzibari wanaoishi kisheria.

Mhe. Naibu Spika, ushauri huo karibu wote ambao umetolewa na Mhe.Mwenyekiti, na Waheshimiwa wengine ndio mambo ya msingi ambayo tumeyaeleza katika hotuba yetu ya bajeti ukiangalia.

Mhe. Naibu Spika, Idara Maalum za SMZ na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum zimepatiwa asilimia ndogo ya fedha. Hoja hii imetolewa na Waheshimiwa wa kwanza; Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Suleiman Sarahani na Waheshimiwa wengi wamelizungumza hili. Maelezo ya hoja ni kweli katika fungu 0D1, ukiangalia kwenye kiambatanisho No. 5 Waheshimiwa Wajumbe, kwenye kiambatanisho No.5 ambacho kimeonesha wazi wazi asilimia ndogo ambazo zimezungumzwa za Tume ya Utumishi Idara Maalum, na Idara ya Utaratibu kwa Idara Maalum.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kwenye fungu hilo ambalo Wajumbe wamelizugumza utakutia uratibu wa Tawala za Mikoa kwenye OC kuna asilimia hiyo kama Wajumbe walivyosema, kwenye uratibu wa Idara Maalum kuna asilimia nane. Kuna Tume ya Utumishi asilimia sita, mipango sera asilimia tatu, utumishi na uendeshaji asilimia ishrini na sita na ofisi kuu Pemba asilimia arubaini. Kwanini asilimia ishirini na sita, kwa sababu zile huduma nyengine zote ambazo wanazitumia Idara hizi nyengine zinapitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Na kwa kuzingatia hii Tume ya Utumishi Idara Maalum na Idara ya Uratibu wa Idara Maalum, watumishi wake wote wanalipwa mafao yao na maslahi yao katika Idara zao maalum, kwa sababu wafanyakazi wa idara hizi na wafanyakazi wa Tume hii wote ni Askari kwa lugha nyengine ni wapiganaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo ukiangalia kwenye kiambatanisho hichi No. 5 kama tungetofautisha OC basi utakutia ofisi zote yaani fungu hili D01 basi kiwango chake cha kupata asilimia ni ndogo. Kwa hiyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe hilo na sio kwamba pengine labda kulikuwa na mambo ya kuwanyima. Lakini wafanyakazi hawa wanaposafiri kikazi fungu wanalolitumia ni la ofisi ya uendeshaji na utumishi kwasababu ndipo kwenye gharama hizo.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya pili, ilikuwa ni barabara za ndani. Hoja hii kwanza ilikuwa na swali hasa kwa Mhe. Nadir mchangiaji wa mwanzo katika suala hili, aliuliza kwanini mamlaka za Serikali za Mitaa zinajenga barabara hizi za ndani. Kwa mujibu wa sheria No. 7 ya mwaka 2014 kifungu cha 26(1)(d) ndicho kimeipa au kinazipa mamlaka za Serikali za Mitaa kushughulikia barabara za ndani na sio utashi kama pengine mnavyodhania. Kwa hivyo hili ni jukumu letu la msingi na mimi kamaWaziri ninaesimamia suala hili hili ni jukumu

langu la msingi. Ni kweli Idara ya Utunzaji na Ujenzi wa Barabara inalo jukumu hili. Lakini sisi pia tunapokuwa na nyenzo ya kuweza kujenga barabara za ndani tunaweza hata tukawaajiri Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kuifanya kazi hiyo, kama tunavyoziajiri kampuni nyengine.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengine waliochangia, wamechangia Wajumbe wengi na mimi nataka niwashukuru kwamba Wajumbe wote wameonesha kukubaliana na wazo hili na sisi kushughulikia hizi barabara za ndani. Na kama nilivyosema wazo hili limetolewa Mhe. Nadir Abdulatif, lakini yeye nimepata kutoa ufafanuzi kwa sababu alitaka kujua ni kwanini sisi, sasa ufafanuzi wake ni huo.

Mhe. Naibu Spika, lakini hoja hii ilichangiwa na Mhe. Nassor Salim Jazira, Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), Mhe. Mwanaasha Khamis, Mhe. Zulfa Mmaka, Mhe. Massoud Abrahman na wengi wengineo. Na Waheshimiwa Wajumbe wametaka kujua jambo hili ni vipi? Ni kweli sisi vyanzo vyetu vya ujenzi wa barabara cha kwanza ni *resources* zinazotokana na mapato yetu kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa. Cha pili ni *fund* ya mfuko wa barabara, cha tatu tuna uwezo wa kuomba misaada, mikopo kwa ajili ya kujenga barabara hizi iwapo mahitaji hayo yapo. Na kweli mahitaji hayo ya ujenzi wa barabara za ndani yapo. Na sera yetu sisi ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

Mhe. Naibu Spika, na kwanini tumeamua kuwa na haya kwa sababu tumeona barabara nyingi ambazo zimekuwa zikifadhiliwa na Serikali za Mitaa zinajengwa kwa kifusi baada ya muda mdogo barabara zile zinakufa. Kwa hiyo katika eneo hili la *resources* zinazotokea kwenye Serikali za Mitaa bado ni finyu na hilo ni jukumu la madiwani watakapokaa kwenye Halmashauri zao kwenye Mabaraza yao kupanga sasa ipi ambayo haipitiki na inahitaji huduma ya mwanzo irekebishwe ili wananchi waweze kupata huduma, waweze kufika hata kama ule mpaka wa kuweza kuijenga kwa kiwango cha lami haujafika.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwanini tumejenga barabara ambazo tumezitaja kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti, tumejenga hizo kutokana na mgao wa *percentage* tunayoipokea kutoka kwenye mfuko wa barabara. Kwenye *percentage* ya *hundred percent* yaani asilimia mia moja Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa barabara inapewa asilimia thamanini na tano. Sisi tunapewa asilimia kumi na tano. Asilimia kumi na tano kwa bajeti ya mwaka tunaoenda nao ni sawa na 1.5 bilioni, ndio tumeweza kujenga hizo barabara kama tulivyoanza barabara ya mwembe kisonge kuzunguka kwenye mnara wa kumbukumbu ya mapinduzi. Ujenzi tunaoendelea nao wa barabara ya

Kilimani, ujenzi tulioendelea nao wa barabara ya Mnazimmoja yaani Maisara mpaka Kikwajuni na ujenzi wa barabara ya Mitiulaya mpaka kwa Biziredi, ujenzi wa barabara ya Mitiulaya.

Mhe. Naibu Spika, pia katika bajeti ya mwaka huu pia kwenye fedha hizo 1.5 ujenzi wa barabara pia tutaufanya katika eneo la Chake Chake - Hospitali mpaka kutokezea kwenye soko la Qatar na kutokezea kwenye Uwanja wa Tibirinzi. Pia kama alivyohoji Mhe. Sulaiman Sarahani, barabara hiyo inaanza kujengwa mwezi huu. Mkandarasi ameshapatikana na ujenzi utaanza mwezi huu.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Misufini kwa Biziredi nayo vile vile itajengwa mwezi huu, Mkandarasi ameshapatikana na barabara itajengwa.

Mhe. Naibu Spika, barabara ambazo tulizozitembelea ni chache kuliko zile barabara ambazo tunataka tuzijenge kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo wale Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wametuomba na barabara zao tuzifikie, nataka niwahakikishie kwamba tukimaliza bajeti hii tutafanya *survey* kama tuliyoifanya kwa barabara ambazo tumezitaja kwenye kitabu chetu cha bajeti na hizo zitaingia katika mpango wetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba jambo hili sio kwamba tunataka tuseme hapa kwa sababu mupitishe bajeti, hapana. Waliona wiki mbili nyuma zilizopita waliniona nimekaa na Bodi ya Mfuko wa Barabara, nilikuja kujitambulisha kwangu na kutoa maoni yao na mimi kuwapa maoni yangu. Moja kati ya eneo ambalo tumelizungumza ni kuhakikisha kwamba hii bajeti ya *percentage* inaongezwa kuja kwenye Serikali za Mitaa badala ya kubaki na hii bajeti hii ya asilimia kumi na tano na mambo mengine ambayo wanayafikiria wao na moja kati ya mambo ambayo wanayafikiria wao kwamba watazingatia pia suala la nani atapa-*perform* vizuri katika hizi fedha zilizotengwa, yule ambae ata-*perform* vizuri kutakuwa na asilimia thalathini itakwenda kwa yule ambae ataweza kufanya kazi zake haraka na tutafanya kazi hiyo kwa uadilifu.

Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba barabara kama walivyotuomba tutajitahidi sana kuzifanyia kazi ili tuweze kuondosha na tuweze kujibu na kuweza kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, barabara nyingi zimetajwa, kwa mfano barabara ametaja Mhe. Hamza na wengineo wametaja barabara nyingi, lakini barabara hizo zote

tutazianza kuzifanyia kazi pamoja na zile zilizotajwa na Waheshimiwa tutafanya *evaluation* ya kwenda kuzikagua na kuona *possibility* ya kuweza kuzijenga barabara hizo. Sasa sitakwenda kwa Mheshimiwa mmoja mmoja lakini maelezo yangu ya jumla kuhusu hoja hiyo ya barabara nadhani niseme hivyo.

Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kueleza barabara ambazo nyengine haziko moja kwa moja kwangu mimi, ambazo zimeelezwa. Nadhani nakubaliana naye na Waheshimiwa Wajumbe nadhani waridhike tu na majibu ya Mhe. Naibu Waziri.

Kuhusu Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba kuwepo kwenye jengo la mtu binafsi. Ni kweli ofisi hii bado inaendelea kuwepo kwenye jengo la mtu binafsi, lakini nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba si muda mrefu kwenye mwaka ujao wa fedha tutahamia kwenye majengo yetu. Tunalo jengo la Halmashauri ya Wilaya na jengo la iliyokuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tutachagua wapi tunaweza kwenda kati ya majengo yale lakini tutaondoka kwenye jengo la mtu binafsi ili tukae kwenye majengo ya serikali.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili la ofisi limezungumzwa pia katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Hii ni changamoto kwa serikali nzima sio kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa tu hata wizara zetu. Kwa wale waliobahatika kunitembelea pale ofisini kwangu hata ile ofisi ninayoishi mimi ina vyumba visivyozidi vitano, kwa hiyo tuko katika maeneo tofauti tofauti, lakini hili kama alivyolieleza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwenye majumuisho yake siku ya kuwasilisha bajeti kuu ya serikali, kwamba serikali ina mpango madhubuti wa kuweza kujenga majengo ya serikali hatua kwa hatua kama ilivyokwisha kuanza.

Suala la gari pia limezungumzwa gari wanazopanda Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Ma-*DC* na hata Mstahiki Meya, haina hadhi. Ni kweli, magari hata wanayopanda mawaziri mengi yao yamechoka. Kwa hiyo, jambo hili litazingatiwa kwenye mpango mkuu wa serikali pale ambapo serikali itanunua magari kwa ajili ya kuwapa viongozi wake. Kwa hiyo, kupanda gari Meya ambalo imani yangu lile lina umri kama wa miaka 10 au minane ni kweli, Ma-*DC* nao magari yao, Ma-*RC*, Mawaziri ukiacha mawaziri wachache. Mimi nina gari ambalo limetumika miaka mitano na wachache wana magari ambayo hayajafika muda mkubwa na kwa nini? Kwa sababu mimi nilipoteuliwa kwa kipindi kama cha miaka miwili nilitumia gari yangu binafsi kwa sababu serikalini kulikuwa hakuna gari. Kwa hiyo, mimi nadhani cha

msingi serikali sasa hivi inaandaa utaratibu wa kuweza kupata magari kwa ajili ya viongozi wa serikali. Sasa tusubiri tu pale utakapofika muda kila mwenye haki, kila mwenye *status* ya kupanda gari gani atapewa kwa mujibu wa *status* yake, tuvumilie Waheshimiwa.

Taarifa za wakaazi wasiokuwa Wazanzibari na kusajiliwa kwao. Ni kweli sheria tuliifanyia marekebisho ya kufanya zoezi hili na kanuni nilishazisaini za kuwawezesha Wazanzibari wasio kuwa wakaazi kusajiliwa, lakini tumekwama kidogo kutokana *resources*. Tuna tatizo la *material* ya hivyo vitambulisho vyenyewe na tuna tatizo pia la kiufundi kuhusu mitambo yetu na hayo yote yanasababishwa na upungufu wa fedha hatujapata fedha. Kwa hiyo, tunatarajia kwenye bajeti hii ya mwaka tunaokwendanao mambo mengi mazito ya kitafa, kwa mfano jambo ambalo lilikuwepo sote tunajua kwamba tulilazimika kufanya uchaguzi mara mbili. Sasa kupanga ni kuchagua, ilikuwa muhimu kupeleka *funds* ili zikenda kwenye vitambulisho au kuhakikisha uchaguzi unafanyika ili sote turudi humu ndani. Nadhani sote tutakubaliana kwamba uchaguzi kufanyika ilikuwa ni jambo *very important* na ni *first priority* kwa serikali na sio kitu kingine. Kwa hiyo, hili tunakiri kuwepo kwa mapungufu hayo lakini mapungufu haya yanatokana na uwezo wa kifedha. Kuna mambo mengine ya kiutendaji nadhani nisingependa kuyasema.

Hoja nyengine ilikuwa kuwe na utaratibu wa kuangalia vijana ambao wanatimiza miaka 18 kwa kupitia wilayani ili vijana wapate wepesi wa kupata vitambulisho na zoezi hilo lifanyike kila mwaka. Utaratibu ni kwamba kila anayetaka kusajiliwa aende kwenye ofisi ya usajili ya wilaya na hili limezungumzwa na Waheshimiwa wengi, lakini utaratibu wetu ni huo na madhumuni ya kuunganisha idara au Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo na Ofisi ya Kadi ya Utambulisho ni kwamba tunataka tumsajili Mzanzibari toka siku anazaliwa mpaka siku anakufa anaingia kaburini. Kwa hiyo, yale yote ambayo wameyazungumza Waheshimiwa Wajumbe ni muhimu na ushauri wao tumeuzingatia.

Wizara itaendelea na mkakati wake wa kuelimisha wananchi kupitia programu mbali mbali kwenye *television* kuhusu umuhimu wa kuwasajili Wazanzibari kuanzia anapozaliwa mpaka anapoingia kaburini. Hapa nitoe wito kwamba tumekuwa tuna mazowea ya kusajili vizazi, Uzanzibari, lakini ni kweli wale waliosema kwamba tuna tatizo la kusajili ndoa zetu, tuna tatizo la kusajili vifo na tatizo la kusajili talaka. Haya yote ni matukio ya kijamii ambayo yanatakiwa kila yatakapofanyika kama ukishakupata ile *certificate* ya Kadhi uende Idara ya Usajili ukasajili sasa kwenye *certificate* rasmi ya ndoa, kwenye *certificate* rasmi ya talaka na kwenye *certificate* rasmi ya kifo.

Kwa hiyo, yako maeneo muhimu matano ambayo kila Mzanzibari anatakiwa afanyiwe na hayo ofisi yangu kupitia Idara ya Vizazi na Vifo na Kadi za Utambulisho itajitahidi katika kipindi hiki kuhakikisha kwamba tunayafanyia kazi vizuri na tunawaondoshea wananchi kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuboreshwa au kuimarishwa Ofisi ya Vizazi na Vifo Pemba. Hoja hii imetolewa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na wengine wamezungumzia suala hili. Nataka nimhakikishie kwamba tunatambua kuwepo kwa kasoro hiyo na tutaendelea kuiboresha kama tulivyoiboresha ofisi iliyopo hapa.

Tatizo la upotevu wa vyeti vya kuzaliwa katika Wilaya ya Kaskazini 'A' limezungumzwa na Mhe. Mtumwa. Hili jambo ni kweli lipo lakini pale muhusika anapokosa kumbukumbu katika Ofisi ya Wilaya anatakiwa aje Makao Makuu au Ofisi Kuu kumbukumbu zote pale zipo.

Hapa nataka nizungumzie na suala la Mhe. Hassan Khamis Hafidh juu ya suala la *AC* na mazingira mazuri ya *strong room* ya kuhifadhi nyaraka zetu. Ni kweli mimi baada ya kupewa jukumu hili nilifanya ziara, ni kweli hakuna *AC*, kuna matatizo kidogo ya kimalipo kati ya *Client* na mkandarasi. Kwa hiyo, *AC* pale sio kwamba haipo lakini mkandarasi hajairuhusu kwa sababu hajamaliziwa malipo yake, mara tu baada ya malipo hayo na nadhani serikali katika bajeti ya serikali iliyopita kupitia Wizara ya Fedha waliahidi kwamba suala hili watalitatua ili mkandarasi aweze kuruhusu na yale maeneo mengine. Eneo hili la *AC* na eneo la *lift* ya lile jengo. Kwa hiyo, mimi nadhani litakapokamilika hilo, hili jambo litarekebishika, lakini pia mkakati wetu sisi Mhe. Hassan Khamis ni kuhakikisha hata zile *documents* zenyewe zinakaa pahala pazuri ambapo haziwezi kuharibika. Lakini pia namna ya kuziweka zile *documents* zenyewe tutahakikisha tunaimarisha mfumo badala ya ule uliopo kuziweka.

Mhe. Naibu Spika, ukienda pale utakuta zile *document* za miaka kuanzia 1964 na zilizoanza kusajiliwa mwaka 1840 basi zile za 1840 ziko vizuri kuliko zile za miaka ya karibuni. Kwa hivyo, tunakiri kwa msingi huo mimi moja kati ya jukumu langu ni kuhakikisha kwamba hizo *documents* tunazihifadhi vizuri.

Lini mfumo unaotumia elektroniki utaweza kutumika kwa wilaya zote? Kama tulivyosema mfumo huu hili jambo lilizungumzwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Khadija Omar Kibano na wengine. Suala hili kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba limeanza kwa *pilot area* katika wilaya tatu za Mkowa Mjini Magharibi. Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi 'A' na Wilaya ya Magharibi 'B'. Sasa jambo hili linaendana na uwezo wa kifedha, pale tu ofisi

yangu itapata uwezo kifedha itahakikisha kwamba jambo hili linafanyika kwa wizara zote. Kwa sababu ndio lengo la serikali kuondosha usumbufu na kuweza kuleta ufanisi wa majukumu ambayo yamepangwa na serikali.

Kwa hiyo, utaratibu wa Sheria Nam. 10 ya Mwaka 2016 kipengele cha usajili wa watu waliochelewa, (*late registration)* utaendelea kwa mujibu wa sheria kama ilivyo sasa mpaka pale tutakapoamua kurekebisha sheria.

Idadi ya ndoa na talaka zilizo kwenye hotuba ya bajeti Mhe. Khadija Omar Kibano; idadi ya ndoa 125 na talaka 16. Hapa ukiziona kwa takwimu zetu ni kidogo na nakiri kwamba ni kidogo, lakni hizo zinatokana na utamaduni ambao tumejiwekea. Yanapofanyika haya matukio ya kijamii hatwendi kuyasajili. Kwa hiyo, naomba kutoa wito kwamba matukio haya sasa nayo yanastahiki kusajiliwa. Sisi kama ofisi, tutaendelea kutoa taaluma hiyo, lakini tukio la kifo pia linastahiki kusajiliwa.

Idara Maalum. Baadhi ya wapiganaji wa Idara Maalum wanakiuka maadili na kufanya kazi zisizowahusu, anashauri wapiganaji waelimishwe. Jambo hili lilizungumzwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Hamza Hassan Juma na wengineo. Nataka niseme wazo hili tunalichukua na tutaendelea kulifanyia kazi na pale linapotokezea jambo hili popote pale pa kuvunja maadili kwa askari ni vizuri tukaeleweshana mapema, sisemi msije kuhoji Baraza la Wawakilishi lakini mnapokuja kuhoji Barazani maana yake tatizo lake ni kwamba ninaweza nisiwe na upeo wa kuweza kulifanyia kazi kwa haraka na utaratibu wa kawaida wa kuwachukulia askari nidhmu za kisheria upo.

Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe niwaombe wale wote wanaokutana na kadhia hii linapotokezea tu tatizo hili ni vizuri ama kwangu mimi au kwa wasaidizi walio katika ofisi yetu kulieleza ama kwa Wakuu wa Vikosi ili tuweze ku-*trace* wapiganaji hawa wako katika maeneo gani ili tuweze kuwachukulia hatua za kinidhamu. Kwa sababu askari anapotoka kwenye operesheni au anapokwenda kwenye lindo anakuwa kwenye *register*. Sasa unapotwambia kwamba askari wamefanya jambo moja, mbili, mapema inakuwa rahisi na utambuzi wao unakuwa tafauti na utambuzi mwengine; unawaweka kwenye paredi la utambulisho unakuja kusema askari aliyenifanyia jambo hili ni huyu.

Kwa hiyo, anachukuliwa hatua za nidhamu kwa mujibu wa taratibu zao za kijeshi na za kiaskari zilizotandikwa kwa mujibu wa sheria zao, kanuni na Sheria ya Utumishi Idara Maalum za Serikali.

Sasa niwaombe sana Waheshimiwa tufuate wasia ule wa Mzee Ali Hassan Mwinyi kwamba yapo mambo ni vizuri tukayazungumza humu lakini yapo mambo tusiyasubiri, tuje tuyazungumze humu wakati yashaharibika, yanapoharibika marekebisho yake yanakuwa ni ya muda mrefu.

Mhe. Ali Hassan Mwinyi kwenye mwaka ule alisema kwamba: "Wawakilishi ni viongozi wa watu na tunayo haki ya kusema jambo lolote ndani ya Baraza la Wawakilishi, lakini pia Wawakilishi sio wanyapara".

Kwa msingi huo na sisi tunao wajibu wa kutoa taarifa kwa sekta husika ili kufanya kazi hii ya kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Madai kwamba wapiganaji wa Idara Maalum wanapohitimu mafunzo wengine hawapandishwi vyeo na wastaafu wa vikosi wanadai mafao ya kustaafu. Kwanza jambo la wastaafu ni utaratibu wa kawaida, sisi mstaafu yeyote wa Idara Maalum anapokwisha kustaafu kazi yetu sisi ni kuiarifu Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha kulingana na uwezo walionao wanachukua hatua ya kuweza kuwalipa mafao. Jambo hili haliko kwa taasisi nyengine yoyote ya serikali zaidi ya Wizara ya Fedha na bahati nzuri wastaafu wa Idara Maalum hawako mpaka sasa kwenye mfumo wa *ZSSF*.

Jengine madai kwamba wapiganaji wa Idara Maalum hawapandishwi vyeo pale wanaporudi. Hili jambo lilizungumzwa na Mhe Abdalla Ali Kombo na Mhe. Said Omar Said. Upo utaratibu katika Idara Maalum anaweza akapandishwa cheo mtu kutokana na tukio alilolifanya kabla ya kwenda kwenye *course* ya yale mafunzo aliyoyapata. Kwa hiyo, saa nyengine mpiganaji anaweza akenda *course* wakati ameshavalishwa cheo, anapokwenda kwenye ile *course* anakwenda kufanya kazi ya kile cheo ambacho amevalishwa na anakwenda kupata mafunzo ya kile cheo ambacho amevalishwa. Hata hivyo, Mhe. Abdalla Ali Kombo na wengine kama liko tatizo hili nawahakikishia kwamba nitalifuatilia ili tujue ukweli wa mambo ukoje na tuweze kulirekebisha. Lakini kwa utaratibu wetu ulivyo sasa hivi ndio hali halisi ilivyo.

Ajira za vikosi hazizingatii vijana waliopata mafunzo JKU na JKT. Wajumbe wengi wameshauri ajira katika vyombo vya ulinzi wapewe vipaumbele hawa watu ambao wanakwenda kwenye vikosi vyetu hivi viwili JKT na JKU. Jambo hili lilizungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa wengi katika michango yao.

Kwanza ushauri wa Waheshimiwa Wawakilishi ndio ushauri ambao umeagizwa na serikali zetu zote mbili na ndio ambao sasa tutaanza kuufanyia kazi.

Hapa nataka niunganishe hata hili suala la JKT kuna waheshimiwa wanasema hawajui lolote. Ni kweli nafasi za kwenda JKT zimekuja na sisi tumezigawa katika mikoa na wilaya na tuliwapa kabisa Wakuu wa Mikoa. Mimi mwenyewe binafsi niliwapa Wakuu wa Mikoa ukiacha wale wa Pemba ndio tulipeleka kwa utaratibu wa njia ya kutuma, lakini wale Wakuu wa Mikoa wa Unguja niliwaita ofisini kwangu nikawasomea masharti ya zile nafasi na ni imani yangu kwamba watakuwa wamefanya hivyo.

Kwa bahati mbaya kama watakuwa hawajafanya hivyo basi wale watu wa JKT watakapokuja kwa sababu itabidi wasome na ule muongozo wao walioutoa kwamba watu hawa wanatakiwa watoke vijijini na maeneo husika ya kila Wilaya na Mkoa. Lakini akiwa hawezi kwenda kwenye JKT kujitolea hawezi kutoka JKU. Kwa sababu JKU na JKT ni kitu kimoja kule wanajenga Taifa na huku wanajenga Taifa na moja kati ya masharti ya hawa vijana wanaokwenda JKT hakuna mkataba wa kwamba lazima wapate ajira kule. Lakini wanaweza wakapata fursa ya kuajiriwa iwapo watakuwa wanavigezo vinavyostahiki kuajiriwa kwa zile nafasi ambazo zitapelewekwa na Vikosi vya Ulinzi na Usalama.

Vikosi vya Ulinzi na Usalama, Jeshi, Polisi, Usalama wa Taifa, Uhamiaji na wengineo wana vigenzo vyao vya kuwaajiri watu. Kwa hiyo, wanaweza wakabahatika fursa hiyo ya kuajiriwa, wanaweza wasipate fursa ya kuajiriwa na lengo la kuwapeleka vijana katika makambi yetu ni kuwapatia ujuzi wa kujiendeleza katika maisha yao. Kwa hiyo, anaweza wakawa wamepata ujuzi na wakaajiriwa na wanaweza wakawa wamepata ujuzi na wasiajiriwe. Hakuna mkataba kwamba lazima unapokwenda kule uajiriwe, kwa sababu ajira zote zina vigezo na watu gani wanatakiwa kwenda ni kuanzia darasa la 7.

Kwa hiyo, kama wenzetu kwa kule darasa la 7 Watanzania Bara wana-*qualify* maana yake wanaomaliza darasa la 10 pia wana-*qualify* kujiunga na kambi zetu. Lakini hakuna kigezo kwamba kila anaekwenda Kambini aajiriwe, ile ni fursa tu anaweza akaajiriwa na kila akiwa na kigezo cha elimu anaajirika haraka katika hizo taasisi kuliko yule anaekuwa hana elimu.

Nadhani Waheshimiwa Wajumbe katika eneo hili itabidi tuelewane vizuri. Lakini serikali maamuzi yake kwamba zinapotoka nafasi hizi wazingatiwe waliokwenda JKT na JKU. Kwa nini, kwa sababu hawa ambao watakuwa tayari wamekwenda JKU na JKT ndio ambao watakuwa watapunguza hata muda wa mafunzo ya awali ya ule uaskari wenyewe.

Kwa hiyo, imani yangu Waheshimiwa eneo hili mtakuwa mmelisikia. Sasa kama kuna mtu atakuwa amefanya vyenginevyo mimi nadhani tuacheni tu, tuaminini tufatilie ili tujue huyo aliefanya hivyo nani. Lakini *conditions* zipo na hakika Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa watakuwa wamefata masharti hayo.

Hoja nyengine ilikuwa ni mrundikano wa vijana waliomaliza mafunzo ya JKT na JKU, ni kweli hili limezungumzwa na Wahehimiwa wengi katika Baraza hili sina haja ya kuwataja. Lakini inatokana na huo utaratibu wa kwenda JKU na JKT sio lazima aajiriwe, akeshakutoka kama fursa ipo ataajiriwa kama fursa hakuna hataajiriwa. Kuna suala pia nilichomeke hapa hapa niliulizwa katika kipindi cha miaka 5 tuliajiri mara ngapi vijana Idara Maalum. Kwenye bajeti ya mwaka 2012/13 tuliajiri vijana na hatujaajiri vijana wengine tena katika kipindi chote hicho.

Suala pia aliliuliza Mhe. Yussuf Hassan Idd ni kwa nini vijana waliotaka kuajiriwa kipindi kingine kilichopita nafikiri ilikuwa mwaka 2014/15 ni kweli tulisitisha zoezi lile na tulisitisha kwa nia njema kabisa. Tulitangaza nafasi zilikuwa elfu moja waliomba nafasi walikuwa ni kumi na tano elfu mpaka kumi na sita elfu. Bado tu malalamiko yangeendelea kuwepo. Kwa hiyo, busara ya serikali ikaonesha tuipe nafasi serikali itafute nafasi nyingi zaidi kuliko zile elfu moja ili tutakapoajiri angalau tufike angalau asilimia ishirini au thalathini ya wale ambao watakuwa na vigezo na wana sifa na idadi ya wale ambao wameajiriwa.

Kwa hiyo, kilichotusababisha tusitishe ni busara tu na hata juzi Tume ya Utumishi imetoa nafasi za mapengo kwa Idara Maalum kama mia nne. Kwa taarifa yenu nimesitisha zoezi hilo. Kama hoja yetu ile ya mwanzo ipo ina maana haiwezi kuondoka kwa nafasi hizi mia nne na malalamiko Waheshimiwa Wajumbe mngekuja kunipa hapa. Kwa hiyo, busara ya serikali tumeamua tusitishe tuisubiri serikali ipate uwezo wa kuongeza hizi nafasi ili tuweze kuajiri watu wengi zaidi. (*Makofi*)

Kufuatia kupitishwa kwa sheria ya Uwakala wa Ulinzi Mhe. Yussuf Hassan Idd na Waheshimiwa wengine walieleza ni kweli sheria ya uwakala wa ulinzi imepitishwa na imeshasainiwa hivi sasa maelezo tuliyoyaeleza kwenye kitabu chetu cha Bajeti na bajeti imeonesha ni kwamba tunataka kuanzisha hicho kikosi cha ulinzi na napenda niwafahamishe Waheshimiwa kwamba tutakapoanzisha kikosi hiki kwenye bajeti ya mwaka huu hakuna askari au kikosi chochote kitakachoruhusiwa kupeleka askari wake kwenye malindo ya kibiashara.

Kikosi hichi cha Ulinzi cha JKU ndicho kitakachokuwa kinafanyakazi ya kufanya ulinzi kwenye maeneo yote ya uwekezaji, maeneo ya utalii, maeneo ya makampuni mbali mbali. Kwa hiyo, askari wote wanaolinda kwenye vituo mbali mbali sasa watarudi makambini na kufanya kazi zao za nchi katika kuilinda nchi na kufanya kazi nyengine ambazo atapangiwa na serikali au na wakuu wao wa taasisi.

Kambi ya JKU Mwambe Mhe. Mussa Foum, hali yake si mzuri, tunatambua hilo na hapa nataka nizungumzie pia walilolizungumza Waheshimiwa wengi kuhusu makaazi ya askari na mazingira yao. Tunakiri kwamba makaazi ya askari na mazingira yao hayaridhishi hata kidogo na kwa kupitia bajeti hizi za serikali tunaweza tusifikie pahala kwa sababu bajeti zinakuwa zina ukomo wake. Kwa hiyo, pale kikosi kinapopata nafasi ya uzalishaji kwenye eneo lake ndio kinajaribu kuweza kufanya ukarabati na kuweza kujenga majengo mengine kupitia zile *resources* ambazo wanazipata kwenye *revenue* zao. Hapa nataka niunganishe kwamba zile *revenue* ambazo wanakushanya vikosi wameruhusiwa rasmi na serikali kuzitumia katika maeneo hayo ya kujisadia badala ya kusubiri peke yake ile ya kukisiwa ambayo inatoka serikalini.

Kwa hiyo, maeneo mengi ya askari makazi yao ni kweli ni hafifu tunalitambua hilo serikali. Lakini nawaomba Waheshimiwa Wajumbe watuvumilie na sisi huku wizarani tuna mpango mzima wa kuhakikisha kwamba tunapata nyenzo za kuweza kuyafanyia kazi, maeneo haya na pale tutakapopata uwezo basi lile tatizo litaondoka.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa nini mapato ya mifugo au Mhe. Hamza Hassan Juma hayakuoneshwa. Imetokana na kupungua kwa idadi ya mifugo ikiwemo na kuzongwa na maradhi. Lakini mapato kwa jumla yanayotakiwa tuwasilishe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, ni yale ambayo tumeyaonesha kwenye hotuba ya bajeti yetu. Lakini kwenye maeneo ya Idara Maalum mapato hayo wanayakusanya na wanajua wenyewe wanavyoatumia. Utaratibu upo wa kisheria wa kamati inayohusika kwenda kufatilia matumizi hayo na utaratibu wa kawaida kwa mujibu wa katiba, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anayo haki ya kwenda kufatilia masuala hayo na ukishafatilia maana yake ripoti hiyo italetwa hapa, ikishakuletwa hapa kamati ya *PAC* itakabidhiwa na kamati ya *PAC* itakwenda na itakuja kutupa taarifa. Wajumbe sasa tutakuwa na uwezo wa kuweza kutaka tupewe ufafanuzi zaidi juu ya hoja ambazo kamati ya *PAC* kama haikuridhika, ili tuweze kutoa ufafanuzi zaidi.

Kama nilivyosema wengi wamesema kuhusu nyumba za watumishi haziridhishi, nataka nikubaliane nao kwa asilimia mia moja lakini kwa pale

ambapo tunapata nafasi hiyo basi tunajitahidi sana kupitia yale mapato ambayo vikosi vina uzalishaji mali na kwa kupitia fedha hizo basi wanajenga hizo nyumba. Je, tunao utaratibu wa kuwafatilia wanafunzi wanapomaliza muda wao. Kwa hivi, sasa hatujawa na utaratibu huo isipokuwa Chuo cha Mafunzo kwa kushirikiana na Ustawi wa Jamii na Asasi za Kiraia hasa *Red Cross* tumeanza kuandaa huu mpango na pengine tunaweza tuufanye ili tufatilie zile tabia za wanafunzi wanapotoka vyuoni.

Kuhusu magodoro ya wanafunzi kuchakaa haraka na mpango wa kuwapatia vitanda wanafunzi. Suala hili limeletwa na Mhe. Ali Salum Haji ni mpango mzuri lakini kutokana na mfumo na muundo wa Magereza yetu inatuwia ugumu kidogo kwa sababu nafasi zile mimi nakukaribisheni Waheshimiwa Wajumbe, Waheshimiwa ni moja kati ya Wajumbe ambao viongozi wametajwa ndani ya sheria kwamba wanao uwezo wa kuweza kutembelea Vyuo vya Mafunzo saa yoyote. Kwa hiyo, niwakaribishe mwende mkajionee yale mazingira.

Hata hivyo ushauri tunaupokea na tunaufanyia kazi hasa katika kile jengo la Chuo cha Mafunzo tutakalolianza sasa tutazingatia kuwa na nafasi kubwa, ili iweze kukidhi haja ya kuwa kuweka vitanda baada ya kuweka magodoro matupu kwa sababu jambo hilo ni zuri na Taasisi za haki za Binaadamu zinatuhimiza kufanya hivyo. Kwa hiyo, pale tutakapopata uwezo tutafanya hivyo.

Suala la wafungwa kutemebelewa na jamaa zao. Hili jambo lilizungumzwa na Mhe. Suleiman Sarahan, fursa ya wanafunzi kutembelewa na jamaa zao ipo, fursa ipo lakini ule utaratibu mwengine uliopendekeza ule bado haupo. Isipokuwa ushauri tunauchukuwa tupate uzoefu wa nchi nyengine ili kama unaleta manufaa basi tutautekeleza. Kwa hiyo, ushauri wako tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Ujenzi wa Chuo kipya Hanyegwa Mchana amezungumza Mhe. Ali Salim Haji na wengine. Idara inaendelea na hatua ya ukamilishaji wa ujenzi wa ukuta kwa mwaka huu wa fedha na kwa mwaka ujao wa fedha tunatarajia na ujezi wa Gereza la Watoto *juvenile* kama alivyouliza Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi). Utaratibu wa sasa wa *juvenile* tumetenga eneo karibu na eneo la jengo la wanafunzi, kina mama tumewaka huko. Kwa hiyo, sasa hivi wanafunzi *juvenile* hawakai tena huku kwa upande wetu sisi. Kwa sababu tulikuwa tunaona na mimi nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria tuliona hiyo athari ambayo Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) ameisema na ndio maana katika bajeti ijayo tumeamua kwenye eneo la Hanyegwa Mchana,

tuanze na ujenzi wa jengo la Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kuwahifadhi watoto kwa sababu ya kutaka wasiendelee kuharibika kisaikolojia na mambo mengine.

Mafunzo gani wanayopatiwa wanafunzi wanapokuwa chuoni. Mafunzo wanayopatiwa wanafunzi wanapokuwa chuoni ni yale mafunzo ya ujasiriamali, useremala, uwashi, stadi za kilimo na mifugo, ushoni na kazi za amali pamoja na elimu ya watu wazima kwa wale wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika. Hizi ndizo stadi ambazo tunawapatia wanafunzi wanaokuwepo kule kwenye Vyuo vya Mafunzo.

Ukosefu wa huduma za maji na umeme hatua za uchimbaji wa kisima hili lilizungumzwa na Mhe. Ame Haji Ame, nadhani hatua za uchimbaji wa kisima zilikwisha fanyika na tayari yanapatika na suala la umeme hatua zilizochukuliwa ni uwekaji wa *solar* kwa ajili ya mawasiliano huku mchakato wa kutafuta umeme unaendelea.

Nadhani Mhe. Ame Haji Ame alizungumzia kuhusu kituo cha Kibwengo. Kwa hiyo, hizo ndizo hatua ambazo tumezichukuwa kwamba kwa dharura tumechimba kisima na tayari tumeweka *solar* kwa kuanzia. Lakini suala la umeme tunaendelea nalo ili na wao waweze kufaidika na jambo hili.

Mhe. Asha Abdalla na Mhe. Yussuf Hassan KMKM ni watu wangapi ambao wamepatikana na kuleta magendo na kesi ngapi zimeshughulikiwa. Hakuna watu waliokamatwa wala kesi inayoshughulikiwa kutokana na watuhimuwa kukimbia mzigo wao na kubaki kuwa ni mali ya kuokota kwa mujibu wa sheria ya jinai. Hawa watu wamekuwa ni wajanja sana wanapopata taarifa na wanapoona kwamba tayari kuna njia za kuweza kuwakamatwa wanatelekeza mizingo yao na wanaondoka. Kwa hiyo, tunachofanya sisi bidhaa iliyokamatwa tunaipeleka kwenye taasisi inayohusika kwa mfano karafuu tunazipeleka ZSTC bidhaa nyengine tunazipeleka kwa taasisi nyengine na tunazikabidhi kwa *TRA* na *ZRB* ili waweze kuziuza na kupata kodi zetu.

Kambi ya KMKM Msuka imezungumziwa hii na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Shamata Shaame Khamis. Ni kweli mmommonyoko katika maeneo huchukuwa hatua ya kupanda miti ya mivinje ili kuzuia mmommonyoko huo.

Kuhusu suala la usafiri karibu vituo vyetu vyote tutaweka mkakati madhubuti wa kuweza kupata usafiri ama uwe wa baharini na uwe wa nchi kavu kwa ajili ya kupunguzia pale inapotokea dharura. Kwa hivi sasa utaratibu uliopo ni kwamba inapotokea dharura yoyote taarifa inapelekwa kwenye Afisi ya Makao

Makuu wa *zone* jambo ambalo si sahihi sana. Lakini hili linatokana na uwezo pale tutakapopata uwezo basi sisi tunatamani kuwapatia walinzi wetu kila kinachostahiki wao kukipata na kama mnavyojua Waheshimiwa Wajumbe katika eneo hili ni eneo gumu sana kuweza kupata msaada. Kwa hiyo, mimi nadhani pale ambapo tutapata fedha nzuri basi tutaweza kuchukuwa hatua.

Mhe. Hidaya Ali Makame KMKM kazi zake ni kuzuia magendo yasitokea au kuingia kwa magendo. Kazi ya KMKM ni kuzuia na inapobidi kukamata yawe yanaingia yawe yanatoka. Hilo ndilo jukumu la msingi la KMKM na tutafurahi sana tukipata na tumefurahi sana kupata hii taarifa ya Bandari ya Nungwi sisi tunajua kwamba kama nilivyoelezwa na Wajumbe wengi kwamba tunayo changamoto ya Bandari bubu. Sasa changamoto hii tutaitatua kwa kukaa na taasisi zote zinazohusika tuweke mikakati madhubuti pamoja na wananchi waliopo katika maeno ili tuone tunakabiliana vipi na changamoto hii.

Ushauri wa kituo cha Uokozi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha ufafanuzi ameutoa kwamba Zanzibar tunatarajia kujenga vituo kumi vya uokozi kwa mpango wa awali. Hivi vituo vilipangwa katika kila Wilaya. Lakini sasa tuna Wilaya kumi na moja. Je, vinabakia kumi? Hilo ni jambo ambalo litakuja kwenye mipango ya baadae. (*Makofi*)

Katika mpango wa serikali kila Wilaya tunahitaji kuwa na kituo kimoja na kama alivyokusema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kuanzia tunaanza na vitano. Kimoja tayari kimeshakamilika pale KMKM. Chengine kinaendelea kujengwa Mkoani. Chengine kitajengwa Nungwi na chengine kitajengwa Wete na chengine kitajengwa Kizimkazi. (*Makofi*)

Vituo vitano vitakuwa vimekamilika na vyengine tutavijenga kwa kuzingatia maeneo ambayo tunahisi haya ikitokea ajali kama walivyosema Waheshimiwa wengi, ama iwe ya vyombo vile vikubwa na vile vyombo vidogo vidogo vya wavuvi. Kwa sababu nchi yetu ni nchi ya visiwa, basi serikali kila tutakapopata uwezo tutajenga. Na vituo hivi tunavijenga na boti zao tano tayari katika bajeti ijayo tutavinunua kwa ajili ya uokozi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ukichanganya na zile boti ambazo amezitaja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambazo zipo katika *component* ya mradi ule wa Mji Salama au ya masuala ya ulinzi ambazo zinajulikana kwa jina la *interceptor* ambazo zinakwenda *speed* hiyo *nautical miles 60* kwa saa. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba tutakuwa na uwezo wa kumfukuza yeyote ambae itakuwa tumegundua au tumepata taarifa pahala alipo. Na boti hizo tatu zitakapokuja; moja tutaiweka Kisiwani Pemba na mbili zitakuwepo Unguja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na kadiri tutakavyopata hizi boti na hizi boti hizi za *interceptor* tunataka nazo kila Wilaya ziwe na boti moja ili kuhakikisha kwamba tunajilinda vizuri na kukabiliana na mambo yote ambayo ya kimagendo na ya uharamia. Kwa hivyo ushauri wake ni mzuri na sisi tayari Ofisi yangu kwa kushirikiana na Kikosi cha KMKM tumeshaanza kuufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuongeza ulinzi katika ukanda wa Micheweni Mhe. Bihindi Hamadi Khamis. Tunapokea ushauri wake. Hivi sasa ulinzi upo na tutaendelea kuimarisha hasa baada ya kupata taarifa hizo ambazo ametwambia hapa au ametushauri.

Mhe. Naibu Spika, suala la KMKM kupatiwa nyenzo za kisasa za kufanyia doria, zikiwemo boti za kisasa na mafuta. Jambo hili lilizungumzwa na Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Ame Haji Ali, Mhe. Shehe Hamad Mattar na Waheshimiwa wengi wengineo. Kama nilivyokwisha kusema kwamba juhudi hii sasa tumeanza kuichukua ili kuhakikisha kwamba tunawatafutia vifaa na vitendea kazi ili kuweza kumudu kazi zao vyema kama tulivyowataka na kwa mujibu wa sheria yao inavyozungumza.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu nambari za askari zilitolewa. Hizi namba zilitolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma. Kwanza mimi nimuombe sana ndugu yangu au kaka yangu Mhe. Hamza kwamba suala za namba za askari…

Mhe. Hamza nisikilize! (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninataka niseme kwamba jambo hili nimelipokea na kama nilivyosema mwanzo kwamba umenipa hapa na pengine kwa maadili na taratibu na sheria za Idara Maalum, siwezi kuchukua hatua hapa na kukupa jibu ya kadhia hii. Lakini ninalichukua nitalifanyia kazi na tutakwita kwa kusaidia taarifa hizi ulipozipata kwanza. Kwa sababu taarifa za namba za askari ni siri. Ndiyo maana utaona hawa ni tofauti na Polisi. Polisi namba zao zinatakiwa ziwe wazi, kwa sababu hawa ni watu waliopo kwa wananchi moja kwa moja. Hawa askari wa Idara Maalum wana *elements* za kijeshi. Kwa hivyo haitakiwi kitu chao chochote kile kuwekwa hadharani. (*Makofi*)

Kwa hivyo taarifa mheshimiwa tutakwita ili utupe, tujue kadhia, kama kuna makosa yamefanyika. Kwa yeyote aliyehusika na makosa ambayo wamekufanya wewe utaje namba hizi tutashirikiana ili tuweze kuyafikisha katika taasisi zinazohusika na waweze kuchukuliwa hatua kisheria. Lakini kwa

hapa Mhe. Hamza ndugu yangu, Mtumbatu wa juu. Maana wewe unatoka kule Chaani. Saa nyengine huniita mwalimu wangu. Nikuombe sana jambo hili tutakutafuta ili utupe taarifa. Si kwa nia mbaya lakini utupe taarifa ili tujue kadhia imetokana na nini ili kama kuna mtu kakosea tuweze kumchukulia hatua za kinidhamu na kisheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu makusanyo ambayo umetaka maelezo. Kuhusu mapato ya Fungu D 06 kwa 2015/2016 makusanyo kwa miezi ni bilioni tano na laki sita na siyo bilioni saba. Sasa kama imejitokeza kwenye kitabu Mhe. Hamza.

Mimi naomba sana Waheshimiwa tunaposema mutusikilize *otherwise* labda iwe buti ni *fashions*. Lakini tunapotoa majibu naomba mutusikilize ili unapokuja kupiga buti upige buti ya uhakika kwa jambo ambalo hujaridhika na majibu au sijayajibu. Lakini kwa lile jibu ambalo nitakuwa nimelitolea ufafanuzi, mimi ninadhani utaratibu, itabidi tufuate, Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo ninakuomba sana ndugu yangu Mhe. Hamza kwa sababu ninatoa majibu yanayokuhusu wewe na umeweka msisitizo tukujibu. Ndiyo maana pale ulipoleta hoja kwamba unataka muda wa uchangiaji uongezeke. Serikali tulikubali na ndiyo maana tumekwenda kukaa kutafakari. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hesabu inayoonekana hapo kutoka makadirio ya bilioni kumi na saba, laki sita na sita, kwa mwaka ujao wa makadirio ya makusanyo ni ishirini na moja bilioni thamanini na nne elfu ambayo yamepelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kuhusu mapato mengine yanatumika katika kugharamia shughuli mbali mbali za fungu hilo.

Aidha, pesa wanazochangishwa askari kama ulivyosema. Hizi ni tuhuma. Hivyo naomba unipe muda niweze kuthibitisha. Gari hiyo namba uliyosema. Gari hili limenunuliwa katika *yard* kwa kufuata utaratibu wa Kiserikali.

Kuhusu wafanyakazi wanne wanaofanya kazi nje ya kikosi. Huu ni utaratibu wa kawaida wa kikosi chochote kile askari kupangiwa kazi sehemu kwa mujibu wa utaratibu wa kikosi. Hata hivyo kama kuna ukiukwaji wa taratibu. Tunaomba mashirikiano yako ili tuweze kulichunguza. Nipo tayari kushirikiana na wewe Mhe. Hamza katika kujua kadhia hizi zote mbili nilizozisema. Kwa sababu nia yetu ni kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kufuata utawala bora. Sasa kama kuna mambo yamekiukwa na watendaji ama wapiganaji wenyewe. Ni vizuri tukapeana muda wa kuangalia tuhuma ili tuweze kuzifanyia kazi na tuchukue hatua kisheria.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine la Mhe. Bihind Hamad Khamis kuhusu KVZ ilipatiwa kiwanja huko Pemba lakini muda vipi. Ni kweli suala la kiwanja cha Micheweni limepatikana na sasa hivi KVZ imeshajenga mpaka kufikia ngazi ya *linter*. Kwa hivyo mwaka ujao wa fedha tutaona ni kiasi gani tunaweza kuliendeleza lile jengo ili kasoro iliopo katika eneo la Micheweni kukosa kituo cha Valantia tuweze kuliondosha.

Mhe. Naibu Spika, suala la makaazi ya Zimamoto na Uokozi Mkoani hayaridhishi na maeneo mengine ya Wete na kwengineko, hili limezungumzwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo. Ni kweli jambo hili tunalijua na sisi tutajitahidi kadiri iwezekanavyo pale tunapopata nafasi ya bajeti tuweze kuwajengea mazingira kama nilivyokwisha kusema. Na jambo hili linafanywa kwanza kwa kuhakikisha kwamba maeneo yote ya wapiganaji yanapimwa na yanakuwa na hati miliki.

Kuongeza huduma za Zimamoto na Uokozi. Kama nilivyosema mwanzo Mhe.Naibu Spika, Wajumbe wengi wamelisemea hili. Kikosi kimeshapata hati miliki ya eneo hilo na tayari kimeshalipa fidia kwa vipando vya wananchi waliokuwa wakitumia eneo hilo. Tunapokea ushauri wenu na tutachukua juhudi za kuanza kutoa huduma za Zimamoto na Uokozi pale ambapo tutahakikisha hata kama hatujajenga hicho kituo, lakini pale huduma ya Zimamoto na Uokozi itakapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la vifaa chakavu limezungumzwa. Tunakubaliana nalo kwamba kikosi kishaanza kufanya manunuzi ya vifaa vipya ya kuzimia. Nadhani hili lilizungumzwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na wengine wengi. Wapiganaji lakini limeruhusiwa na serikali kununua magari yaliyotumika kutokana na ufinyu wa bajeti tuliyonayo. Hata hivyo kupitia hadhara hii ninataka niseme kwamba kupitia mradi ule wa ujenzi wa uwanja wa ndege na kupitia fedha za *World Bank*, kuna magari mawili ambayo yatanunuliwa mapya kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. (*Makofi*)

Mradi huu *CCTV*, tuna magari manne mapya, tutakapoyanunua kupitia mradi huu wa Miji Salama na Nchi Salama. Kwa hivyo na kadiri pale serikali itakapopata uwezo basi tutaendeleza huduma hizi. Magari mengine haya tunapewa msaada, haya *recondition*. Kwa mfano juzi tumepokea msaada wa gari tatu kutoka Japan na gari la nne tumeshaambiwa lipo Dar es Salaam. Tunasubiri tukamilishe taratibu ili tukalichukue lile gari tuweze kulipeleka Pemba. Ni gari ambalo lina uwezo mkubwa wa kuweza kufanya kazi ya zimamoto. Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe tutajaribu

kushughulikia upatikanaji wa vitendea kazi kwa wapiganaji wetu kila pale ambapo tunapata uwezo wa kuweza kufanya hivyo unafanyika. (*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika, kuhusu kutambuliwa kwa namba ya zimamoto. Mhe. Simai Mohammed Said. Namba ipo na Kikosi cha Zima Moto na Uokozi kimekuwa kikitoa mara kwa mara pale wanapopata nafasi ya kuweza kutoa taaluma kwenye vipindi vya redio, televisheni na hata vipeperushi. Hata hivyo ushauri wako ni mzuri tunaupokea na tutazidi kuzidisha kasi ya kuweza kutoa taaluma ili hii namba 114 iweze kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, umeeleza pia suala la wapiganaji wetu wa Zima Moto na Uokozi kutokutambua mitaa. Ninataka nikuhakikishie kwamba utaalamu maalum, mafunzo maalum yanatolewa *topographic* kwa ajili ya kuelimisha wapiganaji wetu waweze kuzijua njia za maeneo ya Mji Mkongwe na mengine. Kinachotukwaza kwenye maeneo ya Mji Mkongwe ni suala la kuekewa vizuizi. Saa nyengine inatupa taabu kuweza kufikia ile huduma kwa haraka lakini pia uwembamba wa njia zenyewe kimaumbile na kwa mujibu wa uhifadhi na ujenzi wa majengo yale inawapa shida. Hata hivyo ushauri wako tutauchukua na tutakwenda tuone sasa katika hayo maeneo ni maeneo gani pamoja na mafunzo tunayotoa ili tuzidi kuwaelimisha wapiganaji wetu waweze kuyaelewa vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri umeanza tangu saa kumi na moja na dakika arobaini. Naomba kidogo uongeze au ujaribu ku-*summarize* hoja zako. Lakini jengine nimeona una-*address* moja kwa moja Waheshimiwa Wajumbe badala kupitia kwangu. Sijasikia hata jina langu kusema Naibu Spika. (*Makofi*)

Kwa hivyo ninakuomba Mhe. Waziri ufanye hivyo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe.Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunikumbusha. Hii inatokana na hoja ninavyotaka zieleweke kwa Wajumbe. Ndiyo maana saa nyengine ninajisahau, ninawa-*address* Wajumbe badala ya ku-*address* kwako. Kwa hivyo naomba radhi kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sababu za kushuka kwa mapato ya Halmashauri na baadhi ya Mabaraza ya Miji. Hili jambo lilielezwa na Mhe. Machano Othman Said na baadhi ya Waheshimiwa wengine.

Mhe. Naibu Spika, yapo maeneo ambayo mapato mpaka mwezi wa Machi yamekusanywa vizuri. Lakini hasa kwenye Halmashauri na Mabaraza ya Pemba lipo tatizo. Nakiri kwamba upungufu huo upo na sisi kazi yetu ni kuweka mkakati wa kuhakikisha kwamba pengo hilo tunaliziba. Hii taarifa ni ya kutoka Julai mpaka Machi. Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba katika kipindi hiki tutakuwa ongezeko hili la mapato, litakuwa limekwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kupitia fedha zilizotengwa katika Programu ya Kuratibu za Maendeleo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Jambo hili lilizungumzwa Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Shehe Hamad Mattar. Fedha zilizotengwa si kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo kwa miradi ya kisekta. Na fedha hizo nyengine pia katika fungu hilo ni kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama na masuala mengine ya kijamii. Kwa hivyo siyo pesa hasa ambazo zimetengwa kwa kutekelezwa miradi lakini kwa sababu kama munavyojua Sheria Nam. 8 ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sheria Nam. 7 ya Serikali za Mitaa. Jukumu la msingi la Ofisi ya Mkoa ni kuratibu shughuli zote za serikali ndani ya mkoa ule na kufuatilia utekelezaji wake.

Sheria hii imetutaka kuondoka na ule utamaduni wa zamani. Sheria hii inawataka Wakuu wa Mikoa sasa kwenye sekta zote na hata wale Maafisa watakaopelekwa katika sekta husika kwenye Mikoa, badala ya kuripoti kwa Makatibu Wakuu, wanatakiwa sasa waripoti kwa Wakuu wa Mikoa. Kwa hivyo utaratibu huu ndiyo umeweka sasa utaratibu wa ufuatiliaji wa hii miradi na siyo suala la utekelezaji wa kujenga ile miradi yenyewe Mhe. Naibu Spika.

Suala la uimarishaji wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya nimeshazisema, sina haja ya kurejea. Madiwani hawajalipwa posho zao. Ni kweli na hili ninataka niliunganishe pamoja na yale maelezo ya Waheshimiwa wengi ambao wamelizungumzia suala hili la kwa nini Madiwani hawajaanza kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, tukumbuke Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Madiwani wanakula viapo viwili. Wanakula kiapo cha kuitumikia Wadi yake. Ninapenda niliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Madiwani wote wameshakula viapo vya kuzitumia Wadi zao. Sasa hili halisubiri utaratibu mwengine na ndiyo tuliwaapisha. Lakini wanakula kiapo pia kwa kutumikia Mabaraza yao ya Halmashauri, Mabaraza ya Manispaa na Mabaraza ya Mji.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli jambo hili halijafanyika.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini halijafanyika. Kwa sababu kuna mabadiliko ya muundo wa Halmashauri na Mabaraza. Mabadiliko haya yalihitaji *instruments*, yaani *legal notes* kisheria ziweze kutangazwa kwenye gazeti rasmi la serikali. Ili huo uongozi uweze kupatikana, ni vizuri Mstahiki Meya wa Mji wa Unguja, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Magharibi A na Magharibi B anapoomba uongozi basi aelewe anaomba uongozi kupitia taasisi ipi kwa mujibu wa sheria.

Kwa hivyo, ucheleweshaji wa kuanza kazi kwa Halmashauri umesababishwa na kukamilisha taratibu za kisheria na kwa msingi huo, suala la kuchelewa halipunguzi hata kidogo utendaji wao madiwani, watakapofika kwenye mabaraza baada ya kula kiapo kutumikia mabaraza yao, majukumu yao yote waliyopanga, hata uidhinishaji wa miradi wataufanya wenyewe na wala sio wizara na wala sio serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu wa sasa kwa mujibu wa sheria kutakuwa kuna Kamati ya Maendeleo ya Sheha ya Shehia, Kamati ya Wadi ambayo inaongozwa na Mhe. Diwani. Wakimaliza pale mambo yale yanakwenda kwenye Baraza la mamlaka husika au Halmashauri au Manispaa. Maamuzi yale yakitoka pale yanakwenda kwenye Kamati ya *RDC*, Kamati ya Maendeleo ya Mkoa ambayo inaongozwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa. Sasa suala hili sio suala la kwamba serikali itakuwa inaingilia majukumu yao. Ni utaratibu wa kisheria wa utekelezaji wa madaraka ya wananchi kutoka ngazi za chini kwenda ngazi za juu. Pale *RDC* Waheshimiwa Wajumbe, sote wa Baraza la Wawakilishi ni wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, kuna swali niliulizwa nafikiri na Mhe. Ame Haji Ali, sisi tunahusikaje? Tutahusika baada ya madiwani kuamua mambo yao ya kuyatekeleza, tunakuja kuyaleta kwenye kamati zile za maendeleo za Mikoa na mipango ile sasa inakwenda kwenye ngazi ya juu taifa kwa ajili ya kushughulikiwa na kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa ile miradi. Kwa ile miradi ambayo moja kwa moja Halmashauri wana uwezo wa kuitekeleza ile *RDC* inaamua pale pale ile miradi waende wakaitekeleze, ndio utaratibu.

Kwa hivyo, kuna mabadiliko makubwa katika ugatuzi huu ambao umeulizwa, ugatuzi wa Madaraka Mikoani na Wilayani katika sheria hizi mbili, Sheria Nam. 7 ya Serikali za Mitaa na Sheria Nam. 8 ya Serikali za Mikoa.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wapate na wainunuwe ile sheria na waisome vizuri ili tuweze kutekeleza majukumu yetu vizuri. Lengo ni kupeleka madaraka kwa wananchi wenyewe na wananchi wanasimamiwa na hayo Mabaraza ya Sheha, Mabaraza ya Madiwani, Kamati hizo za Maendeleo

za Mikoa ambazo sisi wawakilishi wa wananchi tumo na wabunge kama wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, utanivumilia kwa sababu hoja zilikua nyingi, inabidi nizitolee ufafanuzi. Mimi niko tayari nijibu hoja hizi, vyenginevyo, nisikilize kauli yako kama unaniambia *stop* niache. Lakini sasa nitakapofika hapa unilinde vile vile kwa buti kwa wale ambao nitakuwa sikuwajibu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ushauri katika kuziwezesha *SACCOS*. Tunaupokea ushauri ambao ulitolewa na Mhe. Bihindi, kupitia Halmashauri za Wilaya tutaifanya hiyo kazi, hasa kwa kutoa taaluma. Pale ambapo Halmashauri zitakuwa na uwezo wa kuweza kuzisaidia *SACCOS* hizo kwa mujibu wa bajeti zao tutafanya hivyo. Lakini kama Halmashauri hazina uwezo basi mifuko iliyowekwa kisheria itasajihisha *SACCOS* hizi ziweze kwenda kupata *fund* kwa ajili ya utekelezaji wao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa bandari bubu. Tayari nimeshalitolea maelezo, serikali itaweka mkakati maalum kwa kushirikiana na taasisi husika, jambo hili lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, sitaki niwataje mmoja mmoja, lakini ni wengi kila aliyelizungumza kwa kuokoa muda basi naomba aelewe kwamba serikali itaweka mkakati na tunashukuru sana kwa ushauri wenu na taarifa zenu zitakazotuwezesha sisi kufanya kazi hiyo.
Kuhusu diko la Wambaa Mhe. Naibu Spika. Jambo hili limezungumzwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chambani. Naomba nikiri ni kweli kuna tatizo la wavuvi ambao wanatumia fursa ya migomo ya kisasa kudhoofisha upatikanaji wa mapato kwa kukiuka taratibu za mnada, kuamua kwa makusudi kuhamia sehemu nyengine, na tayari viongozi mbali mbali wa Wilaya na Mkoa katika eneo hilo wanaohusika na jambo hilo wamefikishwa katika vyombo vya kisheria, yaani viongozi wa Mikoa na Wilaya wamewachukulia hatua na wamefikishwa katika vyombo vya kisheria. Kwa hivyo, tusubiri hatima ya hayo maamuzi ya kisheria yatakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika hili nataka nitowe wito. Limezungumzwa hapa suala la soko la Tumbe pia kuwa lipo tu halifanyikazi. Ni kweli hii inatokana na utaratibu uliokuwepo wa taasisi ambayo ilifadhili lile soko, iliwakabidhi wananchi moja kwa moja. Jambo kama hili Mhe. Naibu Spika, liko katika eneo la Nungwi, kuwa watu wanahisi kwamba soko ni la kwao. Soko limejengwa kupitia mradi wa *MANCEP*, kupitia Idara ya Uvuvi. Lakini masoko yote kwa mujibu wa sheria ni mali ya Halmashauri na mabaraza, sasa wako watu ambao wanakiuka hizi taratibu wanafanya haya masoko kama ni ya kwao. Sasa tumeanza kuchukua hatua na tutaendelea kuchukua hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, Serikali za Mitaa na Serikali za Mikoa zitachukua hatua kwa mujibu wa sheria na tutakapochukua hatua tusilaumiwe kwamba tumetumia nguvu kubwa. Mfano mdogo tu hapa wa ng'ombe Mhe. Hassan, amezungumza vizuri na mimi nimependa *style* yake ya Kimapinduzi, kwamba inakuwaje nchi ya Kimapinduzi Rais wa nchi anatangaza jambo halichukuliwi hatua. Nataka nikuhakikishie Mhe. Hassan na wengine, kwamba suala la ng'ombe tutawafuata wanamofugwa, hatuwasubiri barabarani na kwa yeyote ambaye ana ng'ombe kwenye Manispaa hizi na Manispaa nyengine, basi tutachukua hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi najisikia aibu Waheshimiwa Wajumbe, kwamba agizo hili limetolewa siku nyingi. Kwa bahati nzuri anapolitoa agizo hili Mhe. Rais na mimi nakuwepo. Kwa hivyo, hatua tumeanza kuchukua; punda, ng'ombe na wanyama wengine. Kwa taarifa niliyonayo Hanyegwamchana sasa hivi kuna ng'ombe zaidi ya 40. Wanaowahitaji ng'ombe wao waende wakalipe faini ambayo tumeiweka kwa mujibu wa sheria na taratibu. Masharti ya kumchukua huyo ng'ombe au mnyama mwengine yoyote, asionekane mjini. Akionekana mjini tukimkamata tena tutatumia kwa mujibu wa sheria na kanuni zetu, atakuwa muflisi mnyama huyo hawezi kurejeshwa kwa mwenyewe. Kwa sababu wanaofanya haya mambo wanafanya kusudi.

Mhe. Naibu Spika, kadhia ya ng'ombe waliokuwepo Amani ambapo Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema tumetumia nguvu. Mkakati wetu ni kwamba kumfuata ng'ombe popote anapofugwa ndani ya mjini, na kabla ya kufanya kazi hii, wiki moja iliyopita kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tulifanya mkutano na Masheha wote na wawakilishi wa *NGO's* mbali mbali kuwaelimisha juu ya hili. Tulitoa muda wa wiki moja, ikitimia wiki moja basi ng'ombe wawe wameondoka mjini.

Kwa hivyo, utekelezaji wetu unakuja baada ya sisi kutoa taarifa na hatutorudi nyuma, kwa nini? Tulichukua hatua kule Amani, tulipata taarifa kwamba kuna ng'ombe 14 wanafugwa kule Amani wamepelekwa, katika ng'ombe 14 kuna watu wanasema ng'ombe 4 ni wa Itikafu, lakini sisi tumekuta ng'ombe 14. Sasa ng'ombe 14 hao kila mwenye ng'ombe aende Hanyegwamchana afuate taratibu na masharti yetu ni kwamba ng'ombe hatakama anakuja kwa Itikafu asifugwe mjini, atafutiwe eneo siku ikifika ya kwenda kuchinjwa achinjwe iletwe nyama mjini badala ya kuja ng'ombe aliye hai.

Suala hili nadhani tumeshaanza kuchukua hatua na hatutarudi nyuma. Naogopa kutumbuliwa jibu na Mhe.Rais alikuwa wazi, anayeshindwa kuwasimamia waliochini yake tutamuanza yeye. Kwa hivyo, bado mimi nafasi hii ya uwaziri

naitaka. Kwa hivyo, ndio maana watendaji waliochini yangu wanafanyakazi hiyo kwa nguvu kubwa sana na kwa kasi, lakini kwa mujibu wa sheria, hawafanyikazi kwa kutumia mabavu. Kitendo kilichotokea pale Amani, walikwenda Askari wetu wa Manispaa pamoja na Askari wetu wa vikosi, kwa sababu operesheni hii tunaifanya kwa mashirikiano. Ikaingia rova kwenda ku...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, najua kwamba unataka kuwapa taarifa zote wajumbe, lakini muda hatuna. Naomba ufupishe hotuba yako Mhe. Waziri, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Niache nimalizie hili, halafu na *CCTV* na suala la jaa la Kibele. Kwa hivyo, kitendo kilichofanyika walinzi wa pale walivunja sheria, baada ya kuingia ile gari yetu wakaifungia ndani, kwa hivyo, Mkuu wa Mkoa na yeye na nafasi yake ya kuweza kuchungua hatua katika mkoa wake. Kwa hivyo, hatua tumezichukua za kuweza kuwakamata wale ng'ombe na kuwapeleka Hanyegwamchana.

Mhe. Hamza Hassan Juma, hili suala ulilizungumza, lakini hatukutumia nguvu, isipokuwa pale tulipolazimishwa kutumia nguvu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda, lakini majibu yote ninayo kama Waheshimiwa Wajumbe, walivyoyataka. Lakini kwa sababu unanihimiza basi sitopata muda wa kuweza kuyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la Mradi wa *ZUSP* ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameshalitolea ufafanuzi sina haja ya kulirejea, kwamba yale maeneo ambayo michirizi haijajengwa ni kuwa tunasubiri. Masharti ya *World Bank* wanataka tulipe fidia kwanza halafu ndipo tuvunje nyumba za watu tupitishe ile michirizi, lakini hatua zinaendelea za kuweza kujenga katika yale maeneo ambayo hayana *commitment* za kulipa fidia.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni kuhusu jaa la Kibele. Jambo hili lilizungumzwa na Mhe. Simai Mohamed Said Mpakabasi, najua kwa nini amelizungumza hili, kwa sababu yeye ni Mwakilishi wa wananchi katika Jimbo la Tunguu. Lakini ipo programu nzuri kupitia mradi huu wa *ZUSP* Mhe. Naibu Spika, ya kuweza kuweka utaratibu mzuri wa kuchukua taka toka zinapochukuliwa na kufika kwenye kituo maalum karibu na mji kabla hazijapelekwa Kibele, na kubagua zile taka, zipi taka hatari, zipi ngumu na zipi zinazoweza kuleta madhara na kupelekwa katika maeneo ambayo zinaweza

zikateketezwa. Pale kwenye eneo la Kibele litajengwa jaa la kisasa ambalo litawekewa *level* ya zege, ambayo itasaidia kutokupeleka uchafu yakakutana na maji ya kunywa.

Eneo lile lina hekta 45 na eneo hilo ni lile ambalo lilichimbwa kifusi ndilo ambalo tutalitumia. Pia, tutachimba kisima pale kwa ajili ya kufanyia *test* kila baada ya muda ili kujua ni athari gani ambayo imepatikana kupitia taka zile ambazo zimepelekwa pale Kibele. Kwa hivyo, Mhe. Simai Mohamed Mpakabasi, naomba usiwe na wasi wasi kwa hili, serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha hili jambo linafanyiwa kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, majibu ni mengi lakini kwa sababu ya muda naomba mengine niyawache niyaruke, na niende moja kwa moja kwenye mradi wa *CCTV*. Mhe. Naibu Spika, jina kwenye kitabu linaitwa Mradi wa *CCTV*, lakini jina sahihi la mradi huu ni Mradi wa Miji Salama, na umeanza kwa hapa Mkoa wa Mjini, tutaendelea na maeneo mengine kadri pale serikali itakapoone imepata uwezo wa kutekeleza miradi hii. Lazima tukubali wenzetu sasa hivi kama alivyosema Mhe. Hassan, twende kileo, tumekuwa tunapata tabu kwa wahalifu wa makosa ya jinai, kwa sababu tunaambiwa ushahidi kamili haupo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nitowe historia ya huu mradi. Mradi huu kwanza asili yake ni Mkoa wa Mjini Magharibi, kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama kufuatia agizo la maabara iliyotokana na maamuzi ya Baraza la Biashara la Zanzibar iliyofanyika Bwawani, Wizara yangu ilipewa jukumu hili la kuhakikisha kunakuwa na miji salama kama duniani ilivyo. Lakini jambo hili lilipopelekwa serikalini, ofisi yangu ikatakiwa iliratibu badala ya kuratibiwa na Ofisi ya Mkoa, ndipo asili yake ilivyokuja.

Pia, nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia kwako, tutofautishe kati ya mradi huu ambao mwaka jana ulitengewa bilioni 10, mwaka huu bilioni 18 na mwaka mwengine utatengewa pesa nyengine kufuatia na fedha zitakazokidhi haja kwa mujibu wa mahitaji. Usilinganishwe wala usichanganywe na mradi wa *CCTV* ambazo zimeanza kuwekwa. Kuna *CCTV* za aina mbili; Mradi wa *CCTV* wa msaada wa ndugu zetu wa Kichina *ZTE* unajumla ya kamera 260. Kamera watakazozifunga ni *point* 40 tu katika maeneo ambayo tutawaelekeza sisi, zilizobaki watatupa tuweke katika maeneo ambayo tunahisi yatafaa kuwekwa kamera hizo kwa gharama zetu, na ushauri hapa umetolewa.

Kwa mfano, Mhe. Abdalla Ali Kombo, alishauri kwamba basi angalau kwenye masoko tuweke kamera hizo. Sasa nataka nimthibitishie kwamba kwenye

masoko na maeneo mengine ambayo Kamati ya Ulinzi na Usalama itahisi iziweke hizo kamera kwa msaada wa ndugu zetu wa Kichina wa *ZTE.* Kwenye kamera 260, kamera 40 ndio zitafungwa kwenye maeneo machache na zilizobakia tutazipeleka katika maeneo ambayo yatafungwa. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema kwamba mradi kabla haujaanza kamera sijui imekua na giza. Zile hazihusiani na Mradi huu wa *CCTV* unaosimamiwa na ofisi yangu, isipokuwa baada ya kutekelezwa ule mradi uko chini ya Jeshi la Polisi, na zile kamera ni za *civil* kwa ajili ya *traffic* na sio *military*. Kamera ambazo tunazifunga ni *military* ni kwa ajili ya ulinzi, ni maalum kwa ajili shughuli za ulinzi na ni tofauti kabisa na kamera hizi. Lakini hayo yote ni kwa mujibu wa maamuzi ya serikali, tumetakiwa nazo sasa tuzisimamie sisi. *Control Centre* sasa hivi iko pale Malindi. Utakapokamilika mradi huu *Control Centre* tunajua sisi wapi tutaiweka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, siwezi kuitangaza kwa sababu nikitangaza, maana yake nasema anayetaka kuja kutuvamia ajue *Control Centre* ya mradi huu iko wapi, na mradi ule wa msaada wa Wachina *ZTE* tulipowataka watwambie thamani, walitwambia una thamani ya Dola milioni 3,500,000. Mradi wetu kwenye *Component* ya *CCTV* peke yake kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha una asilimia kumi, sasa kamera za mradi wetu ni 928 zina thamani ya Dola za Kimarekani 3,581,900 sasa kamera 260 na mia 928 zimepishana kwa *how much*?
Kwa hivyo, mradi ule tumesaidiwa na wenzetu Wachina na haihusiani kabisa na mradi huu wa kamera zetu ambazo ni *Military* na sio *Civic* kama vile zilivyo zile, zile ni kwa ajili ya kusaidia matukio ya *Traffic* na mambo mengine, hivi za kwetu kwa ajili ya kusaidia mambo mengine na kama alivyokwisha kusema Waziri wa Fedha kwamba ni asilimia kumi tu ya dola 28,900 kwa hizi kamera na Mhe. Nadir, alitaka kujua kamera hizi zinatoka wapi, Kamera hizi zinatoka Sweden, aina gani hatukwambii ili tusije tukapata mtu mwengine akaja akajua ni aina gani ya kamera hizi na yeye akaweza kuja kutufanyia uhalifu. Kwa hivyo, tunapolinganisha ni vizuri tukalinganisha.

Lakini jengine Mhe. Hamza, kwa hivyo, asilimia kumi ya fedha hizi ndio za *CCTV*, asilimia 90 ni vifaa vyengine vya ulinzi, si vizuri sana kunitaka mimi niseme hapa ni vifaa gani, lakini ndani yake kuna mambo mengi ya kiusalama, tuna janga hapa la ajali ilitokezea sote tulifadhaika, miongoni mwa hivo vifaa kuna vyombo ambavyo vina *Thermal Camera* inayoweza kujua chini ya bahari kuna nini, chombo kimezama wapi, watu waliohai wako wapi ili tuweze kuwaokoa, sasa si jambo tu la kamera za *CCTV*.

Naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, waelewe kwamba mradi huu ni muhimu na hakuna chembe hapa ya hofu, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha, kwa mujibu wa sheria hii Namba 9 ya mwaka 2005, kwenye kifungu inaruhusu kwa miradi hii ya kiusalama kwenda kwenye *Single Source* baada ya Serikali kujiridhisha kifungu cha 67(1)(6) na kabla ya kufanya hivi kuna kampuni saba ziliishauri Serikali kuhusu jambo hili, ziliishauri Serikali kama mimi kama Waziri sijapeleka waraka Baraza la Mapinduzi, kwa hivyo, taratibu za kiserikali zilifuatwa kwa kufuata sheria hii.

Wataalam mbali mbali na viongozi wamekwenda kuona uwezo wa hiyo kampuni na mahusiano na kampuni zenye utaalam wa mambo haya katika nchi ya China, Romania, Dubai, Afrika ya Kusini, Israel na Netherlands, kwa hivyo, Serikali katika jambo hili naomba sana Mhe. Naibu Spika, wasione pengine sisi tumekurupuka au kuna mambo gani yamefanyika, tumefuata taratibu zote za kisheria, sasa nimemsikia Mhe. Hamza, anataka iundwe Kamati Teule, huwezi kuunda Kamati Teule kwa kitu ambacho hakijawa na utekelezaji wake haujawa, hizo pesa hazijapatikana isipokuwa kampuni imeanza ku-*install* na kuweka *order* na kuleta baadhi ya vitu vingine kama magari na mambo mengine, huwezi kuunda Kamati Teule, sasa kama taratibu hizo za Baraza la Wawakilishi, Mhe. Naibu Spika, zinaruhusu sijui.

Lakini huwezi kuunda Kamati teule kwa kitu ambacho hakijatekelezwa, watu duniani watatushangaa, sasa kama tunataka kuunda Kamati Teule kwa matakwa yetu, hiyo ni shauri yetu sisi wenyewe, lakini sisi Serikali tunasema wazi hatuwezi kukubali kuunda Kamati Teule kwa sababu hilo jambo linalotaka kuundiwa Kamati Teule halijafanyika, unakwenda kutafuta *information* gani.

Mhe. Naibu Spika, jengine alilolizungumza Mhe. Hamza, lilikuwa ni suala la kampuni ya kizalengo, yaani suala la kuzoa taka katika Wilaya ya Kaskazini A. Naomba Mhe. Naibu Spika, univumilie nimalize hili na suala la ujenzi wa soko Kinyasini, *ZanRicky* ziko kampuni tano ambazo zimepewa tenda kama wakala wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A kukusanya au kuzoa taka na kupeleka mapato kwenye Halmashauri ya asilimia kumi ya yale mapato wanayoyapata. *ZanRicky* ni kampuni kweli ni ya ubia kati ya Wazalendo na wageni na hiyo kazi inafanywa, lakini kuna kampuni nyengine nne za wazalendo watupu, kuna kampuni ya Safina *Cleaner Hotel*, hii *ZanRicky* ina hoteli saba, hii Safina ina hoteli kumi na mbili, *HK.Trader and Hotel* ina hoteli saba, Mungu Tuwafiki ambayo ndiyo hiyo inayopigiwa kelele ina hoteli kumi na nane na Masemo *Trader Hotel* au sina hakika Mhe. Hamza, alikuwa anaizungumzia kampuni gani.

Lakini ni kweli ipo kampuni ya kizalengo hii Mungu Tuafiki haitulipi kodi yetu, sasa hivi tunaidai milioni kumi na nne na hatukufichi kama ndio hii unayoizungumza tunaipa muda ukifika mwezi wa Julay, tunakata mkataba nao na tutawapeleka kwenye vyombo vya sheria watulipe pesa zetu, kama ni nyingine nje ya hizi nitaomba unifahamishe, ni ipi kati ya hizi tano nilizokutajia. Lakini kwa huyo ambae hata kwa Makamu wa Pili wa Rais amefika, ametembea kwa viongozi wote kama ndio huyu, huyu tuna tatizo nae hatulipi kodi yetu, kwangu amefika, kwa wazee wa Chama Mkoa wa Kaskazini amefika, lakini tatizo lake halipi kodi za Halmashauri, sasa kama ndio huyu Mhe. Hamza, kama sie naomba radhi, utanipa jina la hiyo kampuni, lakini kampuni tulizonazo ni hizo.

Suala la ujenzi wa soko kauli aliyotoa Babla aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa, lililozungumzwa na Mhe. Nadir, amelitoa kwenye kampeni za *CCM,* mimi sina hakika amepandaje kiriri, lakini kama ilikuwa ni mkutano wa chama na akakaribishwa kuweza kusema machache na akasema kwamba ujenzi wa soko utajengwa huyu alikuwa akiifagilia *CCM,* akiwapa matumaini wananchi kwamba kuna soko la Ghorofa litajengwa na hilo soko la Ghorofa litajengwa kweli, hivi sasa utaratibu wa kumpata mkandarasi unakamilishwa na tunatarajia kuanzia tarehe 1 Mwezi wa 8 soko hili na soko la *Qatar* lianze ujenzi wake.

Kwa hivyo, kumtuma sikumtuma Mhe. Nadir, lakini inawezekana alikuwa katika kutekeleza majukumu yake, kwa hivyo, sikumtuma, alifanya wajibu huo kama aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, na kama alipanda kwenye kiriri cha kampeni kama alikwenda kwa njia zake nyengine au ugomvi au kama kuna kitu chochote mimi sitaki nikiingilie. Lakini ukweli ni kweli soko la Kinyasini litajengwa na hivi sasa *Management* ya Halmashauri ya Wilaya imeshazungumza na wafanyabiashara tuwahamishe katika eneo lile wakae kwenye eneo la zamani kwa ajili ya kupiga mnada na kupisha ujenzi wa soko ujengwe. Sasa kama ni eneo hilo basi Mhe. Naibu Spika, huo ndio ukweli wa jambo hili.

Naomba radhi wale wote ambao sikupata nafasi ya kutoa ufafanuzi, isipokuwa kuna jambo jengine la Mhe. Mohammed Said (Dimwa), hili nitaomba alichoomba kwa vijana wake pale *Botanic Garden,* Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ofisi yake iko wazi unaweza kwenda mkenda mkashauriana tukaona ni kwa kiasi gani tunaweza tukashirikiana na hao vijana. Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba radhi kwa wale niliokuwa sikuwajibu na kutotoa ufafanuzi kwa sababu ya muda. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu 156 kwa idhini ya Baraza yote kati ya Kanuni hizi yaweza kutengwa kando kwa madhumuni mahususi baada ya Mjumbe kutoa hoja kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nilikufahamu sana kumuhimiza Mhe. Waziri pale, nilichokijua na kwa vile si muda mrefu ulirudi kutoka Makka na hivi sasa tumo katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa mwaka mara moja, naomba tuahirishe Kikao hichi mpaka kesho ili tuje tuendelee na kitu chenyewe mwaka mara moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kwa mamlaka niliyopewa hilo nalikataa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, bado tunaendelea na Wizara hii na kwa kuwa muda wetu hautotosha kuingia ndani ya Kamati, hivyo, nitamuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kututengulia muda ili tuweze kuendelea na shughuli hii Mhe. Waziri, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum amefanya majumuisho ya Wizara yake na kwa kuwa sasa Baraza lako itabidi likae kama Kamati ya Makadirio na Mapato kwa ajili ya kupitisha bajeti hii, na kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kumaliza shughuli hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako tukufu tuweke kando Kanuni ya muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali Hotuba ya

Bajeti ya Afisi yangu, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Afisi yangu, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

KAMATI YA MATUMIZI

KIFUNGU D01 AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

KIFUNGU D 0101 Idara ya Uendeshaji na Utumishi 900,000

JUMLA YA FUNGU **900,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu na vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0101 Programu Kuu ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kifungu kidogo SD 0101

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ninakushukuru kunipa nafasi hii ili nikaweza kupata ufafanuzi wa ziada kwa Mhe. Waziri, kwanza nataka nimshukuru sana Waziri wa Fedha Dkt. Khalid jinsi alivyokuwa ameweza kutoa ufafanuzi katika baadhi ya masuala yangu. Lakini pia nilikuwa nataka nipate maelezo ambayo Mhe. Waziri, alieleza vizuri sana na alieleza kwamba ameteuliwa kuwa Waziri, ameteuliwa tena kutokana na imani ya Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nenda kwenye hoja huna haja ya kuelezea, muda, muda.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Lakini pia nilikuwa nataka niseme tu kwamba hata wale waliokuwa hawakuteuliwa tena pia Mhe. Rais ana imani nao. Swali langu linakuja hapa, katika mradi wa *CCTV Camera* sitaki kwenda ndani sana kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha, lakini hapa tulikuwa tunataka sisi kupata maelezo, ninafikiri Waheshimiwa Mawaziri wakitujibu kwa utulivu, sisi tunafahamu vizuri na mradi huu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwamba, hii miradi iko miwili. Lakini katika kitabu na katika hotuba yake haikuelezwa kama ni miradi miwili, lakini vile vile ameeleza kwamba huu mradi ambao tuliokuwa tunauhoji tukataka

maelezo anasema mradi huu ni mpya na wala haujaanzwa kutekelezwa.Lakini katika kitabu chake Mhe. Mwenyekiti, niliona kwamba mradi uliwahi kuombewa bilioni kumi mwaka uliopita na zilipatika bilioni nne, sasa ndio maana nikasema hizi bilioni nne ambazo zilizopatikana tupate maelezo yake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri sisi tunafanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Katiba ya Zanzibar Ibara ya 88 na mimi naweka kifungu kimoja tu cha (c) kinaeleza kwamba; "Moja katika kazi yetu kuuliza maswala mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, kuuliza maswala sio nongwa wala chuki wala kibri ni suala limo kwenye Katiba, kwa hivyo, mimi naomba tujibiwe maswali yetu kwa mujibu wa utaratibu wa Katiba unavyotaka naomba jawabu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza, hatukuelewa, ilikuwa ni maoni au ilikuwa unauliza swali, hujaridhika na majibu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nauliza matumizi na kwa sababu hapa tupo kwenye Kamati ya Matumizi. Katika kitabu cha Mhe. Waziri, alielezea kwamba mradi wa *CCTV Camera* uliombewa bilioni kumi kipindi kilichopita na wakapewa bilioni nne. Kwa hivyo, ina maana kama walipewa bilioni nne, *of course,* kuna *activities* tayari zilishaanza kufanyika. Sasa tulitaka tupate maelezo, sio vyenginevyo, hakuna mtu aliyekuja kitu ndani ya kichwa chake, mambo yote tumeyapata kwenye kitabu, ndio hayo tu niliyokuwa nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kama alisikiliza utangulizi wangu nilisema sichukii hata kidogo kuulizwa, kuhojiwa na kutaka ufafanuzi na nilipokuwa nikitoa ufafanuzi pia katika mradi huu nilitoa tofauti ya mradi wa *camera* za *ZTE* ambazo tumepokea msaada na nikatoa mradi wa *CCTV Camera* ambao unajumuisha mambo mengi, lakini nikasema mengine siwezi kuyasema, lakini katika fedha ambazo zimetengwa ni asilimia kumi tu ya fedha hizo, nazo kama utakuwa umenisikiliza vizuri na wajumbe wamenisikiliza ni dola 28,000,000. Asilimia 10 ya fedha hizo ndio za *CCTV* na nilichosema kwamba *component* ya mradi wa *ZTE* haihusiani na *component* ya mradi huu kwa *CCTV* ambao unatekelezwa moja kwa moja na ofisi yangu, hilo nililisema.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kitabu, kitabu kinasema hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, ukurasa wa 12, naomba ninukuu kifungu 29.

"Mhe. Spika, aidha katika kutekeleza huduma ndogo ya pili ya uwekaji ya camera za ulinzi *CCTV camera* na vifaa vya ulinzi Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni kumi hadi kufikia Machi, 2016 Idara imeingiziwa jumla ya shilingi bilioni nne, mia moja na ishirini na nne, mia mbili na tano elfu sawa na asilimia 41".

Sasa ndio maana nikasema kwamba kama hizi fedha tayari ziliingizwa, ndio maana nilitaka *at least* zile *activity* ambazo ziliwahi kufanyika kwa kupitia fedha hizi, hilo tu ndio nililokuwa nauliza swali, limo ndani ya kitabu wala halikutoka kichwani kwangu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi sibishani nae kwamba hakusikia na ndio maana kila wakati nilikuwa nikisisitiza Mheshimiwa, nisikilizwe. Ninajua kwamba katika bilioni kumi, kwanza huu mradi unatekelezwa katika kipindi cha miaka 5 na kuna *guarantee* ya miaka 5 na wanaoleta vifaa vyote hivi vitakuwa chini ya uangalizi wao kwa muda wa miaka 5. Mheshimiwa, mmoja alitaja habari ya *warranty* , kwa hivyo, ni kweli kipindi kilichopita tuliomba bilioni kumi zikaingizwa bilioni 4.124 na nilisema tayari kampuni hii imesha-*install* baadhi ya nguzo, imeleta baadhi ya gari na vifaa vyengine na vipo. Kwa hivyo, kazi iliyobakia sasa ni kuweza kuleta *items* nyengine ambazo zimo ndani ya *component* ya mradi, hilo nililisema, sasa Mhe. Hamza, kama hakusikia ninamuomba kwamba hayo niliyasema na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wengi wao ukiwemo na wewe Mhe. Naibu Spika, umesikia kama nimesema hivyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tumeelewana na kwa sababu kama nilivyosema hoja ya Mhe. Waziri, alizungumza yalikuwa kuna mambo karibu mawili kwa matatu. Moja ule mradi wa *ZTE* ambao alisema kwamba hauhusiani na hili ambalo mimi ilikuwa ndio *project* ambayo niliyokuwa nimejaribu kuizungumza, lakini hili la kusema kwamba tayari kuna hizo nguzo zilizoanza, sasa hilo mimi Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika nalo lakini hoja yangu ilikuwa pale aliposema kwamba huu mradi hauwezi ukaundiwa Kamati Teule kwa sababu haujaanza. Kwa hivyo, mimi ninafikiri tukubaliane tu huu mradi umeanza na ile kusema kwamba tutaunda Kamati Teule *just* kujiridhisha kama sikuridhika na maelezo yake. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima na niwapongeze

Mawaziri wote na Manaibu Waziri wote wanaosapotiana na kuteteana uzuri katika hoja hizi kwanza nawapongeza kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri wanaposimama hawateteani isipokuwa ni wajibu wao kutoa maelezo katika vipengele ambavyo wanatakiwa watoe. Naomba hilo uliweke sawa hawateteani, ni kazi yao na ni wajibu wao. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Sawa ni kazi yao na wajibu wao, ahsante kwa kufanya kazi vizuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaingia kwenye suala hilo la *CCTV Camera.* Kwa kweli Mhe. Waziri anatwambia kwamba 4.1 *billion shillings* keshapewa na ushaanza mradi wa hizo nguzo na gari, mimi ningependa kumuuliza kwanza, nguzo gani na gari ambazo zinafika hizo bilioni nne na milioni mia moja. Angetutajia tu gari ya aina gani na nguzo ngapi ambazo zishakuwa *isolated* kwenye kisiwa hiki ikafika bilioni nne na milioni mi moja.

Isitoshe ninahisi kuna vitu mimi sitaki kuingia kwenye *internal security* kuhoji sitaki kujua, lakini ninahisi saa nyengine tunavyoelewa kama changa la macho, kwa sababu kitu kimoja humu humu kwenye *security*, utaambiwa *military security*, *CCTV Camera*, utaambiwa *camera* za baharini, KMKM inawahusu humu humu, hili suala liko vipi? Kwa sababu kama kuna kifungu kinawahusu KMKM kiwekwe kwenye KMKM tuje tukione. Kama kinahusu *military* kije kwenye *military* tukione, lakini sasa tukipigwa kitu kimoja kwa vitu 4 ndani halafu tukafichwa fichwa tunakuwa hatufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu kwanza ni hilo kwenye hizi bilioni nne na milioni mia moja zimetumika vipi kwenye gari gani kwanza zililoletwa na nguzo ngapi zilizokuwa *installed* ndani ya kisiwa chetu ambazo katika 4.1 *billion shillings*, naomba nimuulize Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Nadir, kwa swali lake ijapokuwa hoja hii mimi nimeshaitolea maelezo. Kwa mujibu wa taratibu nisingepaswa tena kuitolea maelezo, kama ana hoja nyengine ailete. Kwa hivyo, mimi nadhani Mheshimiwa maelezo ni yale na mradi huu ni wa miaka wa mitano, umeanza kutekelezwa na utaendelea kutekelezwa kwa kipindi cha miaka 5. Sasa fedha hizi akitaka nguzo gani, ngapi hata kesho tufatane nimuonesha wapi na wapi zimewekwa nguzo, gari zimewekwa, lakini siwezi kumwambia hapa.

Kwa hivyo, mimi Mheshimiwa kwanza tuzingatia utaratibu, hoja hii nimeshaitolea maelezo, sipaswi kutoa maelezo mengine. Lakini Vile vile Mhe. Nadir, ni mjumbe wa Kamati, jambo hili hakulitolea ufafanuzi wowote wala hakutaka maelezo kwenye kamati na akakubaliana na hoja hii. Sasa anapokuja hapa anageuka, mimi sijui, lakini maelezo yangu ni hayo, sina maelezo mengine zaidi ya hayo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi swali langu Mhe. Waziri, hajalijibu, halafu mimi ni mjumbe wa kamati, lakini kwanza nilikuwa niko nje ya nchi. Niliporudi nimeridhika na asilimia 90 ya hoja hii, lakini kwa hoja ya *CCTV* sikuridhika nayo na mimi kama mjumbe nina haki ya kuzungumza kwa niaba ya wananchi na kuchangia serikali vile vile. Mimi swali langu liko pale pale kama ni gari tu, ametamka ni gari, mimi nimetaka kujua atwambie labda gari hilo ni *fire*, *ambulance* na nguzo labda nguzo ngapi, lakini ninahisi sijapata jibu nililouliza. Kwa sababu tukizungumza bilioni nne na milioni mia moja sio pesa ya kitoto, ni fedha ambayo nyingi. Mimi ningeomba tu kama ni gari labda ya siri, si tatizo asinitajie, lakini kama ni gari ya kawaida ya kuja kuanza kwa sababu alizungumza Mhe. Waziri, gari iliyokuja kuanza kazi inabidi inaonekana ni gari ya kutendea kazi kwenye masuala ya *camera*.

Utaratibu

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nadir, ana haki zote za kuuliza na kutaka kujua, lakini yeye ni Mjumbe wa Kamati hii na mimi ni Mwenyekiti wake ninamuomba sana Mhe. Nadir, akubali kifungu, tukienda kwenye kamati aombe maelezo kwa waziri na nina hakika atapewa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya Kamati yangu nakubali hili suala na nitakuja kumuomba yeye Mwenyekiti wangu aje twende pamoja akanipe hayo maelezo. Ahsante sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37 inatulinda sisi wajumbe na pia Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa agizo nilimsikia kwamba kuwa Waheshimiwa Mawaziri watujibu kwa ufasaha ili wananchi; wakwezi na wakulima sisi tuweze kufahamu serikali *plans* zao. Mheshimiwa, nilimuuliza, katoa maelezo mazuri kuhusu sasa hivi anachokifanya dhidi ya ng'ombe, lakini nilimuuliza miaka mitatu na nusu imepita agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, agizo la kimapinduzi, kwa nini halikutekelezwa. Nchi za wenzetu agizo kama hili amelitoa Rais

hujalitekelezwa lina hatari kubwa sana. Kwa nini agizo hili, kazunguka lakini hajajibu, kwa nini kwa miaka mitatu na nusu suala hili halikutekezwa mpaka limeleta si picha nzuri. Sitaki *present* nataka *future* hilo la kwanza.

Lakini la pili, niliuliza usafi wa mji, ndio hapa hapa pahali pake, niliuliza hizo taka majaa yapo mangapi sikujibiwa. Vipi zile taka zinakuwa *destroyed,* kwa sababu wasi wasi wangu kwa utaratibu niliouona zinafanyiwa hizi taka huenda zikawa zinasababisha maradhi ya Kipindupindu kwa sababu hazifati Sera ya *Waste Management*. Niliuliza pia majaa ni mangapi na wanafanya vipi ku-*dispose* taka, sijajibia. Lakini pia niliuliza nina wasi wasi na hizi *camera* na taa za barabarani. Nchi nyingi za Kiafrika tunazitafuta hizi *National company*, kampuni za nje kuja kututolea vitu, halafu zinatuacha sisi, hapa hapa jamani Mheshimiwa, nilinde kiti chako, halafu zinatuacha sisi na mapengo chungunzima.

Sasa niliuliza neno '*warranty'* kalitaja lakini hakujibu, sasa nauliza *CCTV Camera* hizi zina *warranty* wa miaka ngapi na taa za barabarani hizi zina *warranty* wa miaka mingapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kwa masuala yake matatu nilikuwa nina hamu sana nimjibu, lakini Mheshimiwa nilikupa indhari itapotokezea kupigiwa buti na wewe unilinde. Kwa sababu sikupata muda wa kuweza kuyajibu masuala yote ya wajumbe na mimi nilidhani pengine kwa heshima ya kiti chako wajumbe wameridhika. Hata hivyo, mimi natambua kwamba ni wajibu wao.

Agizo la Rais limetoka miaka 3 iliyopita, mimi nimeingia ofisi hii miaka 2 iliyopita, tumejitahidi sana kuweza kuchukua hatua, lakini yapo mambo ambayo nimeyasema ya watu wetu kudharau sheria na kutokuwa na vyombo madhubuti ambavyo vinaweza vikenda vikatafsiri hizo sheria zilisababisha zoezi hili likwame. Sasa naomba nimwambie Mhe. Hassan kwamba, zoezi hili limekwama kutokana na hilo na unaweza ukamchukulia mtu hatua ukapata simu za baadhi yaviongozi, barua, leo nataka nimthibitishe Mhe. Hassan, asubuhi nilipokea viongozi wanakuja kuniomba ng'ombe wao niwaruhusu, jambo hilo ndilo lilosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa hili jambo.

Lakini sasa Mhe. Hassan, aamini kwamba tumepania kulitekeleza na ndio maana tumechukua hizo hatua na hivi sasa wakirudi ng'ombe mjini hapa, basi yeye mwenyewe akaja akanishauri au akaniuliza ilikuwaje ng'ombe wakarudi mjini. Kwa sababu tumepania kwa umuhimu huo huo na hii ni nchi ya

kimapinduzi na mimi ninakubali ya wakwezi na wakulima katika tafsiri pia wavuvi wamo na mimi mvuvi na kwetu pia walitoka watu ambao wamepoteza roho zao kwa ajili ya Mapinduzi haya.

Kwa hiyo na mimi ni sehemu ya Mapinduzi. Kwa hiyo, Mhe. Hassan, aridhike kwamba ni kweli ucheleweshaji umekuwepo, lakini hivi sasa tumepania kuondosha kadhia hii kwa ajili ya kulinda kadhia au kauli ya Mhe. Rais, aamini hivyo kwamba timu niliyonayo kuanzia Mkuu wa Mkoa, Wakurugenzi wana uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Majaa yapo mangapi, nilikuwa natamani sana nimjibu lakini kwa sababu ya muda, majaa yako 70 na utaratibu wa kuzikusanya taka na kuzipeleka kunakohusika niliueleza wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Simai Mohammed Said wa Jimbo la Tunguu. Kwamba kupitia Mradi huu wa *ZUSP* tutakuwa na kituo maalum kwanza kuanzia uchukuaji taka kule zinapotoka kwa watumiaji na kuzifikisha katika kituo maalum na kuzipambanua zipi ziweje na zipi ziweje.

Hata ile *volume* kwenye magari itapungua kwa sababu kutakuwa na utaratibu maalum wa kuweza kuzibana ili ziweze kupelekwa katika jaa. Na katika lile jaa utaratibu wa *disposal* utafanyika na kuna mpango na mradi maalum na fungu maalum linalosimamiwa na *ZUSP* chini ya Wizara ya Fedha litarekebisha hayo mambo kwa kuelewa, nathamini sana, yeye amesema hili kwa sababu eneo lake ni moja kati eneo ambalo pengine nalo limeathirika kwa maradhi haya ya Kipindupindu.

Serikali ilipoweka huu mpango umeweka mpango huu kwa ajili ya kuepukana na hayo mambo baada ya kufanya utafiti. Kabla ya kuanza kwa Mradi huu *ZUSP* kumekuwa na washauri wameishauri serikali na *World Bank* wakakubali na ndio maana tunakwenda katika *stage* hiyo sasa ya kuweza kuzihamisha taka na kuzipeleka huko kwa utaratibu huo ambao Mhe. Hassan, kwa uzoefu wake wa nchi ambazo aliwahi kuishi kwa kwenda kufanya kazi, ndio ambao tunautaka tuufanye sasa na sisi tuepukane na kuwa dunia ya mwisho. Sasa tutukuze vya kwetu, ndio hiyo juhudi ambayo inafanywa na serikali. Kwa hiyo, kwa sababu ya muda sikupata muda wa kuweza kueleza, lakini sasa hivi amenisaidia kuweza kumueleza ile mipango ya serikali ambayo inataka kufanyika. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, suala la *warranty* bado hajatujibu kuhusu *warranty* ya taa za barabarani na *CCTV camera* zina *warranty* muda gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, suala la taa lishajibiwa na Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu mradi wa taa unasimamiwa na Wizara ya Fedha na nilidhani maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Fedha, yalikuwa yanakidhi haja. Kwa sababu hapa unajua tumezoea japo kuwa serikali tunafanya kazi kwa pamoja tunawajibika kwa pamoja, lakini ni vizuri lile suala likapelekwa katika sekta husika. Sasa mimi ni mfaidika wa mradi wa taa, lakini sio mimi ninayeweza kumuhoji mkandarasi au *supplier* kwa sababu siye *client* niliyempa kazi. Wizara ya Fedha wakishakabidhiwa ule mradi ndio utaletwa kwangu kwa ajili ya uendeshaji. Kwa hiyo, indhari zote na hadhari zote amezisema Mhe. Waziri wa Fedha.

Lakini kuhusu *warranty* na muda gani mradi huu utakuwa chini ya *contractor* na *supplier* huu wa *CCTV* kwa muda wa miaka mitano utakuwa chini ya uangalizi wa ile kampuni ambayo itafanya kazi hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan, nafikiri majibu yako umejibiwa na jibu ambalo umeliulizia kuhusu suala la taa ni kweli Waziri wa Fedha amelijibu tena vizuri sana. Sasa kwa hiyo…

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Naomba tuendelee amejitahidi.

Kifungu SD 010101	Programu ndogo ya Uratibu wa Tawala za Mikoa	2,191,640,000
Kifungu SD 010102	Programu ndogo ya Uratibu wa Serikali za Mitaa	200,000,000

Mhe. Mwenyekiti: Kimeshapita kifungu Mheshimiwa, umechelewa, Mheshimiwa, nimeshauliza kifungu kimekubaliwa na kimeitikiwa, ndio wewe umegonga. Kwa hiyo, kimeshapita.

Kifungu SD 010102	Programu ndogo ya Uratibu wa Serikali za Mitaa	200,000,000
	Jumla Kuu	**2,391,640,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0102	Programu kuu ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ
Kifungu SD 010201	Programu ndogo ya Uratibu wa Idara Maalum

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, katika suala zima la uratibu wa Idara Maalum nilikuwa na wasi wasi wakati nilipochangia juu ya asilimia ndogo ya fedha ambazo ziliingizwa. Nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kuweza kunijibu hoja hiyo, alisema kwamba wafanyakazi wengi katika idara hii basi mafao yao au mishahara yao inatoka katika vikosi vyao na ndio maana hii asilimia ikawa ndogo. Lakini tuseme kwamba fedha hizi zingeingizwa kwa asilimia 90 au 100 zingetumika kwa matumizi gani?

Vile vile, mwaka 2016/2017 fedha hizi zimeongezwa tena badala ya milioni 44, 854,000 hivi sasa kuna milioni 44,993,000, kama ni hoja kwamba hawa watu wanapata mafao katika vikosi vyao, kwa nini na mwaka huu pesa hiyo inazidi? Kwa mfano, ikiingizwa asilimia 100 pesa hizo zitatumika kwa matumizi gani? Tunataka ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, bajeti yetu inakwenda kwa *cash budget*, yaani unapopata ndipo unatumia, na ndio mfumo tulionao. Na sisi tunapitisha makisio na bajeti, sasa fedha zitavyoingia ndivyo tutakavyozipokea na kuzifanyia kazi. Mimi ningetaka bilioni zote 81,000,000,000 nipate *hundred percent* lakini haiwezekani. Kwa hiyo, Mheshimiwa, zitakapokuja zitatumika kwa zile kazi zilizokusudiwa kufanywa kwa mwaka huu kwa idara hii ya Uratibu wa Idara Maalum. Zisipokuja tutaendelea na mwaka mwengine kuzifata kwa sababu yale malengo tuliyokusudia kuyafanya yatakuwa hayajakamilika.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Makame kwamba, jambo hili ni jambo la kawaida na namuomba Mheshimiwa, aelewe kwamba sisi tungetaka sana, lakini tunapoletewa utaratibu wetu wa kuletewa mafungu, kwa mfano fungu hili liko chini ya D01, yaani ni fungu la ofisi kuu. Kwa hiyo, linapokuja mkipata milioni mbili, maana yake mugawane gawane kidogo kidogo, na inategemea vile vile nani ana jambo gani ambalo tunahisi anaweza akalifanya na kulimaliza tutampa *priority* yule.

Kwa hiyo, mimi nadhani cha msingi tukubaliane tu kwamba jambo hili linatokea kutokana na ufinyu wa fedha, nchi yetu ingekuwa na uwezo wala tusingefika hapa, ingekuwa unaomba pesa za miezi mitatu pengine na unaingiziwa na unafanyiwa shughuli zako. Lakini hali hiyo hairuhusu kwa sababu ya mfumo wetu tunaokwenda nao wa *cash budget* na kwa sababu serikali imeweka msisitizo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi hiki, sio

kuongeza kodi, ni imani yangu pengine serikali inaweza ikatutimizia mahitaji yetu kwa hiki kifungu ambacho tumepewa. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mheshimiwa, tuendelee.

Kifungu SD 010201	Programu ndogo ya Uratibu wa Idara Maalum	44,993,000
	Jumla Kuu	**44,993,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizibila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0103

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna suala nililielezea kutokuridhika kwangu na jinsi uingizwaji wa fedha katika hii Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Katika bajeti ya mwaka uliopita walitengewa fedha karibu zaidi ya milioni 130,000,000 kama sikosei, na yale mategemeo walitegemea wapate kama 122, lakini mpaka tunaingia katika *quarter* hii waliingiziwa shilingi milioni 7,000,000 tu kwa kweli hili suala halikuniridhisha hata kidogo. Kwa maana hiyo tume hii inaonesha kwamba ilishindwa kufanya zile kazi zake ipasavyo, kwa sababu hata asilimia alau ingelifika 25 au 30, lakini asilimia chini ya 10. Hebu labda ningelipata maelezo kwa nini idara hii haikuingiziwa fedha kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, jibu halitotafautiana na lile la mwanzo, sababu za kule ndizo hizo hizo sababu za hapa. Lakini ndio maana yanaitwa makisio, kwa sababu ni makisio unakisia utatumia hiki baada ya kupata ndio unaingiziwa na unatumia, usipopata maana yake hutumii. Na tunapofanya hizi kazi katika shughuli zetu Mhe. Hamza, anaelewa ameshawahi kuwa kwenye nafasi kama hii, unaangalia jambo ambalo haliwezi kusubiri lipi.

Kwa hiyo, jibu langu ni kama lile la kule kwamba sisi tunakwenda kwa mfumo wa *cash budget* na haya ni makisio, tunakisia na tunapitisha makisio na bajeti. Serikali inapopata uwezo wa kuweza kuitekeleza *hundred percent* itatoa na inapokuwa haina uwezo wa kutekeleza kwa asilimia itakayopatikana ndio ambayo serikali inatuingizia. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Hamza, kwamba jibu langu la hapa na kwenye vifungu hivi vya ndani ya *votes* zangu zote kuanzia D01 mpaka D12 hakuna pahala ambapo tutakwenda tusiwe na upungufu wa eneo hili.

Kwa hiyo, naomba waheshimiwa wajumbe, watambue kwamba mimi kama waziri ningefurahi sana kupata asilimia kubwa ya fedha ambazo tumekisia. Lakini kwa sababu ya hali na mimi ndio pale niliposema katika kipindi hasa cha mwaka huu tunaomalizana nao tumekutana na mambo mawili makubwa ambayo yalikuwa hayawezi kusubiri; moja ni la uchaguzi. Sasa mimi nadhani mheshimiwa, wajumbe waelewe kwamba tumepata upungufu kwa sababu ya dharura zilizokuwepo. Namuomba sana Mhe. Hamza, aniruhusu niendelee na mafungu haya kwa sababu sababu nyengine nitakuwa sina zaidi ya haya ambayo nimeyaeleza. Na hata ukimwita Waziri wa Fedha atasema hivyo hivyo kwa sababu yako nje ya uwezo wetu. Mheshimiwa, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakiri maelezo ya waziri, niliwahi kukaa kiti cha mbele, lakini Mhe. Mwenyekiti, asilimia 7. *Oh! This is too much*. Mhe. Mwenyekiti, hizi tume tunazozipitishia mafungu kwa kweli tunazipitishia mafungu ili wakatekeleze yale mambo ambayo waliyotuletea kwenye *PBB*. Sasa mimi ninavyojua kwamba Katibu Mkuu yeye ndiye *accounting officer* zinapokuja zile *OC* anaangalia zile *priorities,* yaani *priority* za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum zilikuwa hazina umuhimu kweli kweli.

Mimi nilikuwa nahisi zilikuwa zina umuhimu labda tu Mhe. Waziri, aniahidi basi alau katika kipindi hiki tunachokwenda nacho hii asilimia ivuke zaidi ya asilimia 10 na twende alau kwenye asilimia 25, ili na hawa walioomba tuwaidhinishie fedha wakatekeleze majukumu yao wawe na nyenzo za kufanyia kazi. Mheshimiwa, asilimia 7 kwa kweli bado mimi nasema kwamba hii Tume ya Utumishi kwa kweli hatukuitendea haki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza, sasa unatwambia tuendelee au vipi, sijakufahamu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Waziri, ameshasema yeye hana jawabu ya ziada ya hiyo, lakini ina maana kama hana jawabu ya ziada, ndio maana nikasema basi asilimia haikufika hata 10, hawa walikuwa wanafanya kazi vipi? Maana yake hili suala unajua Mheshimiwa, kwanza hawa wanaangalia maslahi ya hio idara maalum, na mimi ndio maana nilipokuwa katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kama ulifatilia zaidi suala la maslahi, mishahara na mambo mengine ya Idara Maalum mpaka Mhe. Rais alikuja kuyatolea kauli.

Kwa hiyo, ina maana hayakufanyiwa kazi ipasavyo. Sasa naomba kipindi hiki tunachokwenda nacho mheshimiwa, waingiziwe fedha ili sasa waweze kupendekeza serikalini namna gani haya maslahi ya idara maalum yatekelezwe,

otherwise, Mhe. Mwenyekiti, sijui hiyo kazi aliyoisema Mhe. Rais kwamba Idara Maalum atawaongezea mishahara, nani kule katika Idara Maalum atakwenda kukaa na kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ni maombi, kwa hiyo, uyapokee maombi aliyoyaomba kama una uwezo utaweza kuyafanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, napokea ombi lakini ni vizuri nitoe ufafanuzi, maana kusema kwamba sitakuwa na jibu, ina maana si kwamba sina cha kueleza.

Kwanza Tume hakuna kazi yake ambayo ilijipangia katika kipindi hiki ambayo imeshindwa kuifanya, imefanya shughuli zote. Na mimi nataka nimuhakikishie kuhusu maslahi ya watumishi wa Idara Maalum. Watumishi serikalini wamepatiwa nyongeza mara mbili, watumishi wa Idara Maalum wamepatiwa mara tatu kwa sababu ya tume hii kufanya kazi zake. Kwa hiyo, hakuna tatizo katika hali hii kwa sababu kazi zinaendelea kufanyika, na mimi nitafurahi sana nikiipata hiyo.

Lakini kama nilivyosema ukiangalia huu mtiririko basi sio tume tu ya Idara Maalum iliyopata asilimia ndogo, kuna taasisi nyengine chungumzima kutokana na huu ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, namuomba mheshimiwa kwamba, hakuna kazi iliyolala na kama alinisikiliza kwa makini tume hii pamoja na majukumu yake ni kufanya uwajiri wa wapiganaji. Mara ya mwisho imefanya kazi hiyo mwaka 2012/2013 haijafanya tena. Kwa hiyo, hizi kazi nyengine za kawaida wanazifanya kwa mujibu wa hali ilivyo na hakuna kazi. Nataka nimthibitishie kwamba hakuna kazi na wala maslahi ya mtumishi wa Idara Maalum yatakayokosekana kupatiwa kwa sababu wa ufinyu wa hii bajeti. Na ahadi ya Mhe. Rais kuwalipa mafao wapiganaji wa Idara Maalum kama alivyoahidi kwenye kampeni zetu za uchaguzi litafanyika kama alivyoahidi na fungu la fedha hizi hazipo hapa zipo kwenye lile fungu la mishahara ya serikali nzima. Kwa hiyo, Mhe. Hamza, asiwe na wasi wasi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri, lakini zaidi ya milioni 140,000,000 kama ziliingizwa milioni 7,000,000 na akasema kazi zote zilifanyika. Basi mimi nafikiri hata hizi walizoomba safari hii tuzipunguze, kwa sababu mimi ninavyojua *programme* ya *PBB* ni *programme* inayozingatia zile shughuli zenyewe. Kwa maana hiyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti. hoja yangu nafikiri umeilewa na wizara imeielewa hoja yangu, haja yangu wenzetu hawa waingiziwe fedha, tena naomba ile

kamati mkenda kwenye kamati hebu lifuatilieni, inawezekana hawa wenzetu wamefanya kazi. Unajua Askari anafanya kazi kwa *salute*, yaani kwa nidhamu, pengine wanadai marupurupu na wanasikitika hawasemi.

Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hili Waziri, nimemkubalia lakini Katibu Mkuu na yeye anasikia vizuri kwamba safari hii nataka, lakini bado Kamati hebu naomba waende wakaangalie hawa tume walifanya kazi zao vizuri, wanapewa bajeti hii. Ahsante Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu PD3103

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nilimuuliza Mhe. Waziri, aje anipe majibu kuhusiana na suala la ajira ndani ya miaka mitano, mwaka 2010 mpaka 2015 tunaenda 2016. Ni ajira ngapi Wizara yake imezalisha na wanapotaka kutoa ajira au washajiandaa kutoa ajira, zile ajira wanazigawa kwa mafungu gani, tuseme kwa kila Mkoa au kila Wilaya ningependa kujuwa. Na vile vile ningependa kujuwa kwa upande wa Kaskazini hasa Jimbo langu la Chaani wananchi wa Chaani kaajiri wangapi katika vikosi kwa miaka hiyo niliyoitaja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe Mwenyekiti, kwanza Mhe. Nadir, aelewe, ajira hazitolewi kwa Ukanda wa Chaani, Tumbatu wala wapi. Kuna vigezo na taratibu zilizopo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, ndizo zinazofuatwa jinsi gani mtu anaweza kuwa na vigezo vya kuweza kuajiriwa. Lakini siwezi kumpa namba ya Askari tumeajiri wangapi, hilo kwanza alielewe, siwezi kabisa kabisa kutoa idadi ya Askari ambao tumeajiri. Lakini nilisema tuliajiri mwaka 2012/2013 hatujaajiri tena Mhe. Mwenyekiti, nilisema pale na nilimtaja yeye Mhe. Nadir kwamba, aliuliza suala hilo. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe.Mwenyekiti, kutokana na heshima ya Wizara yake na mimi sitotaka tena kujuwa idadi gani kaajiri, lakini kwenye Jimbo langu la Chaani nina vijana ambao wana-*fit*, kwa hivyo, vielelezo anavyovisema, je, nikimletea vijana mia ataweza kuajiri wangapi katika hao?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, hilo si swali sasa, Mhe. Nadir, naomba tuendelee, naomba tuendelee, tuendelee.

Kifungu PD0103	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Idara Maalum za SMZ	
Kifungu SD010301	Programu Ndogo ya Usimamizi Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ	115,232,000
	Jumla Kuu	**115,232,000**

Kifungu PD0104	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara za SMZ	
Kifungu SD010401	Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Tafiti kwa ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	18,286,501,000
Kifungu SD010402	Programu Ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na IdaraMaalum	1,111,017,000
Kifungu SD010403	Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum - Pemba	511,918,000
	Jumla	19,909,435,000
	Jumla Kuu	**22,461,300.000**

FUNGU D02	JESHI LA KUJENGA UCHUMI	
Kifungu D0201	*Administration* Unguja	44,400.000
	Jumla Kuu	**44,400.000**

FUNGU D02	JESHI LA KUJENGA UCHUMI	
Kifungu PD0201	Programu Kuu ya Uzalendo, Uzalishaji Kazi za Amali na Michezo	
Kifungu SD020101	Programu Ndogo ya uzalendo, Uzalishaji na Michezo	

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kidogo kutilia mkazo hapa juu ya suala nililozungumza kuhusiana na matrekta ya Mbweni na nilisema kwamba, japo kuwa kwamba lile eneo lipo chini ya nafikiri sasa Wizara ya Elimu, lakini kuunganisha masuala hawa vijana wetu wa JKU pamoja na Chuo cha Karume, Karume *Institute of Science and Technology* ili kuhakikisha kwamba tunajenga *Garage* ya kisasa kwa miaka ya mbele na kuhakikisha kwamba magari ya Serikali pia hayatahamishwa ili kuongeza ajira na tija na kuokoa mapato ya Serikali kwa kutumia ile Karakana

ya Matrekta ya Mbweni, kama uwezekano itawezekana nasimamia hoja yangu, naomba tuendelee. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, alikuwa anatoa ushauri tu, kwa hivyo, tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mheshimiwa, nilikuwa nishatoa ushauri, nilikuwa natilia mkazo wazo langu kutokana kwamba Serikali ipo hapa, wote naamini wamenisikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, mkazo umekubaliwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante. nashukuru kwa mkazo huo.

Kifungu SD020101	Programu Ndogo ya Uzalendo, Uzalishaji na Michezo	32,000,000
Kifungu SD020102	Programu Ndogo ya Ufundi na Kazi za Amali	17,000,000
	Jumla	49,000,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu PD0202 Programu Kuu ya Ulinzi Mipango na Uendeshaji wa JKU

Kifungu SD020201	Programu Ndogo ya Ulinzi, Mipango na Uendeshaji wa JKU	11,407,400.000
	Jumla Kuu	**11,407,400.000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

FUNGU D03	CHUO CHA MAFUNZO	
Kifungu D0301	Sheria na Urekebishaji	60,578,000
	Jumla Kuu	**60,578,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu PD0301 Programu Kuu ya Huduma za Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilikuta bajeti ndogo sana ya uendeshaji katika Chuo cha mafunzo na nikamshauri Mhe. Waziri, jinsi ya kuendeleza mabwawa ya samaki na mashamba ya kuweza kukodi vitu vya matunda ili kuweza kupeleka Mafunzo ili kuweza kutumia pesa nyengine zile ambazo za *OC* kuzitumia kwa mambo mengine. Sasa nilikuwa naomba *commitment* ya Serikali wamefanya nini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mohammed Said Dimwa, aliuliza suala hilo na ilikuwa tayari kumjibu. Kwanza ninataka nimuhakikishie kwenye shamba la samaki kwenye kituo chetu cha Bumbwini nimeshafika zaidi ya mara moja.Nadhani alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tuliwahi kubadilishana mawazo kuhusu mpango wa kuliendeleza lile eneo. Kwa hiyo, ushauri wake kama alivyoutoa tangu huko nyuma na sasa anauweka katika msisitizo tutaendelea kuuchukuwa na kuufanyia kazi ili lengo lililokusudiwa katika shamba lile la ufugaji wa samaki tuweze kuliendeleza na tuweze kupata mafanikio yale yaliyokusudiwa.Na ushauri wake wa kukodisha miti ya matunda tunauchukuwa na nitaweza kuufanyia kazi kwa kushirikiana na Kamishna wa Mafunzo. (*Makofi*)

Kifungu PD0301 Programu Kuu ya Huduma za Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo

Kifungu SD030101	Programu Ndogo ya Huduma za Urekebishaji wa Wanafunzi	1,218,895,000
Jumla ya Kifungu		**1,218,895,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu PD0302	Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo	
Kifungu DS030201	Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo	8,001,105,000
Jumla Kuu		**9,220,000,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

FUNGU D04	KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO	
Kifungu D0401	Utawala Unguja	31,005,000
	Jumla Kuu	**31,005,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

FUNGU D034 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO
Kifungu PD0401

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mhe. Waziri, katika kuchangia nilimuuliza swali aje anielezee kutokana na hawa kikosi cha KMKM kina umuhimu wake na kwa kuwa vifaa walivyokuwa na haba na kwenye kazi zao vinatakiwa vifaa vinavyokwenda *speed* na vya kisasa. Nilimuuliza Mhe. Waziri, mpaka hivi sasa kikosi cha KMKM kina boti ngapi, zina *speed* gani hizo boti na kiwango gani na wana mpango gani wa kuwaongezea boti nyengine ambazo zitakuwa za *speed* na zinazoweza kuzuia magendo, kwa sababu kazi hizi ni kazi za hatari na ni kazi za kijangili wanatakiwa wawe na vifaa vya kisasa. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, kaa kitako. Wakati Mhe. Waziri, alipokuwa anajibu hoja kuna baadhi ya mambo alisema hasa yanayohusiana na ulinzi wa nchi, hayawezi kuelezwa na kutolewa taarifa zake hapa mbele ya kadam nasi. Mhe. Nadir, nakupa mfano sisi tulikwenda Pemba katika kikosi cha KMKM kama Kamati, lakini hatukupata taarifa hizo ambazo unazitaka wewe, tuliambiwa hilo haliwezekani, labda nimuachie Mhe. Waziri, lakini alishasema suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, maelezo yako ni sahihi, lakini yeyote anayetaka kutuangalia ajaribu kutuchezea, ataona kali yetu. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, hilo jibu Mhe. Waziri, atakuwa anajibu mimi, lakini lengo langu sio kwenda kuchezea KMKM, lengo langu ni kuwaombea, isipokuwa mimi nilikuwa nimeenda kusali na ninachowaombea wanunuliwe pia *helicopter* ya kulinda mambo ya magendo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti, mimi katika kifungu hichi nilizungumza pale juu ya suala zima la Askari wa Kikosi cha Kuzuia Magendo wanapokwenda kozi kule huwa wanalipishwa elfu sabiini za

magodoro, hili nafikiri Mhe. Waziri. hakunipa jibu, naomba anipe jibu halafu tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba ukimya wenu ili Mhe. Waziri, aweze kusikia masuala. Mhe. Waziri, unayo majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningemuomba Mjumbe akanipa hizo taarifa yeye kapewa na nani? Maana hizi ni taarifa za maadili za Askari. Sasa si vizuri kila kitu unachokisikia kuja kukihoji hapa. Nimuombe sana kama anazo hizo taarifa anitafute, kwa sababu kuna maadili, kuna utaratibu, kuna kanuni, unapojiunga katika kikosi chochote cha ulinzi kuna masharti yake, sasa kama umekubaliana na hayo masharti huwezi tena kuja kuhoji. Kwa hiyo, mimi nadhani Mheshimiwa, hili suala angeliacha nisingepaswa tena kusema maneno mengine ambayo hayastahiki kuyasema hapa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika mchango wangu niliongea kwa haraka masuala haya, niligusia kupata taarifa lakini muda haukutosha na napenda kusisitiza tena suala la *fishing using dynamite* kwa upande wa kusini Unguja na upande wa Peka-Pemba limeongezeka na wanaohusika pia kuna watu tafauti. Napenda katika suala hili na kama nilivyolizungumza kutokanana muda haukutosha, nalitilia mkazo tena kwamba Serikali yote ipo hapa lilibebe hili ni jambo muhimu sana kwa sababu vizazi vyetu mbele vitakuja kutulaumu, mabomu yanaongezeka yanafika mpaka kumi hasa kwa upande wa Kizimkazi mpaka kwenda chini karibia na upande wa Fumba kwa nyuma huku chini na upande wa Peka. Ahsante, tuendelee.

Kifungu PD0401 Programu Kuu ya Ulinzi

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii kidogo ya kutoa maelezo juu ya mchango wangu. Mimi langu ni ombi ambalo nililipeleka kwa Mhe. Waziri, kuhusiana na kituo cha KMKM kilichopo katika Jimbo langu cha Msumba, kwamba angalau nataka nipate kauli yake kwa sababu kituo kile kiko kwenye hatari ya kuharibika kutokana na mabadiliko ya hali ya tabia nchi, bahari imekula sana kile kituo eneo la ardhi, hilo la kwanza na wavuvi na wachuuzi wanafanya shughuli zao karibu na kile kituo na kituo ni kama tunavyokijua kama tunavyosema ni kitu cha siri. Kwa hiyo, ningependa Mhe. Waziri, anipe angalau maneno na mimi nipate la kushika kuhusiana na pale, ni lini wale wavuvi na wachuuzi watahamishwa

kutoka pale kuingia kwenye soko ambalo tayari limejengwa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho nilisema kwamba, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya tayari wamechukua hatua za kuweza kuwaondosha hao watu na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Suala la mmong'onyoko pia nililizungumza na mimi kama nilivyomwambia kabla tukimaliza bajeti tukijaaliwa tutafuatana mimi na yeye tukaone ili tuone hatua gani tunaweza tukazichukua katika kuhami huo mmong'onyoko kama nilivyosema pale.

Mhe. Omar Seif Abeid: Nashukuru sana, tuendelee.

Kifungu PD 0401	Programu Kuu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo	
Kifungu SD040101	Programu Ndogo ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo	964,700,000

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, umechelewa. Waheshimiwa, muwe katika vifungu ambavyo mnataka kupiga buti, lakini jengine fungu hili tayari watu watatu wameshalipigia buti, kwa hiyo, hatuwezi kuendelea.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, samahani, najua kidogo hapa napata mashaka, hapa mimi ninavyoona kwamba tunajadili na kupitisha vifungu katika wizara husika ambayo tunayo sasa hivi. Lakini kinachonipa mashaka baadhi ya Wajumbe wengine wanapohoji kunakuwa na kauli kwamba hapa hapahusiki, kwamba kunaonekana kuwa mengine hatupaswi kuyajua hapa.

Vile vile, mimi nadhani tupate muongozo, najua kwamba upya unachangia, lakini pamoja na hayo tukifika lile eneo ambalo halipaswi kuhojiwa basi kutoke ishara fulani ambayo tuweze kuendelea tu kusiwe na labda mtu anataka kujua hatimaye tena kukawa na jibu jengine ambalo kwa kweli pengine nadhani Wajumbe inaweza kuonekana kuwa baadae halitatenda haki. Kwa sababu yale maeneo ambayo ni hatarishi au ni nyeti basi tukifika katika maeneo yale kutolewe ishara tuweze kuendelea ili tusipate kuhoji. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hili tulikuwa tumeshalimaliza, unalipa maelezo makubwa tumeshafahamiana hapa na tumemaliza, tunaendelea. Naomba tuendelee.

Jumla ya Kifungu: **964,700,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0402 Programu Kuu ya Utawala

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi fursa kumuuliza Mhe. Waziri, swali dogo. Wakati nilipokuwa nikichangia nimemuuliza katika kile Kituo cha Afya KMKM kwamba, mwaka jana kilikuwa hakina daktari wa uchunguzi anayetumia vifaa vya kisasa (*X-Ray*). Je, huyu daktari amepatikana au laa, sikupata ufafanuzi wowote wakati wa kufanya majumuisho.

Mhe. Mwenyekiti: Anachokisema Mhe. Waziri kwamba, amekuliza kulikuwa na daktari wa kufanya uchunguzi (*X-Ray*) ambaye alikuwa bado hajapatikana, sasa ameuliza je ,keshapatikana sasa hivi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetupatia kibali cha kuajiri madaktari katika Hospitali ya KMKM akiwemo na daktari huyo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PD 0402 Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM

Kifungu SD 040201 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM 15,411,800,000

Jumla ya Kifungu: **15,411,800,000**

Jumla Kuu: **16,376,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D05 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu D0501	Utawala Unguja	21,084,000
	Jumla Kuu	**21,084,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D05 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu PD0501

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilikuwa nikionesha wasi wasi wangu mkubwa sana juu ya makaazi ya askari wetu wa Zimamoto Wete Pemba. La kwanza. La pili, nilishauri serikali juu ya kuwafanyia mafunzo madogo wafanyakazi wa idara mbali mbali juu ya kupigana na moto na kutumia *fire extinguishers,* sikupata jibu langu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nilisema ushauri huu tumeupokea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PD0501	Programu Kuu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	
Kifungu SD050101	Programu Ndogo ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	268,404,000
	Jumla ya Kifungu:	**268,404,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD0502 Programu Kuu ya Kukuza Huduma za Kiutawala, Mafunzo, Kiutendaji, Mipango na Uongozi kwa wafanyakazi wa Zimamoto Kifungu SD

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nilipozungumza wakati wa kuchangia nilizungumza Kituo cha Zimamoto cha Chake Chake. Nilizungumza kwa ufanisi na kwa mambo yanavyoendelea kile kituo ni kidogo na bado eneo

lipo ambalo linahitaji kuongezwa kwa ufanisi zaidi. Je, Mhe. Waziri, hili kalionaje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Suleimani Sarahan, Kitumbatu Selemani, kwa hiyo, aniwiye radhi kidogo nimekwenda kwenye lafudhi yangu ya Kitumbatu. Ni kweli alipozungumza alitoa ushauri huu na kwa sababu ya muda sikuweza kumjibu, lakini kweli hilo jambo lipo na tunalifanyia kazi na yako baadhi ya maeneo ambayo tumeanza kuyalipia fidia na kuyaingiza katika eneo lile la Chanjaani. Kwa hiyo, ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi, ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PD0501	Programu Kuu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	
Kifungu SD050101	Programu Ndogo ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	268,404,000
	Jumla ya Kifungu:	**268,404,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD0502	Programu ya Kukuza Huduma za Utawala, Mafunzo, Kiutendaji Mipango na Uongozi kwa Wafanyakazi wa Zimamoto	
Kifungu SD050201	Programu Ndogo ya Kukuza Huduma za Kiutawala, Mafunzo, Kiutendaji Mipango na Uongozi kwa Wafanyakazi wa Zimamoto 4,642,696,000	
	Jumla ya Kifungu:	**4,642,696,000**
	Jumla Kuu:	**4,911,100,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D06 KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu PD0601 Utawala Unguja

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kupata ufafanuzi wa masuala yangu ambayo niliyauliza.

Mhe. Mwenyekiti, niliuliza masuala mengi na Mhe. Waziri, alinijibu kwa mujibu wa maadili hawezi akanijibu hapa, lakini hiyo haisababishi masuala yangu yasijibiwe. Sisi tunafanya kazi kwa mujibu wa Katiba, kanuni na sheria mbali mbali ambazo na sisi zinatulinda kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, yale mengine nitaiachia kamati iende ikafuatilie na nitawapa *records* zote zile wakafuatilie na kwa sababu hayo ni mambo ya utawala.

Mhe. Mwenyekiti, tusikinge sana vifua kwa kuwa ndugu zetu hawa Idara Maalumu, Vikosi mambo yao siri na nyeti, sio yote yaliyokuwa siri, yako mambo ambayo yanatakiwa tupate maelezo hasa tunapoona mambo ya utendaji ambayo hayaturidhishi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nataka nipate ufafanuzi katika ukurasa wa 56 wa kitabu cha Mhe. Waziri, tunatoka 55 kwenda 56, naomba nikisome chote ili Mhe. Waziri, anifahamu; "Fungu nambari D6 lenye jumla ya programu kuu mbili linalosimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Valantia kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imepangiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni saba na nyengine hizo zilizotajwa hapo".

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa, najenga hoja kwenye hotuba ya waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, lakini hapa unajua kama tuko kwenye mapato, unatoa hoja ya matumizi kwenye mapato?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mwisho wake iko mapato hapo. Kwa sababu kuna matumizi waliyokadiria halafu kuna mapato ya kukusanya. Sasa nakuja katika hiyo ya mapato ili kuokoa muda. "Hivyo, naliomba Baraza lako liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato wa shilingi 21,084,000 kupitia programu za kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali".

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika hili tabu kubwa kuna shilingi 17,000 halafu juu kuna 03 kwa utaratibu wetu, ina maana ni milioni 15/16, 16/17 wamepangiwa 21 milioni. Sasa Mhe. Mwenyekiti, yale aliyoyaeleza kwamba

wataniita nikatoe maelezo hiyo kazi nitawaachia wenyewe, lakini hapa nataka hili suala zima la mapato.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mapato mimi kamati yangu inasimamia Wizara ya Mawasiliano na tulipokuwa katika ziara zetu mbali mbali tulipita katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na sasa hivi pale pana ulinzi na wakatwambia kwamba wao wanalipa shilingi 20 milioni kwa mwezi. Sasa hapa katika maombi aliyotuomba Mhe. Waziri, ametuomba kumuidhinishia akusanye shilingi 21 milioni kwa mwaka. Sasa hapa hii ndio hoja yangu na ndio maana nikasema sio lindo hili tu, kuna malindo mengine ambayo yanalipwa hiyo sio siri.

Sasa Mhe. Waziri, labda anipe maelezo kwamba, je, hili fungu ndilo alilikusudia shilingi 21 milioni tuwaruhusu na je, hayo malindo mengine hayo malipo yanayolipwa yanakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mapato haya yaliopo hapa ni mapato ambayo Idara ya Kikosi cha Valantia kimetakiwa kichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, haimaanishi kwamba hakuna mapato, kikosi hiki kama vikosi vyengine ambavyo havikusanyi, vinakusanya. Lakini serikali kwa sababu ya umuhimu wa matumizi yao na saa nyengine *OC* zinachelewa wameruhusiwa mapato hayo kuyatumia na utaratibu nilisema pale, utaratibu uko wazi kwamba itakapofika muda wa utaratibu wa kisheria *auditor* anakwenda kukagua hesabu zao na taarifa yake inaletwa kwenye Baraza la Wawakilishi, ikishakuletwa hapa, tunaipokea Mhe. Spika, au Baraza linakabidhi Kamati ya *PAC* na Kamati ya *PAC* inakwenda kukagua ama Kamati ya Kisekta inao wajibu wa kwenda kuhoji na baadae taarifa zake zinaletwa hapa.

Kwa hiyo, haya yaliopo hapa ni mapato ambayo miongoni mwa hayo mapato mengi ambayo wanayapata, lakini katika hayo mapato wametakiwa haya wachangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mapato yao mengine wameruhusiwa kuyatumia na ukifika muda wa kwenda kukagua wanayatumiaje? Ruhusa hiyo ipo, ipo kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, ipo kwa *PAC* na hatimaye Baraza hili litapata taarifa rasmi ya namna gani ya matumizi hayo yamekwenda. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hebu labda nipate utaratibu pengine Waziri wa Fedha anaweza akanisaidia. Kuna fomula gani ya hizi taasisi zinazokusanya mapato kuwasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa

sababu kama taasisi inakusanya shilingi 20 milioni kwa mwezi, halafu kwa mwaka mzima wapeleke Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 21 milioni, mimi nafikiri lazima tuwe na *consistency* katika vigezo, maana yake najua kuna mashirika, kuna taasisi labda tuambiwe kuna vigezo gani vinavyotumika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hizi fedha, maana yake kama nitakuwa sikupata maelezo zaidi ina maana hili fungu itabidi sasa tuongeze makusanyo, tuongeze fedha zitazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa sababu haiwezekani katika mapato ya mwaka mzima lindo moja tu iwe mwezi mmoja tu ndio unakwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na wakati kuna malindo tofauti. Kuna *ZSSF, ZRB*, kuna wapi na wapi. Hebu Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya utaratibu, maana yake isiwe tu anaambiwa wewe changia hiki, wewe hiki, inawezekana pengine wana majengo na majengo ya KVZ mimi nayajua, yako hali mbaya sana. Kwa hivyo, fedha hizi kama nitaambiwa zimepangiwa programu moja, mbili, tatu ya kujenga majengo nitakuwa sina tatizo, lakini nataka hii fomula iliyotumika kwa idara zetu zinazokusanya fedha kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hii tunayoifanyia kazi sasa hivi ni Kamati ya Matumizi na wala sio Kamati ya Mapato. Suala la kuidhinisha mapato lilishapita kwenye Bajeti Kuu ya Serikali, yale makusanyo na tuliridhia hapa na tutakwenda tena kutakuja mswada tutaupitisha, hii ni Kamati ya Matumizi. Sasa utaratibu anaotaka kuuhoji katika fungu hili haupo, huo ndio ukweli Mhe. Hamza, tunakwenda kinyume na Kanuni. Mhe. Mwenyekiti, sasa usiruhusu tu ukavunja utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, kama alivyosema Mhe. Waziri, kwamba kiutaratibu hii ni Kamati ya Matumizi, kwa hiyo, wewe umeulizia mapato ambayo tayari tumeshapitisha. Haya ni mapato na nilikwambia tangu mwanzo kwamba hapa tunazungumzia suala la mapato katika kifungu hiki. Lakini sasa hata hivyo, mimi nafikiri Mhe. Waziri, ni vizuri na yeye akapata maelezo mazuri ili akafahamu mara nyengine tena asije akarudia kosa hilo ambalo analifanya sasa hivi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi naheshimu sana maelekezo yako na mimi huwa namfatilia sana kwanza Mhe. Hamza Hassan Juma, ni Mwakilishi hodari sana wa kutaka tufate utaratibu kwa mujibu wa sheria na katiba. Tusiridhiane katika kufuata utaratibu.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, hicho anachokisema hichi ndicho tulichopangiwa kukionesha, tungepangiwa tuoneshe bilioni hamsini kama tunazo tungeziandika na zingeonekana hapa. Lakini tumepangiwa ishirini na moja, sasa kama kuna taarifa nyengine ambazo yeye anazijua, maana ametoa taarifa hapa za ukusanyaji wa mapato wa milioni ishirini kwenye mamlaka, nataka nimuarifu hizo pesa sisi hatujalipwa na wako askari pale bataliani nzima wanalinda, tunatumia gharama zetu, mafuta, chakula na mambo yote na pesa mamlaka hawajatulipa. Sasa tunafanya kwa madhumuni ya kuitumikia nchi yetu.

Sasa na huu utaratibu umeidhinishwa rasmi na Wizara ya Fedha kwamba, wanachokikusanya baadhi yao wakitumie wao wenyewe. Sasa anapotaka mimi nije hapa niseme, kwa nini hizo nyengine hazijaja ndio utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapa naona nasoma muhtasari wa Makadirio na Mapato, haya ndio mapato ambayo tunayoyaidhinisha. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuna mambo mawili; suala la hoja yangu nafikiri imeeleweka kwamba mapato haya ambayo yanakusanywa Wizara ya Fedha, haya kwa kweli kwa uono wangu haya mapato ni madogo yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Nilitaka nipate utaratibu.

Utaratibu nikipewa hautolifumua fungu hili, hautoliongeza wala kulipunguza, nilitaka nipate utaratibu wa hizo taasisi zinavyotakiwa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Je, kuna asilimia au inaangaliwa mazingira yale ambayo yanayopaswa. Lakini hili ambalo alilojibu Mhe. Waziri, pia na mimi amenisaidia kwa sababu na mimi hiyo taasisi, yaani yangu hiyo Mamlaka ya Anga iko chini ya kamati yangu. Kwa hiyo, nitapata kwenda kuuliza kwamba wao wanasema pesa wanapeleka huku hazijafika.

Pia, na mimi amenisaidia kazi nitapata kujua hizi pesa ziko wapi mpaka sasa hivi. Lakini bado naomba tena Mhe. Mwenyekiti, nipate kigezo cha utaratibu na ndio maana hili suala nililenga moja kwa moja Mhe. Waziri wa Fedha, kama kuna kigezo na kama hakipo basi. Na hiyo basi yenyewe pia nitaomba nisimame tena kama itakuwa hakuna kigezo, basi niwaachie kamati waende wakalifuatilie suala hili. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Waziri, tusaidieni kwa hili, nafikiri labda Mhe. Mwanasheria Mkuu, utusaidie kwa hili. Mhe. Hamza Hassan Juma, anataka kigezo, nafikiri umeelewa vizuri suala lake naomba utusaidie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Hamza Hassan Juma, anachotaka kujua kama kuna kigezo ambacho kimewekwa na serikali kwa hizi taasisi au wizara ambazo zinachangia kwenye Bajeti ya Serikali. Labda tu nimwambie kwamba kwa sasa hakuna kigezo ambacho kimewekwa. Kwa sababu haya ni makusanyo yanayofanywa wale ambao wanatakiwa kuchangia yanakadiria kwamba kwa mwaka fulani wa fedha wao wanaweza wakachangia serikalini kiasi gani na utaratibu uliobaki wa matumizi nadhani Mhe. Waziri, ameueleza vizuri. Kama zile ambazo wanachangia kuna nyengine zinabaki kwa njia ya *retention* ili waweze kufanya kazi zao na zile ambazo nyengine zinakwenda sasa kwenye Mfuko wa Serikali ili kusaidia matumizi ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na serikali yetu mfumo tunaokwenda nao sasa hivi wa kudhibiti mapato. Na hapa tumeona ni namna gani fedha nyingi tunazikusanya, lakini bado katika utaratibu wa kutumia kuna tatizo kidogo. Sasa bado hili suala langu nitaomba tuendelee lakini naomba Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii hili ende akalifuatilie na akalifuatilie kwanza na leo tunazungumza tarehe 06/06/2017 na tutafanya *cross check* na mimi katika wizara yangu kule Mamlaka ya Anga fedha zilianza kutoka lini na kule KVZ hazijafika, zimefikia wapi.

Lakini vile vile baadae Wizara ya Fedha, pia wajaribu kuangalia haya makusanyo namna gani waelekeze kwa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini bado nitaridhika vile vile kama kuna *retention*, mimi sikatai kwa sababu bado majengo ya KVZ ukiangalia na hata utaratibu na *uniform* na mambo mengine hawako vizuri sana. Kama *retention* imeeleza vizuri wazitumie sina tatizo kwa sababu nataka kuboresha, sio fedha iende Mfuko Mkuu wa Serikali. Tunataka kuboresha vikosi vyetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee. (*Makofi*)

Kifungu D 0601	Utawala Unguja	21, 084,000
	Jumla Kuu	**21,084,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D 06 KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu PD 0601	Program ya Amani na Utulivu kwa Taifa Raia na Mali zao

Kifungu SD 060101	Programu ndogo ya Amani na Utulivu kwa Taifa raia na mali zao	358,000,000
Kifungu PD0602	**Program ya usimamizi na utawala wa kikosi cha Valantia**	
Kifungu SD 0602	Programu ya usimamizi na utawala wa kikosi cha Valantia	7,169,100,000
	Jumla Kuu	**7,527,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D07 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Kifungu PD 0701	*Planning and Policy*	35,989,000
	Jumla Kuu	**35,989,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D 07 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Kifungu PD 0701	Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo

Mhe. Abdallah Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina makubwa sana, isipokuwa nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa ukakamavu wake wa kujibu maswali. Lakini mimi katika kuchangia hotuba hii alieleza barabara nyingi sana ambazo zitakazopata manufaa zile *FIDA road*, nikauliza na barabara ya kwangu Kidongo Chekundu ipi, kwa sababu pale pana barabara tatu, hasa ipi moja wapo, mimi naomba Mhe. Waziri, anambie ili tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hebu rudia tena ulichokisema, maana naona waziri hajakusikia vizuri.

Mhe. Abdallah Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika kuchangia nilichangia kipengele kwenye kitabu chake 126 juu ya zile barabara za *feeder roads* ambapo zinatengenezwa na Halmashauri. Kwa hiyo, kuna barabara nyingi alizitaja pale lakini kwa mimi nilipata faraja barabara ya Kidongo Chekundu. Je, ni ipi moja wapo, maana mimi nina barabara tatu ndogo. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri, anijuilishe halafu tuendelee, basi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sikupata fursa ya kujibu au kutoa ufafanuzi katika suala la Mhe. Abdalla Maulid Diwani, ambalo aliliuliza kwa sababu ya muda.

Lakini barabara ambavyo itafanyiwa matengenezo au barabara ambazo zimetembelewa ya Kidogo Chekundu ni ile kutoka Kidongo Chekundu msikitini kupitia Homoud, ndio iliyokuwa ikiitwa Homuod Kidongo Chekundu skuli mpaka kutokezea Jang'ombe kuelekea Mpendae.

Kifungu PD 0701	**Programu Kuu ya uratibu wa shughuli za Maendeleo**	
Kifungu PD 070101	Programu Kuu ya uratibu wa shughuli za Maendeleo ya Mkoa	240,388,000

Kifungu PD0702 Programu Kuu

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati wa mchango wangu nilizungumza masuala ya ulinzi na usalama yapo chini ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na magari ya Baraza la Mji yanayotoka kubeba taka kutoka Mkoa wa Mjini kuelekea Mkoa ya Kusini yanapita barabara ya Fuoni yanakwenda kwa mwendo wa kasi, yanahatarisha maisha ya watu na mali za watu pia na nikauliza haya magari kwamba kweli yana *insurance* na kama yana *insurance* ni *insurance* gani kama ni *comprehensive* ambayo pia panapotokezea ajali kutokana na mwendo wao kasi italazimika pia watu ambao watakaoathirika au kufa kuweza kulipwa.

Endapo kama halitafanyika hilo kama ajali haijatokezea, ina maana moja kwa moja au ajali ikitokezea ni kwamba serikali itabidi ilipe fungu katika kufidia wananchi ambapo mara nyingi zinakuwa zile fedha zinazopatikana sizo ambazo kama yale magari yana *insurance* yangepata. Sasa nilikuwa nataka kujua kwenye suala zima la haya magari na ulinzi wa wananchi na mali zao ni *fomular* gani inayotumika katika kuwadhibiti hawa madereva na haya magari juu ya suala zima. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza magari yote ya Manispaa yanayo *insurance* na ni *comprehensive*. Lakini suala jengine ambalo amelisema la madereva kwenda mbio hiyo ni taarufa ambayo tunayo miezi miwili nyumba na uongozi wa Baraza la Manispaa umechukuwa hatua ya kuweza kuwaonya madereva na vile vile hili ni jukumu la kikosi cha usalama barabarani, pale

watakapowaona kwamba wanakwenda kinyume na sheria wanahatarisha usalama wa raia majiani na usalama wao, basi tunawaomba au tunawahimiza watekeleze wajibu wao.

Lakini mara ya kwanza tulipolisikia hili jambo tulipeleka kwenye Baraza la Manispaa na Baraza la Manispaa limekaa na madereva wao na wameweza kuzungumza nao na wale ambao watakwenda kinyume na hayo maelekezo basi hatua za kinidhamu zinatachukuliwa dhidi yao. Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwa majibu ya Mhe. Waziri. Lakini napenda kusisitiza kwamba hili jambo bado linaendelea na mimi mwenyewe nimeshalidhuhudia mara nyingi napita barabara ya Fuoni hasa kutokana na mazingira ya barabara ilivyo sasa hivi, wanapita wao kama ni wafalme njiani na wanakwenda mwendo wa kasi, ni hatari sana na ni kitu ambacho tunasubiri jambo litokezee wakati wowote.
Mimi naomba utaratibu wa kisheria au wa kinidhamu uchukuliwe haraka sana ili hili jambo litokomezwe moja kwa moja mara moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomna tuendelee.

Kifungu PD0702 Programu kuu ya usimamizi na Utawala wa Mkoa		
Kifungu SD070201	Programu ndogo ya Utawala na Uongozi wa Mkoa	1,396,812,000
	Jumla Kuu	**1,637,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD0801

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa wakati natoa mchango wangu nilizungumza umuhimu wa kujenga masoko katika maeneo tofauti na hili jambo kwa kweli limo ndani ya moyo wangu na wananchi wangu wanalisubiri kwa hamu na karibu Mhe. Naibu Waziri, anayeshughulikia masuala la kilimo alikiri katika maswali na majibu asubuhi kwamba ziko tayari ramani zimeshatayarishwa katika masoko maeneo tofauti likiwemo Kivunge, alizungumza sijui na Mahonda.

Lakini nazungumzia kwa Mkoa wa Kusini suala la Kaebona pamoja na Dunga mitini hasa Kaebona. Sasa ningeomba Mhe. Waziri, afuatilie katika hizo ramani zilizoyatarishwa katika wizara ya Kilimo ili zifikie kwenye

Halmashauri yetu kwa vile hapa tuna Mkuu wa Wilaya ya Kati Mhe. Mashavu Sukwa ni jembe, tuanze kazi mara moja ya maendeleo kusogeza huduma za wananchi Mkoa wetu wa Kusini.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, tuendelee Mheshimiwa?

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, alifuatilie hilo suala la ramani zifike kwenye Wilaya zetu ili Mkuu wetu wa Wilaya aweze kufuatilia na sisi wananchi tuweze kusaidia. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, umeombwa ufuatilie hili suala. Una jibu lolote au una suala lolote.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza shughuli ya masoko ni shughuli ya ofisi yangu rasmi kwa mujibu wa sheria na huo ni wajibu wangu, sihitaji kuhimizwa. (*Makofi*)

Lakini pili katika jimbo lake hilo soko analolizungumzia Halmashauri ya Wilaya ya Kati ilitoa msaada wa kuweza hasa hilo la Kaebona. Ilitoa msaada wa kwenda kuliwezeka baada ya kuunga nguvu za wananchi. Lakini pia alizungumzia, amesahau kwamba, je, serikali ina mpango gani wa kuweza kujenga soko katika maeneo ya Dunga mitini. Nadhani katika *Hansard* kama nimeona kitu kama hicho. Je, serikali ina mpango gani.

Serikali kweli ilitaka kujenga soko katika eneo la Dunga mitini, lakini ikaona kwamba soko lile litakuwa barabarani na nyuma kuna maeneo ya watu. Kwa hiyo, serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi inatafuta eneo jengine kwa nia ile ile aliyoisema Mhe. Mwakilishi Simai Mohammed Said (Mpakabasi) kwa ajili ya kuwepo na soko litakalowaunganisha watu wa Mkowa wa Kusini.
Sasa na kwa sababu nilitoa maelezo ya kutosha ni kwa jinsi gani maendeleo yoyote yanatakiwa yafanyike na kwa sababu hayo maendeleo pia yatakapofikiriwa huko *grass root* yatafika kwenye kamati ya *RDC* na yeye akiwa Mjumbe. Nadhani hapo sasa patakuwa pahala mazuri pa kuweza kutoa wazo la wapi kujenga soko. Afisi yangu iko tayari, inapokea ushauri wake. Lakini kwa sababu alilichangia nimesema ni vizuri nilitolee maelezo.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri kwamba, kuhimizwa ni

wajibu wake yeye anautambua, lakini na sisi pia ma-*back benchers* ni wajibu kuhimiza serikali. Hilo la kwanza.

Namuomba Mhe. Waziri, alitambue hilo vizuri kabisa kwamba sisi ma- *back benchers* tutaendelea kuhimiza wananchi kwa sababu sera yetu ya Chama cha Mapinduzi, "Hapa kazi tu". Hilo la kwanza.(*Makofi*)

Lakini pia hiyo ramani ambayo ninayoizungumza mimi, tulizungumza katika maswali na majibu na eneo ambalo nimezungumza *specifically* siyo kwamba la kuwekeza, ni katika soko jipya ambalo lilikuwa limezungumzwa katika eneo la Kaebona ambalo litaunganisha wananchi wa Mkoa wa Kusini wote kwa jumla, pamoja na majimbo ya Paje, Makunduchi, Kae Pwani Tindini pamoja na Kikungwi. Kwa hivyo, hili ni soko jipya, sio soko ambalo tunataka tuje tuwekewe mabati. Mimi ninachoomba ni kwamba nitamtafuta mimi kwa muda wangu pamoja na Wizara ya Kilimo kuangalia hizo ramani, pengine inawezekana hizo ramani ni masoko ya Kaskazini bado la kwetu halijatayarishwa.

Hivyo, sitopenda kupoteza muda, akiri tu basi mimi nitamfuatilia, na nitaendelea kumuhimiza kila siku na sio leo. "Hapa kazi tu". Ahsante sana, tuendelee Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tunaendelea.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PD 0801 Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa Kusini Unguja	Shs.193,727,000/-
Kifungu PD 0802 Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala Mkoa wa Kusini Unguja	Shs.1,099,873,000/-
Jumla Kuu	**Shs.1,263,600,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 09 MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu D 0901 Mipango na Sera	Shs.4,790,000/-

Kifungu PD 0901 Programu...

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninasikitishwa sana na Mwenyekiti wa Halmashauri kuja kudanganya wananchi. Kwa kuwa Chama cha Mapinduzi hakina wanafiki wala waongo.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe.Waziri, aje anijuulishe mtu kama huyu anayepita, akatumia jina la wizara yake au Halmashauri yake kwenye kuzungumza uwongo atamchukulia hatua gani.

Suala langu jengine...

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa, hilo linahusiana na nini na kifungu hichi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, maendeleo ya Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh!

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Soko.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! Lakini lina husiana na nini? Nimekuuliza. Nenda kwenye programu usiende na kumzungumza mtu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Nipo kwenye programu.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! Sasa sema hicho ambacho wewe unakihisi kwamba ni cha uwongo, siyo mtu. Usimzungumze.

Waheshimiwa, tusikilizane, usimzungumze mtu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Nipo kwenye PD 0901 "Uratibu wa Shughuli za Maendeleo Ndani ya Mkoa wa Kaskazini". Na huu Mkoa ndipo mimi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kumuuliza Mhe. Waziri, soko la Kinyasini, nimeambiwa kwamba kuna wafadhili wameshatoa pesa. Ni kiasi gani pesa hizo zimelipwa na lini litaanza kujengwa.

Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ufafanuzi niliutoa pale kwenye *podium*. Kuwa namna gani soko la Kinyasini litajengwa.

Lakini mimi nimshauri Mhe. Nadir, hayupo hapa kwa ajili ya kumshutumu mtu ambaye hayumo humu. Kanuni zetu zinakataza kama ulivyomuelekeza na mimi nilisema, ninampa ushauri kama kuna sintofahamu, mimi nisingependa kuziingia. Nilichosema aliyekuwa Mwenyekiti, alipokwenda kuwaambia wananchi wa Kinyasini juu ya ujenzi wa soko hakudanganya. Kwa sababu soko linajengwa kuanzia tarehe mosi mwezi wa nane.

Na alisema Mhe. Nadir kwamba, sina hakika kama alisema, alisema kwenye kampeni zake za uchaguzi za kufunga kampeni, kama nimefahamu hivyo, kama sivyo anirekebishe.

Sasa ninataka nimuhakikishie kwamba soko la Kinyasini linajengwa na mkandarasi ameshapatikana na tarehe mosi mwezi wa nane sambamba na soko la *Qatar* linajengwa. Kwa hivyo, kama aliyekuwa Mwenyekiti, kenda kutoa tamko hilo, hakudanganya. (*Makofi*)

Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mwanzo Mhe.Waziri, aliposimama mbele alizungumza kwamba alienda kwa maslahi yake mwenyewe na hakumtuma, hiyo ninanukuu alivyozungumza huyo aliyekuwa Mwenyekiti. Lakini kama ni Mwenyekiti wa Halmashauri, kama ni muhusika wa Wizara bila shaka yeye Mhe. Waziri, linamuhusu.

Sasa hivi anasema kwamba anajaribu kumlinda kwamba hajasema uwongo. Mwanzo alizungumza kwamba alienda kwa niaba yake mwenyewe kudanganya. Sasa na alipokwenda kuahidi pale, aliahidi kwamba zile pesa zipo tayari kwenye Mfuko wa Halmashauri, hajazungumzia kwanza kwamba kuna mfuko utafadhiliwa.

Pili, Mhe. Waziri, ninamnukuu amesema siyo muda mrefu hapo nyuma kwamba, yeye alienda kwa maslahi yake mwenyewe binafsi yule kwenda kusema. Sasa hivi ananiambia kwamba, yaani hilo suala ni kweli. Sasa sijui nilifahamu vipi, lakini wacha liendelee tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, unajua ukiacha iendelee itaonekana kama taarifa siyo sahihi.

Nilipokuwa pale nilitamka sikumtuma hata kidogo na bado ninaendelea na msisitizo wangu kwamba sijamtuma. Hiyo taarifa ya kwamba aliyekuwa Mwenyekiti kenda kutoa tamko, amenijuulisha yeye jana baada ya kuchangia.

Lakini kama ni mipango ya Wizara na Mwenyekiti wakati huo hiyo mipango imepitia Halmashauri kama kenda kasema, ndiyo ninathibitisha kwamba hajafanya kosa kwa sababu soko linajengwa kweli. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Nadir, akitaka kuni-*drive* kwenye maeneo ambayo wao wana mambo yao, waende wakamalizane huko nje, siyo humu ndani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi huyu mtu sina matatizo naye. Lakini kwenye suala la ukweli nitazungumza ukweli, kwa sababu Wizara hii inamuhusu yeye. Bila shaka ata-*defend* tu, lakini ninachozungumza nimeuliza suala moja kwamba, kiasi gani kimesaidiwa na hawa watu binafsi kujengwa lile soko naomba anijibu. Kiasi gani kimesaidiwa kujengwa lile soko na la aina gani litajengwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tuendelee. Sasa unaongeza suala jengine juu yake. Ulisema mwenyewe tuendelee Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifingu PD0901 Programu Kuu ya Uratibu ya Shughuli Ndani ya Mkoa

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka maelezo kuhusu suala la mradi wa uzwaji wa taka. Kama alivyosema Mhe. Waziri, mimi ni Mtumbatu wa juu, yeye ni Mtumbatu wa kisiwani, tunajuana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika zile kampuni ambazo alizozitaja, hawa waliokuja kuleta malalamiko yao ni wale Kikundi cha 'Mungu Tusaidie'. Mhe. Mwenyekiti, Waziri, hasikii vizuri mnazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika hoja yao wanasema kwamba mipango ya serikali ni kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lakini hoja yao wanasema kwamba ile kazi walianza wao tokea mji ulikuwa eneo lilikuwa chafu wamejitahidi kuzoa taka, wakatengeneza mradi wao, wamepata ufadhili vile

vile kwa taasisi mbali mbali za kimataifa na mpaka wakaweza kuajiri watu zaidi karibu ishirini na tano.

Lakini hivi sasa kuna watoa huduma wa kigeni ambao ni raia wa kigeni ambao siyo Watanzania na siyo Wazanzibari kwamba, wamekuja sasa ile kazi wanaifanya wao. Mhe. Waziri, nimemsikiliza vizuri, akasema huu mradi wa hawa wageni akakiri kwamba wapo, lakini ubia pamoja na wananchi.

Suala hili Mhe. Mwenyekiti, nilikuta ninataka nipate ufafanuzi wa kina katika huo mkataba wa hao wananchi na hao wageni. Kwa sababu hili tumeliona mpaka katika sekta hii nyengine ya utalii. Kwenye sekta ya *Tour Operator* na wengine, kwamba zile kazi ambazo kwa mujibu wa sera zetu wanatakiwa wafanye wazalendo, wanakuja wageni pengine anamtafuta mtu mmoja pengine hana hisia ya aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, uliza swali, unaelezea mambo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa hivyo, swali hoja yangu nilikuwa ninataka je, katika huu mkataba wa hii kampuni ambayo tuliambiwa kuna ubia na wageni. Je, mkataba huu unasemaje? Hawa wageni wana asilimia ngapi na wenyeji wana asilimia ngapi.

Hoja yangu hapa tusipoke hapa ajira za wenyeji na kuwapa ajira hizo wageni. Ninataka jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Hamza, ambaye ni Mtumbatu wa juu, Mtumbatu mwenzangu. Amehamisha goli.

Hoja yake ilikuwa kwa nini kampuni za wazawa zinanyimwa kazi, zinapewa kampuni za wageni. Angetaka hizo *data* (takwimu) za *shares* ningekuja nazo na ndiyo maana alitoa hoja kwamba Baraza hili lisimalize kipindi cha asubuhi, ili sisi tupate muda tukaweze kujiandaa na hizo hoja ambazo wao watazitoa. Serikali ilikubali kwa moyo mkunjufu na tumewasikia. Hoja aliyoileta ni kwamba kuna kampuni ya wazawa imenyimwa kazi. Ndiyo maana nikasema, kwa hivyo, hiyo taarifa kama anaitaka nitamletea kwa maandishi. (*Makofi*)

Lakini kampuni ambayo amethibitisha kwamba ndiyo imetoa mashitaka hayo ya 'Mungu Tuafiki' tuna matatizo nayo, hawalipi kodi yetu. Sasa kwa sababu na wao ndiyo kampuni ambao wana hoteli nyingi zaidi za kuzifanyia kazi kuliko kampuni nyengine zote tano. Nilisema *ZanRicky* ambayo ina ubia na wenyeji,

kweli ina *share* na sikuwa na sababu ya kuficha wala kudanganya kwa sababu Baraza hili halidanganywi.

Na sheria inaruhusu kuwa na ubia wa wazawa na wenyeji. Sheria haikatazi lakini kuna kampuni ya Safina, yenyewe hiyo *ZanRicky* ina hoteli saba. *New* Safina inahudumia hoteli kumi na mbili. *H.K Traders* inahudumia hoteli saba, nilisema pale. *Masemo Traders* ina hoteli nne. Mungu Tuafiki ambayo haitulipi kodi zetu ina hoteli kumi na nane.

Sasa kwa lile alilolisema alo-*raise* hoja nyengine nitamletea kwa maandishi. Vile vile, ninatoa indhari kwamba huyu ambaye ana kampuni hii ambaye hatulipi pesa zetu, tukifika mwezi wa Julai hajalipa pesa hizi. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Baraza la Madiwani, kwa sababu maamuzi haya yalifanyika kwenye Baraza la Madiwani, kama hatulipi tutavunja naye mkataba. Tuitafute kampuni ambayo italipa kodi kwenye Halmashauri ili isaidie maendeleo ya watu wetu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza, tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea na wala usiwe na wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo niliyopata kwa Mhe. Waziri, yapo kinyume kidogo na hao wadau ambao walioleta hiyo hoja yao. Mhe.Waziri, ameniambia sasa hivi hawa 'Mungu Tuafiki' wana hoteli kumi na nane.

Kwa taarifa yao wao wameniambia wana hoteli nne. Sasa Mhe.Mwenyekiti, mimi unanijua mara nyingi ninashauri. Basi hii kamati ambayo inayohusika ya kitaasisi basi wajaribu kufanya *follow up* ili tujue. Na hii watapata kujua wala Mhe.Waziri, hatopata tabu tena ya kufuatilia hii kampuni kama ina *shares* ngapi.

Mimi ninafikiri kamati ifuatilie ili kuweza kuwalinda wadau wetu wa ndani ambao moja katika hiyo *investments* ya mahoteli kuweza kuwapatia ajira watu wetu. Na hiyo kamati vile vile itawashauri kama hawalipi kodi ya serikali, hapa tunapigia kelele mapato ya Halmashauri waweze kulipa hiyo kodi ili na wao waweze ku-s*urvive* katika hiyo kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru tuendelee.(*Makofi*)

Kifungu PD 0901 Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo Ndani ya Mkoa Shs.213,952,000/-

Kifungu PD 0902 Programu ya Utawala na Uendeshaji Shs.1,059,448,000/-

Jumla Kuu **Shs.1,273,400,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 10 MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu PD 1001 Programu Kuu ya Kuratibu

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia kwa maandishi nilizungumza kuhusu suala la kadhia ya *stand* ya magari ya Chake Chake. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, anipe kauli juu ya kadhia hii ya *stand* ya magari ya Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti: Utajibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaendelea kusisitiza taratibu. Lakini kimsingi jambo hili Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, alitoa ufafanuzi. Lakini pia jambo hili nitatolewa maelezo zaidi itakapokuja wizara hiyo.

Kwa sababu jambo hili kimsingi halipo kwenye Ofisi yangu, isipokuwa sisi ni wahusika au wadau linapotekelezwa hili jambo tunashauriana kwa kushirikiana na mipango miji na kadhalika. Kwa hivyo, maelezo ya kina kwa wajumbe wote na lilishajibiwa swali hili, wasubiri kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji waje wapate maelezo ya kina kabisa sio ofisi hii. *(Makofi)*

Mhe Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema Mkoa wa Kusini Pemba hakuna makusanyo ya mapato ambayo yanaweza kukusanywa kwa kipindi kikubwa sana. Sasa nilikuwa tu nataka kuomba ufafanuzi, kwa nini hawakusanyi wakati mikoa mingine mingi inakusanya au kama Wakuu wa Mikoa wamenuna au wengine, nataka kujua tu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alisema hivyo. Bado narudi pale pale kwenye hoja yangu kwamba muda sikupata, lakini nataka nimthibitishie kwa Wakuu wa Mikoa wale walipo hawawezi kwenda kwenye *style* hiyo ya kununa. Wanaonuna ni wengine na sio wao *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi jambo hili inaonekana wao hawakupangiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kukusanya haya mapato na kwa sababu *Revenue* yenyewe vyanzo vyake nimeviulizia. Kwanza vinatokana na ndoa ya bomani, hicho ni kianzio cha kwanza.

Kianzio cha pili, ni fomu zile za *late registration*, inaonekana kule wamekua wasamaria wema, wamekua wanazitoa na kwa sababu tu wamekua hawajaelewa utaratibu wa kukusanya mapato.Lakini kianzio chengine ni uhaulishaji wa ardhi. Kwa hivyo, tumewaomba Wizara ya Fedha katika eneo hili, lakini wamesema kwa sababu mwaka huu tayari haya mafungu yalikwishapitishwa, basi hawawezi tena, kwa sababu wakati tunalikumbuka hili jambo wakati huo na hivi vitabu vilishachapishwa. Hata hivyo, ofisi yangu kwa sababu imeshajua kwamba hizi *source* zipo basi tutazisimamia na kama yatatokea makusanyo, tutawaomba wenzetu wa Wizara ya Fedha waridhie tuzipeleke kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuongeza kima cha mapato ambayo yatakusanywa katika Mikoa yetu. Mhe Dimwa, hiyo ndio ilikua sababu kwamba wao Pemba walikua hawakusanyi pesa hizi, lakini Unguja wanakusanya pesa hizi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, lakini kitu kama hiki kinatokea hapa kodi ya serikali haikusanywi ni aibu sana kwetu na tunakwenda wapi. Ninaamini ndoa zile za bomani zipo, tufuate utaratibu Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PD1001 Programu Kuu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa	
Kifungu SD100101 Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa	50,938,000
Jumla Kuu	**50,938,000**

Kifungu PD1003 Programu Kuu ya Mipango na Utawala katika Mkoa	
Kifungu SD100301 Programu Ndogo ya Kusimamia Mipango na Utawala	1,867,488,000
Jumla Kuu	**1,918,426,000**

FUNGU D11 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu PD1101 Programu Kuu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa

Kifungu SD110101 Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba hii katika ukurasa wa 62, kifungu cha 171, niliomba waziri atakapokuja aniambie ni miradi mingapi iliyoratibiwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na mimi nielewe. Pia, nilichangia kwa maandishi kuhusu malalamiko ya Baraza la Mji Wete, kwamba hawapati likizo wala *overtime*.

Vile vile, kuna wafanyakazi mwaka wa sita huu bado ni *daily paid*, sikupata maelezo, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Shehe Hamad Mattar, alihoji suala hilo. Bado Waheshimiwa Wajumbe, watambuwe kwa nini sikupata wasaa wa kutoa ufafanuzi. Lakini ninachotaka kusema kwamba miradi hatuwezi kuijua hapa, kwa sababu miradi hii inatoka katika sekta mbali mbali. Ile miradi yote ambayo itapitishwa na sekta katika bajeti hii kwa Mkoa wa Kaskazin Pemba, ndio itakayoratibiwa na kufuatiliwa na Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa jumla.

Kwa hivyo, siwezi kujua kwa sababu hatujajua hasa hiyo miradi mingapi ambayo itakuwa kwenye Mkoa. Kuna miradi ambayo imo ndani ya bajeti hii, kuna miradi ya wananchi wenyewe, kwa hivyo, miradi hiyo ndio ambayo itaratibiwa. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe, aendelee kustahamili kukubali utaratibu kwamba miradi hiyo itatambulika pale tu bajeti hii yote tutakapokuwa tayari tumeshaipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la likizo za wafanyakazi wa Baraza la Mji. Serikali inahimiza sana kwamba mfanyakazi anapofika muda wake wa kwenda likizo aende likizo. Sasa imekuwa ni tabia ya baadhi ya wafanyakazi kutokwenda likizo. Hiyo ni kama taarifa amenipa nitakaa na uongozi ili nijuwe ni wafanyakazi gani hao ambao hawajenda likizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wafanyakazi ambao wako kwenye *daily paid*. Ni kweli katika Sheria ya Utumishi wa Umma kuna utaratibu wa mfanyakazi kufanyakazi ya *daily paid* kwa kipindi fulani. Lakini ni wafanyakazi wenyewe

saa nyengine unapowaambia kwamba masharti hayakubali, basi wanasema hawataki kuondoka bora waendelee na utaratibu huo. Kama mfanyakazi huyo anakubali na uwezo wa kumuajiri haujakuwepo na pengine nafasi anayoifanyia kazi, hana vile vigezo vya kuweza kuajiriwa. Utamfukuza kwa nguvu umwambie kuanzia leo usije kwa sababu utaratibu haukubali. Tunaweza tukafanya hivyo, lakini ni sisi wenyewe waheshimiwa tunaochaguliwa huko majimboni, tunaweza vile vile tukaja kulalamikia utaratibu huu.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana naye, na naitambua ile *concern* yake, lakini tutizame pande mbili zote za shilingi. Wananchi wetu hawa ni masikini, ni kweli wanafanyakazi ya *daily paid* kwa miaka mitatu na zaidi, tuko tayari sisi kuwaambia tuna-*phase out,* yaani tunakuondoeni. Je, tayari tumeshawaelimisha wafanyakazi, kwa sababu hili jambo tusilitizame tu tukaibebesha lawama serikali kwamba tunafanya makosa, lakini uwezo wa kuwaajiri hatuna, lakini vile vile, kwenda sisi tukawaambia wananchi ondokeni hapa kwa sababu nyinyi ni wafanyakazi wa *daily paid.* Hiyo sasa inabidi tupime sisi wenyewe wawakilishi, ni matatizo gani yatakayotokezea ndani ya jamii tunazoziongoza. Kama tunakubaliana, basi sisi mkitushauri na mkituagiza tutafuata hayo maagizo, lakini tujuwe *repossession* yake itarudi kwetu sisi kwa wawakilishi wa wananchi huko majimboni. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu SD110101	Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa	86,792,000
Jumla Kuu		**86,792,000**

Kifungu PD1103 Programu Kuu ya Mipango na Utawala katika Mkoa

Kifungu SD110301	Programu Ndogo ya Mipango na Utawala katika Mkoa	1,487,508,000
	Jumla Mkuu	**1,574,300,000**

FUNGU D12 OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu D1202

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa wakati nilipokuwa nachangia, najua Mhe. Waziri, hakupata muda wa kutoa yote. Lakini ningependa nipate maelezo japo kidogo. Kwa mwaka 2015/2016 jumla ya Wazanzibari zaidi kwenye ukurasa wake wa 40 wa

hotuba yake 8,691 walipatiwa vitambulisho kwa mwaka huo na kwa bajeti ya mwaka ule pesa zilizoidhiniswa zilikuwa bilioni 1,768,000,000 na pesa ambazo zinakadiriwa kutumia ni bilioni 100,369,000,000, lakini kwa mwaka wa fedha walipatiwa fedha milioni 600 ni sawa na asilimia 43.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa idadi ya watu ukiangalia na mazingira muhimu ya ofisi hii na pia umuhimu wa hiki kitambulisho kwa jinsi utaratibu wa nchi yetu tunavyoendesha ni kwamba huduma zote unazozihitaji za ardhi, kwenda kufungua *account* benki ni nyingi. Sasa sijui Mhe. Waziri, mmejipanga vipi katika suala hili la fedha na kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa wananchi wote.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Simai Mohamed, naielewa kwamba fedha kidogo ambazo wameingiziwa ofisi hii. Lakini jibu linabaki pale pale kwamba uwezo wa serikali kuweza kutimiza haja asilimia 100 au asilimia 50 au asilimia 70 badala ya asilimia 46 naiona na mimi ningependa iwe hivyo, na ndio maana safari hii pia tumekuja na bajeti yetu hii ili tuweze kuikisia na kuomba fedha serikalini tuweze kufanyaka majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuhakikishia Mhe. Mjumbe, kwamba kila mwenye haki ya kusajiliwa Mzanzibari yeyote ambaye ametimiza masharti kwa mujibu wa sheria, basi huyo mtu ataendelea kusajiliwa kama tulivyofanya huko nyuma, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini pia utaratibu unaotumika wakati mwengine kwenye taasisi tofauti na kutokana na ufinyu wa hii bajeti. Zipo taasisi huwa zinatolewa fedha kwa *monthly* na ziko ambazo zinatolewa kwa *quarterly* ambazo zinakwenda kwa miezi mitatu. Sasa sijui katika ofisi hii hizi fedha hutiwa kwa kila mwezi au kwa kila baada ya miezi mitatu au minne. Ningeomba kupata maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, *OC* ya wizara hii inatiwa kwa mwezi na bahati nzuri hapa hapawezi kuwa na dhana yoyote ile pengine labda wizara inawanyima. Kwa sababu hii ni *vote* na fedha zao zinakwenda moja kwa moja, wala hazipiti wizarani wanapelekewa wenyewe, lakini wanapelekewa kutokana na hali halisi ya mapato ya serikali na ugawaji wa *ceilings* zinazopelekwa wizarani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea sisi kuhakikisha kwamba wanapata fedha ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria zilizopo. Lakini hiyo ndio hali halisi, sisi hatupendi kwamba taasisi zetu zikose fedha kwa ajili ya kufanyia kazi zao na hasa taasisi hizi mbili; Taasisi ya Vizazi na Vifo na Taasisi ya Kadi za Vitambulisho. Kwa hivyo, kutokana na hali ilivyo ndio pesa hiyo iliyopatikana, lakini tumewaomba serikali na wanajua kwamba fedha walizotuingizia sio mahitaji yetu ni kidogo zaidi, ndio maana wamekubali makisio haya kwa mwaka huu, ahsante sana.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, amejipanga vizuri leo, nampongeza kwa hilo. Kwa hivyo, ninachokiomba ni kuwa ahakikishe tu kwamba hii haki ambayo sasa hivi kwa mwenendo tunaokwenda nchi yetu, yaani watu wote wanatarajia kupata hii kadi na ziendelee na hizo fedha ambazo hizi taasisi inazipata waendelee. Kwa hivyo, naomba tuendelee, ahsante sana.

Kifungu D1202	Utawala	35,926,000,000
Kifungu D1203	Ofisi ya Mrajisi Vizazi na Vifo	239,504,000
	Jumla Kuu	**275,430,000,000**

FUNGU D12 OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu PD1201	Programu Kuu ya Kusajili na Kutoa Vitambulisho kwa Wazanzibari wote na wasiokuwa Wazanzibari wanaoishi kisheria	
Kifungu SD120101	Programu Kuu ya Kusajili na Kutoa Vitambulisho kwa Wazanzibari wote na wasiokuwa Wazanzibari wanaoishi kisheria	75,000,000
	Jumla Kuu	**75,000,000**

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu kwenye hotuba hii, nilimtaka Mhe. Waziri, atakapokuja anieleze juu ya hawa wasiokuwa Wazanzibari kuhusiana na suala zima la vitambulisho. Nashukuru katika ufafanuzi wake wa hoja, alisema kwamba zoezi hili halijakwenda.

Vile vile, pamoja na kutaka idadi, mimi nilitaka vigezo ambavyo vitatumika katika kuwapatia vitambulisho watu hawa wasiokuwa Wazanzibari, lakini

wakaazi wanaoishi hapa kisheria. Kwa hivyo, ningependa achukuwe fursa hiyo kuweza kunipa ufafanuzi wa vigezo ambavyo vitatumika katika utoaji wa vitambulisho kwa hawa watu wasiokuwa Wazanzibari wanaoishi hapa kisheria, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, kwa suala lake. Mhe. Mwenyekiti, vigezo vipo kwa mujibu wa sheria na kanuni, ndio maana tunasema tutawasajili wageni waliokuwa sio Wazanzibari wanaoishi kisheria.

Kwa hivyo, kigezo cha kwanza uwe si Mzanzibari, uwe mgeni, lakini umeingia hapa nchini na unaishi kisheria. Ukishakuwa na kigezo hicho basi sisi tutakusajili na kuna mambo mengine tutayafanya ikiwa utakuwa raia mwema, huna makosa ya kijinai huko unakotoka na mambo mengine. Kwa hivyo, vigezo ni hivyo kwamba ukishakua mtu, huko ulikotoka huna makosa ya kijinai na umeingia hapa kisheria, na unaishi basi tutakusajili ili tukutambuwe wakati ukiwa unaishi hapa, idadi kama nilivyosema kwa sababu zoezi hili halijaanza mpaka sasa hatuna idadi ya namba ya watu ambao tumewasajili, ahsante sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

	Jumla Kuu	**75,000,000**
Kifungu PD1202	Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	
Kifungu SD120201	Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	1,240,696,000
Kifungu SD120202	Ofisi Kuu Pemba	245,401,000
	Jumla Kuu	**1,486,100,000**
Kifungu PD1203	Programu Kuu ya Kusajili Matukio ya Kijamii	
Kifungu SD120301	Programu Ndogo Kusajili Matukio ya Kijamii	528,800,000
	Jumla Kifungu	**528,800,000**
	Jumla Kuu	**2,089,900,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ilivyokua Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ametoa hoja. Sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe fursa hii adhimu kwanza kuwashukuru sana nyote kwa utulivu wenu, lakini vile vile kwa michango mbali mbali ambayo imetolewa hapa. Pia, niwashukuru na watendaji wote walioko juu ambao wametulia kwa muda mrefu na kuhakikisha kwamba bajeti ya wizara zao na vitengo vyao imeweza kupita kwa ajili ya matumizi.

Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hadi kesho tarehe 07/06/2016 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 3:59 usiku Kikao kiliahirishwa mpaka
tarehe 07/06/2016 saa 3:00 za asubuhi)